MANENO YALIYOTEULIWA YA MWENYEKITI MAO TSETUNG

WAFANYA KAZI WA NCHI ZOTE
UNGANENI!

MANENO YALIYOTEULIWA YA MWENYEKITI MAO TSETUNG

★

OFISI YA UCHAPAJI WA LUGHA ZA KIGENI
PEKING 1972

Kimepigwa chapa katika Jamhuri ya Watu wa China

YALIYOMO

1.	Chama cha Kikoministi	1
2.	Matabaka na Mapigano ya Kitabaka	9
3.	Usoshalisti na Ukoministi	25
4.	Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma	51
5.	Vita na Amani	65
6.	Wabeberu na Wapinga Maendeleo Wote Ni Chui wa Karatasi	80
7.	Kuthubutu Kupigana na Kuthubutu Kushinda	91
8.	Vita vya Umma	98
9.	Jeshi la Umma	110
10.	Uongozi wa Kamiti za Chama	115
11.	Msimamo wa Kiumma	130
12.	Kazi ya Kisiasa	148

13. Mahusiano Baina ya Maofisa na Maaskari 163
14. Mahusiano Baina ya Jeshi na Umma 168
15. Demokrasi Katika Mambo Matatu Muhimu 172
16. Uelimishaji na Ufundishaji wa Vikosi 180
17. Kutumikia Umma 185
18. Hisia za Kiwananchi na Udugu wa Kilimwengu 190
19. Ushujaa wa Kimapinduzi 197
20. Kujenga Nchi Yetu kwa Bidii na Bila ya Isirafu 202
21. Kujitegemea Wenyewe na Kufanya Jitihada kwa Ushupavu 211
22. Njia za Kufikiri na Njia za Kufanya Kazi 221
23. Uchunguzi na Masomo 251
24. Kusahihisha Mawazo ya Makosa 259
25. Umoja 275
26. Nidhamu 278

27.	Kutoa Makosa na Kujitoa Makosa	283
28.	Wakoministi	294
29.	Makada	304
30.	Vijana	317
31.	Wanawake	323
32.	Utamaduni na Sanaa	329
33.	Masomo	335

1. CHAMA CHA KIKOMINISTI

Kiini cha nguvu zinazoongoza jihadi yetu ni Chama cha Kikoministi cha China. Msingi wa nadharia [*theory*] unaoelekeza fikra zetu ni Umarx-lenin.

Hotuba ya ufunguzi katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Mwanzo la Umma la Taifa la Jamhuri ya Watu wa China (Septemba 15, 1954).

Kwa ajili ya kuwepo mapinduzi, ni lazima kiwepo chama cha kimapinduzi. Bila ya chama cha kimapinduzi, bila ya chama kilichojengwa kwa nadharia ya kimapinduzi ya Kimarx-lenin na mtindo wa kimapinduzi wa Kimarx-lenin, ni muhali kuongoza

tabaka la wafanya kazi na umma mkubwa wa watu katika kuushinda ubeberu na vijibwa vyake.

"Nguvu za Kimapinduzi za Dunia Nzima Unganeni, Piganeni na Ushambulizi wa Kibeberu!" (Novemba 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Bila ya jitihada za Chama cha Kikoministi cha China, bila ya Wakoministi wa China kuwa nguzo ya watu wa China, China maisha haiwezi kupata uhuru na ukombozi, au kutekeleza uenezi wa makarahana na kufanya ukulima wake kuwa wa kisasa.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Chama cha Kikoministi cha China ni kiini cha uongozi wa watu wote wa China.

Bila ya kiini kama hicho, jihadi ya usoshalisti haiwezi kufanikiwa.

Mazungumzo kwenye mkutano wa kuwapokea wajumbe wa Baraza la Taifa la Tatu la Umoja wa Vijana wa Demokrasi Mpya wa China (Mei 25, 1957).

Chama chenye nidhamu kilichozatitiwa na nadharia ya Kimarx-lenin, kitumiacho njia ya kujitoa makosa na kujiunganisha na umma wa watu; jeshi lililo chini ya uongozi wa Chama kama hicho; muungano wa pamoja wa matabaka yote ya kimapinduzi na makundi yote ya kimapinduzi chini ya uongozi wa Chama kama hicho — hizi ndio silaha tatu kubwa tulizowashindia maadui.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Lazima tuuamini umma, lazima tukiamini Chama. Hizi ni kanuni mbili za

msingi. Tukizitilia shaka kanuni hizi mbili hatutofanikiwa katika jambo lo lote.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Kikijizatiti na nadharia na fikra za Kimarx-lenin, Chama cha Kikoministi cha China kimeleta mtindo mpya wa kufanya kazi miongoni mwa watu wa China, mtindo wa kazi ambao kiini chake ni kuunganisha mawazo na vitendo, kujifungamanisha vyema na umma na kufuata njia ya kujitoa makosa.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ni muhali kwa chama cha kisiasa kuweza kuongoza vugu vugu kubwa la kimapinduzi mpaka ushindi bila ya kuwa na

nadharia ya kimapinduzi na ujuzi wa historia na kufahamu barabara vugu vugu lenyewe.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kama tulivyokuwa tukisema, vugu vugu la masahihisho ni "vugu vugu lililotapakaa la elimu ya Kimarx". Masahihisho maana yake ni kwamba Chama kizima kinajifunza Umarx kwa njia ya kutoa na kujitoa makosa. Hakika, tunaweza kujifunza Umarx zaidi katika mwenendo wa vugu vugu la masahihisho.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Ni kazi ngumu mno kuhakikisha maisha bora kwa mamia ya milioni ya watu wa China na kuijenga nchi yetu iliyo nyuma katika uchumi na utamaduni kuwa nchi

iliyostawi na yenye nguvu ikiwa na daraja ya juu ya utamaduni. Kwa hivyo, ili tuweze kuibeba kazi hii kwa urahisi kidogo na kufanya kazi vizuri zaidi pamoja na watu wote wasio wanachama ambao wana malengo makuu na kuazimu kuleta mabadiliko, lazima tufanye mavugu vugu ya masahihisho kwa hivi sasa na katika siku za mbele, na kwa namna hiyo daima tutajiondoshea kila kisicho barabara.

Kama juu.

Siasa ndio chanzo cha vitendo hasa vyote vya chama cha kimapinduzi na hujionyesha katika mwendo na matokeo ya vitendo vya chama hicho. Chama cha kimapinduzi hutekeleza siasa kila kifanyapo jambo. Kama hakitekelezi siasa iliyo barabara, basi kinatekeleza siasa isio barabara; kama hakitekelezi siasa fulani kwa kufahamu kifanyavyo, basi hufanya hivyo kwa upofu. Kile tunachokiita maarifa, ni mwendo na matokeo ya kutekeleza siasa. Kwa kupitia vitendo vya watu tu, yaani,

kwa kupitia maarifa, ndio tutaweza kuhakikisha kama siasa hiyo ni sahihi au ya makosa na kuamua kwa kiwango gani ni sahihi au ya makosa. Lakini vitendo vya watu, hususan vitendo vya chama cha kimapinduzi na umma wa kimapinduzi, havina budi ila kuambatana na siasa moja au nyengineyo. Kwa hivyo, kabla ya kitendo cho chote kufanywa, lazima tuwaeleze wanachama wa Chama na umma siasa tulioitunga kwa mujibu wa hali ilivyo. Kama si hivyo, wanachama wa Chama na umma wataachana na uongozi wa siasa yetu, watatenda mambo kwa upofu na kufuata siasa isio barabara.

"Juu ya Siasa ya Makarahana na Biashara" (Februari 27, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Chama chetu kimeweka msimamo mkuu na siasa kuu kwa mapinduzi ya China na vile vile misimamo maalum ya kazi na siasa maalum mbali mbali. Lakini, makomredi wengi mara nyingi hukumbuka

misimamo maalum ya kazi na siasa maalum za Chama chetu, na husahau msimamo mkuu na siasa kuu. Ikiwa kwa kweli tunasahau msimamo mkuu na siasa kuu ya Chama, basi tutakuwa wana-mapinduzi vipofu, wasiopevuka na wapumbavu; na tunapofuata msimamo maalum wa kazi na siasa maalum, tutapoteza muelekeo wetu na kuyumba yumba mara kushoto mara kulia, na kazi itaathirika.

"Hotuba Kwenye Mkutano wa Makada Katika Eneo Lililokombolewa la Shansi-Suiyuan" (Aprili 1, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Siasa na mbinu ndio maisha ya Chama; makomredi viongozi wa daraja zote lazima wayaangalie kwa makini mambo haya mawili na kabisa wasiyapuuze kwa hali yo yote ile.

"Barua Juu ya Hali ya Mambo" (Machi 20, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

2. MATABAKA NA MAPIGANO YA KITABAKA

Matabaka yanapigana, baadhi ya matabaka yanafaulu, na mengine yanafyekwa. Hivyo ndivyo ilivyo historia, hivyo ndivyo ilivyo historia ya ustaarabu kwa maelfu ya miaka. Kuifasiri historia kwa mtizamo huu ni uyakinifu wa kihistoria [*historical materialism*]; kusimama kinyume na mtizamo huu ni udhanifu wa kihistoria [*historical idealism*].

"Ondosheni Ndoto, Jitayarisheni kwa Mapigano" (Agosti 14, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika jamii ya matabaka kila mtu anaishi kama mtu wa tabaka maalum, na

kila aina ya fikra, bila ya mbaguo wo wote, inapigwa muhuri wa kitabaka.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Mabadiliko katika jamii yanatokana hasa na ukuaji wa hitilafu za ndani ya jamii, yaani hitilafu baina ya nguvu za uchumi na mahusiano ya uchumi, hitilafu baina ya matabaka na hitilafu baina ya kitu kikongwe na kipya; ni ukuaji wa hitilafu hizi ndio unaopeleka mbele jamii na kuleta jamii mpya kukamata mwahala pa jamii kongwe.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Unyonyaji damu wa kiuchumi na ukandamizaji wa kisiasa wa kihabithi wanaofanyiwa wakulima na tabaka la mabwanashamba uliwalazimisha kufanya miinuko mara kwa mara ya kupinga utawala wa tabaka la mabwana-shamba. . . . Ni jihadi

za kitabaka za wakulima, miinuko ya wakulima na vita vya wakulima ndizo nguvu hasa zilizopeleka mbele maendeleo ya historia katika jamii ya kimwinyi ya China.

"Mapinduzi ya China na Chama cha Kikoministi cha China" (Desemba 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika uchambuzi wa mwisho, mapigano ya kitaifa ni suala la mapigano ya kitabaka. Katika Marekani wale wanaowakandamiza watu weusi ni vikundi vya watawala wa kipinga maendeleo tu miongoni mwa watu weupe. Kwa namna yo yote ile vikundi hivyo haviwezi kuwawakilisha wafanya kazi, wakulima, wataalamu wa kimapinduzi na watu wengine wenye fikra za uongofu ambao ndio sehemu kubwa ya watu weupe.

"Taarifa ya Kuunga Mkono Watu Weusi wa Kimarekani Katika Mapigano Yao ya Haki Dhidi ya Ubaguzi wa Rangi Unaofanywa na Ubeberu wa Kimarekani" (Agosti 8, 1963), *Watu wa Ulimwengu, Unganeni na Muwashinde Washambulizi wa Kimarekani na Vibaraka Vyao Vyote.*

Ni juu yetu sisi kuukusanya pamoja umma. Kuhusu wapinga maendeleo katika China, ni juu yetu sisi kuukusanya umma kuwapindua. Kitu cho chote kipingacho maendeleo ni namna moja; kama hukipigi, basi hakianguki. Hii vile vile ni kama kufagia sakafu; kwa kawaida, pale usipofika ufagio, vumbi halitoondoka wenyewe.

"Hali ya Mambo na Siasa Yetu Baada ya Ushindi Katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Agosti 13, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Adui hatotoweka kwa hiari yake. Si wapinga maendeleo wa Kichina wala si nguvu za kishambulizi za ubeberu wa Kimarekani katika China ambazo zitatoweka katika jukwaa la historia kwa hiari yao.

"Endeleza Mapinduzi Mpaka Mwisho" (Desemba 30, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Mapinduzi si kufanya karamu, au kuandika insha, au kuchora picha, au kutia tarizi; mapinduzi hayawezi kuwa yenye makini kama hivyo, yenye utulivu na uungwana kama hivyo, yenye upole, huruma, adabu, unyenyekevu na heshima kama hivyo. Mapinduzi ni uasi, kitendo cha utumiaji nguvu cha tabaka moja kulipindua jengine.

"Ripoti Juu ya Uchunguzi wa Vugu Vugu la Wakulima wa Hunan" (Machi 1927), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Chiang Kai-shek siku zote anajaribu kuwapokonya watu hata chembe ya nguvu na kila wakia ya faida. Na sisi jee? Siasa yetu ni kupigana naye pigo kwa pigo na kuipigania kila inchi ya ardhi. Sisi tunatenda kwa kufuata anavyofanya Chiang Kai-shek. Kila siku anajaribu kuwatwisha watu vita, akishika upanga mmoja katika mkono wake wa kushoto na mwengine mkono wa kulia. Sisi vile vile tunachukua

panga kwa kufuata mfano wake. . . . Ilivyokuwa Chiang Kai-shek sasa ananoa panga zake, lazima tunoe zetu vile vile.

"Hali ya Mambo na Siasa Yetu Baada ya Ushindi Katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Agosti 13, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Nani maadui zetu? Nani marafiki zetu? Hili ni suala muhimu kabisa katika mapinduzi. Mapigano yote ya kimapinduzi yaliotangulia katika China yalipata mafanikio machache sana; sababu kubwa ni kwamba wana-mapinduzi walishindwa kuungana na marafiki zao wa kweli ili kuwashambulia maadui zao wa kweli. Chama cha kimapinduzi ni kiongozi wa umma, na wala hapana mapinduzi yo yote yawezayo kufanikiwa pindi chama cha kimapinduzi kikiongoza umma kwenye njia iliopotoka. Ili kuhakikisha kwamba sisi hatutayaongoza mapinduzi yetu kwenye njia isio barabara bali tupate mafanikio ya hakika, lazima tufanye uangalifu mkubwa wa kuungana na marafiki zetu wa kweli ili

kuwashambulia maadui zetu wa kweli. Kwa ajili ya kuweza kuwapambanua marafiki wa kweli na maadui wa kweli, inatupasa tufanye uchambuzi wa jumla wa hali za uchumi za matabaka mbali mbali katika jamii ya China na tabia yao kuhusu mapinduzi.

"Uchambuzi wa Matabaka Katika Jamii ya China" (Machi 1926), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Maadui zetu ni wote wale wanaoshirikiana na ubeberu, yaani mabwana-vita, mabwana-serikali, tabaka la madalali wa makampuni ya kigeni, tabaka la mabwana-shamba wakubwa na sehemu ipingayo maendeleo miongoni mwa wataalamu ambayo inawategemea. Nguvu ya uongozi katika mapinduzi yetu ni tabaka la wafanya kazi wa makarahana. Marafiki zetu wa karibu sana ni tabaka lote la nusu wafanya kazi na tabaka la mabepari wadogo. Ama tabaka la mabepari wastani wanaoyumba yumba, sehemu ya upande wake wa kulia huenda ikawa maadui zetu na sehemu yake

ya upande wa kushoto huenda ikawa marafiki zetu — lakini ni lazima daima tuwe na hadhari, na tusiwaruhusu kuleta mbabaiko miongoni mwetu.

Kama juu.

Ye yote anayekuwa upande wa watu wa kimapinduzi ni mwana-mapinduzi. Ye yote anayekuwa upande wa ubeberu, umwinyi na ubepari mabwana-serikali ni mpinga mapinduzi. Ye yote anayekuwa upande wa watu wa kimapinduzi kwa mdomo tu na kufanya vyenginevyo ni mwana-mapinduzi wa mdomo. Ye yote anayekuwa upande wa watu wa kimapinduzi sio kwa maneno tu bali pia kwa vitendo ni mwana-mapinduzi kamili.

Hotuba ya ufungaji katika Mkutano wa Pili wa Kamiti ya Kwanza ya Taifa ya Baraza la Kushauriana Siasa la Watu wa China (Juni 23, 1950).

Nafikiria ni jambo baya kwetu inapokuwa mtu, chama cha kisiasa, jeshi au shule

haishambuliwi na adui, kwani hapo hakika itakuwa na maana kwamba tumeshuka chini kuwa sawasawa na adui. Ni jambo zuri pindi tukishambuliwa na adui kwani hapo itathibitisha kuwa tumeweka mpambanuo wazi baina ya adui na sisi wenyewe. Ni jambo bora zaidi ikiwa adui atatushambulia kiwazimu na kutuzulia kila maovu bila ya kutupa hata sifa moja, kwani hapo itaonyesha kwamba si kama tumeweka mpambanuo wazi tu baina ya adui na sisi wenyewe, bali vile vile tumepata mafanikio makubwa katika kazi yetu.

Kupingwa na Adui Si Jambo Baya Bali Ni Jambo Zuri (Mei 26, 1939).

Inatupasa tuunge mkono kila kinachopingwa na adui na tupinge kila kinachoungwa mkono na adui.

"Mazungumzo na Waandishi Habari Watatu Kutoka Shirika Kuu la Utoaji Habari, *Sao Tang Pao* na *Hsin Min Pao*" (Septemba 16, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Msimamo wetu ni ule wa tabaka la kifanya kazi na umma wa watu. Kwa wanachama wa Chama cha Kikoministi, jambo hili lina maana ya kufuata msimamo wa Chama, kufuata moyo wa Chama na siasa ya Chama.

"Mazungumzo Katika Mkutano wa Yenan wa Mambo ya Uandishi na Sanaa" (Mei 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Baada ya kufyekwa maadui wenye bunduki, bado watakuwepo maadui wasiokuwa na bunduki; wao hawana budi kupigana nasi kiwazimu na daima tusiwadharau maadui hawa. Kama sasa hatuliweki wazi na kulifahamu suala hili, basi tutafanya makosa makubwa kabisa.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949). *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Wabeberu na wapinga maendeleo wa nchini hakika hawatokubali kushindwa

kwao bali watapigana mpaka mwisho wao. Baada ya kuweko amani na utulivu nchini kote, wao bado watajishughulisha na mambo ya uharibifu na kuleta michafuko kwa njia mbali mbali na watajaribu kila siku na kila dakika kurejesha utawala wao katika China. Hili ni jambo la lazima na la hakika, na kwa hali yo yote tusiregeze uangalifu wetu.

Hotuba ya ufunguzi katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Baraza la Kushauriana Siasa la Watu wa China (Septemba 21, 1949).

Katika China, ijapokuwa mageuzo ya kisoshalisti kuhusu mpango wa kumiliki kwa jumla yamemalizika na ijapokuwa mapigano ya kitabaka ya umma yaliyo makubwa na makali kama dharuba na kimbunga yaliokuweko katika nyakati zilizopita za kimapinduzi kwa jumla yameshasita, lakini bado yako masalio ya matabaka yaliopinduliwa ya mabwanashamba na madalali wa makampuni ya kigeni, bado lipo tabaka la mabepari, na

utengezaji wa fikra za mabepari wadogo ndio kwanza umeanza. Mapigano ya kitabaka bado hayajesha hata chembe. Mapigano ya kitabaka baina ya wafanya kazi na mabepari, mapigano ya kitabaka baina ya nguvu mbali mbali za kisiasa, na mapigano ya kitabaka katika mambo ya kifikra baina ya wafanya kazi na mabepari yataendelea kuwa marefu na yenye mazonge mazonge na baadhi ya wakati hata yatakuwa makali sana. Tabaka la wafanya kazi linataka kuigeuza dunia kwa mujibu wa mtizamo wake wa kilimwengu na tabaka la mabepari pia linataka jambo hili hili. Katika jambo hili, suala la upi utakaoshinda, usoshalisti au ubepari, kwa kweli bado halijatanzuliwa.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Itachukua muda mrefu sana kukata shauri kama upi utakaoshinda katika mapigano ya kifikra baina ya usoshalisti na ubepari katika nchi yetu. Sababu ni kuwa

taathira za tabaka la mabepari na za wataalamu watokao katika jamii kongwe zitabakia nchini kwetu kwa muda mrefu ujao, na pia fikra zao za kitabaka zitabakia kwa muda mrefu ujao. Kama hali hii haifahamiki kwa kutosha, au haifahamiki kabisa, makosa makubwa yatafanywa na haja ya kufanya mapigano ya kifikra itapuuzwa.

Kama juu.

Katika nchi yetu, fikra za matabaka ya mabepari na mabepari wadogo, fikra zipingazo Umarx, zitaendelea kudumu kwa muda mrefu. Kwa msingi, mpango wa kisoshalisti umeanzishwa katika nchi yetu. Tumepata ushindi wa msingi katika kugeuza mpango wa kumiliki njia za uchumi, lakini bado hatujapata ushindi kamili katika medani ya siasa na ya fikra. Katika upande wa fikra, suala la nani atakayeshinda katika mapigano baina ya tabaka la kifanya kazi na tabaka la kibepari bado halijatanzuliwa hasa. Bado inatubidi tufanye

mapigano marefu dhidi ya fikra za matabaka ya mabepari na mabepari wadogo. Ni makosa kutolifahamu jambo hili na kuyawacha mapigano ya kifikra. Fikra zote za makosa, magugu yote ya sumu, mashetani na majini wote lazima watolewe makosa; kwa hali yo yote ile yasiachiliwe kutapakaa bila ya kuzuiliwa. Juu ya hivyo, utoaji makosa lazima uwe na sababu kamili, wa uchambuzi na unaoingia akilini, na sio wa ukali, wa ubwanamkubwa, wa *metaphysics* au wa kufuata kikasuku maneno ya vitabuni.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Ufuataji kikasuku maneno ya vitabuni na ubadilishaji fikra ni mambo yanayokwenda kinyume na Umarx. Hakika Umarx lazima uende mbele; lazima ukue kwa kuambatana na ukuaji wa vitendo vya watu na hauwezi kubakia papo hapo. Utakuwa hauna uhai ikiwa hautosonga mbele na kukariri mambo yale kwa yale. Lakini juu ya hivyo,

kanuni za msingi za Umarx maisha zisivunjwe, ama si hivyo makosa yatafanywa. Ni ufuataji maneno ya vitabuni kikasuku kuukabili Umarx kwa mtizamo wa *metaphysics* na kuufikiria kama ni kitu kilichong'ang'anaa. Ni ubadilishaji fikra kuzikanusha kanuni za msingi za Umarx na kuukanusha ukweli wake unaofaa po pote ulimwenguni. Ubadilishaji fikra ni aina moja ya fikra za kibepari. Wabadilishaji fikra wanakanusha tofauti zilizoko baina ya usoshalisti na ubepari, baina ya udikteta wa tabaka la kifanya kazi na udikteta wa tabaka la kibepari. Wanachokitetea hasa kusema kweli si msimamo wa kisoshalisti bali msimamo wa kibepari. Katika hali ya hivi sasa, ubadilishaji fikra ni hatari zaidi kuliko ufuataji kikasuku maneno ya vitabuni. Mojawapo ya kazi zetu muhimu za hivi sasa katika medani ya kifikra ni kuanza kuuponda ubadilishaji fikra.

Kama juu.

Ubadilishaji fikra, au upotovu [*opportunism*] wa Upande wa Kulia, ni mwelekeo

wa fikra za kibepari ambao ni hatari zaidi kuliko ufuataji kikasuku maneno ya vitabuni. Wabadilishaji fikra, wapotovu wa Upande wa Kulia, wanabobozokwa tu maneno ya Umarx; wao vile vile wanashambulia "ufuataji kikasuku maneno ya vitabuni". Lakini wanachokishambulia hasa ni misingi muhimu kabisa ya Umarx. Wao wanapinga au kupotoa uyakinifu na upembuzi [*dialectics*], wanapinga au wanajaribu kudhoofisha udikteta wa kidemokrasi wa umma na uongozi wa Chama cha Kikoministi, na wanapinga au wanajaribu kudhoofisha mageuzo ya kisoshalisti na ujenzi wa kisoshalisti. Baada ya ushindi wa msingi wa mapinduzi ya kisoshalisti katika nchi yetu, bado wako baadhi ya watu ambao wanaota ndoto za kuurejesha mpango wa kibepari na kupigana na tabaka la wafanya kazi katika kila medani, pamoja na ile ya kifikra. Na katika mapigano haya wasaidizi wao wakuu ni wabadilishaji fikra.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

3. USOSHALISTI NA UKOMINISTI

Ukoministi ni utaratibu kamili wa fikra za kifanya kazi na kwa wakati ule ule ni mpango mpya wa kijamii. Nao ni tofauti na utaratibu wo wote mwengineo wa kifikra na mpango wo wote mwengineo wa kijamii, na ndio utaratibu na mpango uliokamilika, wa maendeleo, wa kimapinduzi na wa busara kuliko yote katika historia ya binadamu. Utaratibu wa kifikra na mpango wa kijamii wa kimwinyi hauna mwahala unapofaa isipokuwa kwenye makumbusho ya historia tu. Utaratibu wa kifikra na mpango wa kijamii wa kibepari vile vile umekuwa ni kitu cha makumbusho katika sehemu moja ya dunia (katika Umoja wa Soviet), na katika nchi nyengine unafanana na "mtu anayekata roho

akizama kwa haraka sana, kama jua linavyotua katika upande wa pili wa milima ya magharibi", na karibu utatupwa katika makumbusho. Utaratibu wa kifikra na mpango wa kijamii wa kikoministi peke yake tu ndio uliojaa ujana na hamasa na unaikumba dunia kwa kasi kubwa za mporomoko wa theluji na nguvu za radi.

"Juu ya Demokrasi Mpya" (Januari 1940), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mwishowe mpango wa kisoshalisti utachukua mwahala pa mpango wa kibepari; hii ni kanuni hasa ya mambo ambayo haitegemei matakwa ya mtu. Hata wapinga maendeleo wakijaribu kwa namna gani kulirejesha nyuma gurudumu la historia, hapana budi mapinduzi yatatokea karibuni au baadaye, na bila ya shaka yo yote yatashinda.

"Hotuba Katika Mkutano wa Bunge Kuu la Umoja wa Soviet kwa Kusherehekea Kutimia Miaka Arobaini Tangu Mapinduzi Makubwa ya Kisoshalisti ya Oktoba" (Novemba 6, 1957).

Sisi Wakoministi maisha hatufichi maoni yetu ya kisiasa. Hakika na bila ya shaka, lengo letu la siku zijazo au kipeo cha mipango yetu ni kuipeleka mbele China kuendea kwenye usoshalisti na ukoministi. Jina la Chama chetu na mtizamo wetu wa Kimarx kuhusu ulimwengu bila ya mbabaisho wo wote unaelekezea azma yetu hii ya juu kabisa ya siku za mbele, mustakbala wenye mng'aro na uzuri mkubwa usio na mfano.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Tukilichukua kwa jumla, vugu vugu la mapinduzi ya China linaloongozwa na Chama cha Kikoministi lina daraja mbili, yaani mapinduzi ya kidemokrasi na mapinduzi ya kisoshalisti, daraja ambazo kwa msingi ni hatua mbili tofauti za kimapinduzi na kwamba hatua ya pili inaweza kuchukuliwa baada ya kumalizwa tu hatua ya kwanza. Mapinduzi ya kidemokrasi ni

matayarisho ya lazima kwa ajili ya mapinduzi ya kisoshalisti na mapinduzi ya kisoshalisti ni jambo lifuatalo lisiloepukika la mapinduzi ya kidemokrasi. Shabaha ya mwisho ambayo wanaipigania Wakoministi wote ni kuileta jamii ya kisoshalisti na ya kikoministi.

"Mapinduzi ya China na Chama cha Kikoministi cha China" (Desemba 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mapinduzi ya kisoshalisti yanakusudia kuzikomboa nguvu za uchumi. Ugeuzaji kutoka umilikiaji wa kibinafsi kuendea umilikiaji wa shirika wa kisoshalisti katika kilimo na kazi za mikono na kutoka umilikiaji wa kibepari kuendea umilikiaji wa kisoshalisti katika makarahana na biashara za watu binafsi hauna budi kuleta ukombozi mkubwa wa nguvu za uchumi. Kwa njia hii zinaletwa hali mpya za kijamii kwa ajili ya ukuaji mkubwa wa uchumi wa makarahana na ukulima.

Hotuba katika Baraza Kuu la Dola (Januari 25, 1956).

Sasa tunafanya mapinduzi sio katika mpango wa kijamii tu, yaani mgeuko kutoka umilikiaji wa kibinafsi kuendea umilikiaji wa watu wote, lakini vile vile katika mambo ya ufundi, yaani mabadiliko kutoka kazi za mikono kuendea utoaji mkubwa wa vitu wa kisasa kwa kutumia mashine, na mapinduzi haya mawili yamefungamana. Katika ukulima, kwa hali tulizo nazo katika nchi yetu, ushirika lazima uutangulie utumiaji wa mashine kubwa (katika nchi za kibepari ukulima unaendelea kwa njia ya kibepari). Kwa hivyo kwa namna yo yote tusichukulie makarahana na kilimo, uenezaji wa makarahana wa kisoshalisti na mgeuko wa kilimo wa kisoshalisti kama ni vitu viwili mbali mbali na vinavyotengana, na kwa hali yo yote tusitilie nguvu kimoja na kukifanya duni chengine.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Mpango mpya wa kijamii ndio kwanza umesimamishwa na unahitaji muda kwa

ajili ya kuimarishwa kwake. Isidhaniwe kwamba mpango huu mpya unaweza kuimarishwa kabisa mara tu baada ya kuanzishwa, kwani jambo hilo ni muhali. Inabidi kuimarishwa hatua baada ya hatua. Kwa kuweza kuuimarisha kamili, si kama ni lazima tu kuleta uenezaji wa makarahana wa kisoshalisti nchini na kuendeleza mapinduzi ya kisoshalisti katika medani ya uchumi, bali pia kufanya jihadi ya kimapinduzi ya kisoshalisti na uelimishaji wa kisoshalisti usiosita na mgumu katika medani ya siasa na fikra. Zaidi ya hayo, mambo kadha ya ulimwengu yanahitajika kusaidia jambo hili.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Katika China mapigano ya kuimarisha mpango wa kisoshalisti, mapigano ya kuamua kama usoshalisti au ubepari utashinda, bado yatachukua muda mrefu wa historia. Lakini lazima sote tutambue

kwamba mpango mpya wa kisoshalisti bila ya wasi wasi wo wote utaimarishwa. Kwa hakika tunaweza kulijenga taifa la kisoshalisti lenye makarahana ya kisasa, kilimo cha kisasa, na sayansi na utamaduni wa kisasa.

Kama juu.

Idadi ya wataalamu ambao wanaitizama kwa jicho baya dola yetu ni ndogo sana. Wao hawaipendi dola yetu ya udikteta wa kifanya kazi na wana hamu ya jamii kongwe. Wakati wo wote patapotokea fursa, wao wataleta matata na kujaribu kukipindua Chama cha Kikoministi na kuirejesha China kongwe. Ama baina ya njia ya kifanya kazi na ya kibepari, baina ya njia ya usoshalisti na ya ubepari, watu hawa kwa ukaidi wanachagua kuifuata njia ile ya mwisho. Kusema kweli, njia hii ni muhali, na kwa hivyo, kwa kweli wao wako tayari kusalim amri kwa ubeberu, umwinyi na ubepari wa mabwana-serikali. Watu kama hao wanaonekana katika makundi ya siasa, ya makarahana na biashara,

ya utamaduni na elimu, ya sayansi na ufundi na ya dini, na ni wapinga maendeleo kabisa.

Kama juu.

Tatizo kubwa ni kuwaelimisha wakulima. Uchumi wa wakulima umetawanyika, na — kwa mujibu wa maarifa ya Umoja wa Soviet — kufanya kilimo kuwa cha kisoshalisti kutahitaji wakati mrefu na bidii kubwa. Bila ya kufanya kilimo kuwa cha kisoshalisti basi hapatokuweko usoshalisti kamili na imara.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Lazima tuamini, kwanza, kwamba umma mkubwa wa wakulima uko tayari kusonga mbele hatua baada ya hatua kwenye njia ya usoshalisti chini ya uongozi wa Chama, na pili, kwamba Chama kina uwezo wa kuwaongoza wakulima kwenye njia hii.

Mambo haya mawili ni kiini cha mambo na mkondo muhimu.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Vikundi vya uongozi katika vyama vya ushirika lazima vihakikishe kwamba wakulima masikini waliopo sasa na wakulima wepya wa kati wa daraja ya chini wawe na nguvu kubwa katika vikundi hivi vya uongozi, na wakulima wakongwe wa kati wa daraja ya chini na wakulima wa kati wa daraja ya juu wakiwa ni wa zamani au wepya — wawe ni nyongeza ya nguvu. Ni hivi tu ndio umoja baina ya wakulima masikini na wa kati unaweza kupatikana, vyama vya ushirika kuimarishwa, uchumi kupanuliwa na mabadiliko ya kisoshalisti kutimizwa vyema mashambani kote kwa mujibu wa siasa ya Chama. Bila ya kufanywa hivyo, umoja baina ya wakulima wa kati na masikini hautoweza kupatikana, vyama vya ushirika havitoweza kuimarishwa, uchumi hautoweza kupanuliwa,

na mabadiliko ya kisoshalisti mashambani kote hayatoweza kupatikana.

> Maelezo ya utangulizi katika "Vipi Usimamizi wa Chama cha Ushirika cha Wutang Ulitoka Katika Mikono ya Wakulima wa Kati Kuendea Mikononi mwa Wakulima Masikini" (1955).

Ni lazima kuungana na wakulima wa kati, na ni makosa kutofanya hivyo. Lakini tabaka la wafanya kazi na Chama cha Kikoministi lazima wamtegemee nani mashambani kwa ajili ya kuungana na wakulima wa kati na kuleta mageuzo ya kisoshalisti mashambani kote? Hakika si wo wote wengineo isipokuwa wakulima masikini. Hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati mapigano dhidi ya mabwana-shamba yalipokuwa yakifanywa na ugawaji ardhi ulipokuwa ukitekelezwa, na hivyo ndivyo mambo yalivyo leo katika wakati huu yanapofanywa mapigano dhidi ya wakulima matajiri na nguvu nyenginezo za ubepari kwa ajili ya kuyaleta mabadiliko

ya kisoshalisti ya kilimo. Katika nyakati zote hizi mbili za kimapinduzi, wakulima wa kati mwanzoni waliyumba yumba. Ni baada ya kuona wazi mwenendo wa mambo na ushindi unaokaribia wa mapinduzi tu ndipo wakulima wa kati watapokuja kwenye upande wa mapinduzi. Wakulima masikini lazima wawashawishi wakulima wa kati na wawavute kwenye upande wao ili mapinduzi yaenee zaidi siku baada ya siku mpaka upatikane ushindi wa mwisho.

Maelezo ya utangulizi katika "Funzo la 'Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Kati' na 'Chama cha Ushirika cha Wakulima Masikini' Katika Mudiria ya Fuan" (1955).

Kuna mwelekeo mbaya wa kuendea ubepari miongoni mwa wakulima wanaojiweza. Mwelekeo huu utafurutu ada ikiwa sisi tutapuuza japo kidogo kazi ya siasa miongoni mwa wakulima mnamo wakati wa

vugu vugu la vyama vya ushirika na kwa muda mrefu baadaye.

Maelezo ya utangulizi katika "Mapigano Thabiti Lazima Yafanywe Dhidi ya Mwelekeo wa Kibepari" (1955).

Vugu vugu la ushirika wa kilimo lilikuwa mapigano makali ya kifikra na kisiasa tangu mwanzo wake. Hapana chama cha ushirika kinachoweza kuundwa bila ya kupitia mapigano kama hayo. Kabla ya kuweza kujengwa mpango mpya kabisa wa kijamii kwenye kiwanja cha mpango mkongwe, ni lazima kiwanja hiki kifagiliwe kuwa safi. Masalio ya fikra za kizamani zinazomathilisha mpango mkongwe daima yanabakia kwa muda mrefu katika akili za watu, na hayakubali kushindwa kwa urahisi. Baada ya kuundwa chama cha ushirika, ni lazima kipitie mapigano mengi zaidi kabla ya kuweza kuimarishwa. Hata baada ya kuimarishwa,

mara kitaporegeza bidii zake huenda kikaporomoka.

Maelezo ya utangulizi katika "Funzo Kubwa" (1955).

Nguvu za maumbile za kibepari kila kukicha zimekuwa zikikua kidogo kidogo mashambani katika miaka ya karibuni, kwa vile kila mwahala wamechomoza wakulima wepya walio matajiri na wakulima wa kati wanaojiweza wengi wanapigania kuwa wakulima matajiri. Kwa upande mwengine, wakulima masikini wengi bado wanaishi katika hali ya umasikini kwa sababu ya kutokuwa na vifaa vya kutosha vya uchumi, baadhi yao wakiwa katika madeni na wengineo wakiuza au kukodisha ardhi zao. Ikiwa mwelekeo huu utaendelea bila ya kuzuiliwa, pengo baina ya umasikini na utajiri mashambani lazima litazidi siku baada ya siku. Wale wakulima wanaopoteza ardhi zao na wale wanaobakia katika umasikini watanung'unika kwamba

hatufanyi lo lote kuwatoa katika hali mbaya au kuwasaidia kuzishinda shida zao. Wala wale wakulima wa kati wanaojiweza ambao wanaelekea kwenye njia ya ubepari hawatofurahikiwa nasi, kwani maisha hatutoweza kutimiza matakwa yao isipokuwa kama tunataka kuchukua njia ya kibepari. Jee muungano kati ya wafanya kazi na wakulima unaweza kusimama imara katika hali kama hii? Bila ya shaka hauwezi. Tatizo hili haliwezi kutanzuliwa isipokuwa kwa msingi mpya. Na jambo hilo lina maana ya, hatua baada ya hatua, kuleta mabadiliko ya kisoshalisti katika kilimo chote na kwa wakati huo huo, hatua baada ya hatua, kutekeleza uenezaji wa makarahana wa kisoshalisti na ugeuzaji wa kisoshalisti wa kazi za mikono, makarahana na biashara za kibepari; kwa maneno mengine, jambo hilo lina maana ya kufanya vyama vya ushirika na kuufyeka mpango wa uchumi wa wakulima matajiri na wa kibinafsi katika mashamba ili watu wote wa mashambani kwa pamoja wawe wanajiweza zaidi. Tunashikilia kwamba hii

ndio njia ya pekee ya kuimarisha muungano wa wafanya kazi na wakulima.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Kwa mipango inayoangalia kila upande wa mambo, tunakusudia mipango inayofikiria maslaha ya watu 600 milioni wa nchi yetu. Katika kutengeneza mipango yetu, kuendesha mambo au kuyafikiria matatizo, tuanzie kwenye ukweli wa mambo kwamba China ina watu 600 milioni, na lazima tusilisahau milele jambo hili.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Zaidi ya uongozi wa Chama, jambo la uamuzi ni umati wetu wa watu 600 milioni. Watu zaidi, huchomoza mawazo zaidi, shime zaidi na juhudi zaidi. Hapajapatapo kutokea kabla umma wa watu

kuvutika, kuwa imara na mashujaa kuliko hivi sasa.

"Kukijulisha Chama cha Ushirika" (Aprili 15, 1958).

Mbali na tabia zao nyenginezo, jambo kubwa kabisa kuhusu watu 600 milioni wa China ni kuwa wako katika "hali ya umasikini na patupu". Jambo hili linaweza kuonekana kama ni kitu kibaya, lakini kwa kweli ni kitu kizuri. Umasikini huleta hamu ya kutaka mabadiliko, hamu ya kuchukua hatua na hamu ya kufanya mapinduzi. Kwenye karatasi safi isio na alama yo yote, herufi mpya na nzuri kabisa zinaweza kuandikwa, na picha mpya na nzuri kabisa zinaweza kuchorwa.

Kama juu.

Baada ya kupatikana ushindi wa mapinduzi nchini kote na kulitanzua tatizo la ardhi, bado zitabakia hitilafu mbili za msingi katika China. Hitilafu ya kwanza

ni ya ndani, yaani hitilafu baina ya tabaka la wafanya kazi na tabaka la mabepari. Hitilafu ya pili ni ya nje, yaani hitilafu baina ya China na nchi za kibeberu. Kwa sababu hizo baada ya ushindi wa mapinduzi ya kidemokrasi ya umma, hatamu za serikali za jamhuri ya watu chini ya uongozi wa tabaka la wafanya kazi ni lazima zisidhoofishwe bali ziimarishwe.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

"Jee si mnataka kuondosha nguvu za dola?" Ndio tunataka, lakini sio kwa hivi sasa; na bado sasa hatuwezi kufanya hivyo. Kwa nini? Kwa sababu ubeberu bado ungalipo, upingaji maendeleo bado ungalipo na matabaka bado yangalipo nchini kwetu. Kazi yetu ya hivi sasa ni kutilia nguvu mashine ya dola ya umma — hususan jeshi la umma, polisi ya umma na

korti za umma — ili kuimarisha ulinzi wa taifa na kuyahami maslaha ya umma.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Dola yetu ni dola ya udikteta wa kidemokrasi wa umma inayoongozwa na tabaka la wafanya kazi na yenye msingi wa muungano wa wafanya kazi na wakulima. Nini kazi ya udikteta huu? Kazi yake ya mwanzo ni kukandamiza matabaka na makundi ya wapinga maendeleo na wale wanyonyaji damu wanaopinga mapinduzi ya kisoshalisti ya nchini kwetu, kuwakandamiza wale wanaojaribu kuuharibu ujenzi wetu wa kisoshalisti, au kwa maneno mengine, kutanzua hitilafu baina yetu sisi na adui katika nchi yetu. Kwa mfano, kuwakamata, kuwahukumu na kuwafunga wapinga mapinduzi fulani, na kuwanyang'anya mabwana-shamba na mabepari mabwanaserikali haki zao za voti na uhuru wa kusema kwa muda maalum — yote haya

yanaingia katika udikteta wetu. Kwa ajili ya kudumisha utulivu wa nchini na kuyahami maslaha ya umma mkubwa wa watu inatubidi vile vile kutumia udikteta juu ya wale wezi, wanyang'anyi, majambazi, wauaji, watia moto, magengi ya wahalifu na watu wengineo wabaya ambao wanauchafua vibaya utulivu wa nchi. Kazi ya pili ya udikteta huu ni kuihami nchi yetu dhidi ya majungu ya chini kwa chini na hujma zinazoyumkinika kufanywa na maadui wa nje. Wakati hali hiyo itapotokea ni kazi ya udikteta huu kutanzua hitilafu za nje baina yetu sisi na adui. Madhumuni ya udikteta huu ni kuwahami watu wetu wote ili waweze kujishughulisha kufanya kazi katika hali ya amani na kuijenga China kuwa nchi ya kisoshalisti yenye makarahana ya kisasa, kilimo cha kisasa, sayansi na utamaduni wa kisasa.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Udikteta wa kidemokrasi wa umma unahitaji uongozi wa tabaka la wafanya kazi, kwani ni tabaka la wafanya kazi tu ambalo linaona mbali kabisa, lisilojali ubinafsi na lililo la kimapinduzi kamili kuliko yote mengineo. Historia yote ya mapinduzi inathibitisha kwamba bila ya uongozi wa tabaka la wafanya kazi, mapinduzi hufeli na kwamba unapokuweko uongozi wa tabaka la wafanya kazi mapinduzi hufaulu.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Msingi wa udikteta wa kidemokrasi wa umma ni muungano wa matabaka ya wafanya kazi, wakulima na mabepari wadogo wa mjini, na hasa muungano wa wafanya kazi na wakulima, kwa sababu matabaka haya mawili yana idadi ya 80 mpaka 90 katika mia ya umati wa watu wa China. Matabaka haya mawili ndio nguvu kuu

katika kupindua ubeberu na wapinga maendeleo wa Kuomintang. Hatua ya kutoka Demokrasi Mpya kuendea usoshalisti vile vile inategemea sana muungano wao.

Kama juu.

Mapigano ya kitabaka, mapigano ya kiuchumi na majaribio ya kisayansi ni mavugu vugu matatu makubwa ya kimapinduzi kwa ajili ya kujenga nchi ya kisoshalisti yenye nguvu. Mavugu vugu haya ni dhamana ya hakika kwamba Wakoministi wataepukana na mambo ya ubwana-mkubwa na watahifadhika kutokana na ubadilishaji fikra na mambo ya kufuata maneno ya vitabuni kikasuku, na maisha watakuwa hawashindiki. Hizo ni dhamana za kutegemewa kwamba tabaka la wafanya kazi litaweza kuungana na umma mkubwa wa wale wanaoishi kwa jasho lao pamoja na kuutekeleza udikteta wa kidemokrasi. Ikiwa hayatokuweko

mavugu vugu haya, mabwana-shamba, wakulima matajiri, wapinga mapinduzi, watu wabaya na mashetani wa kila aina wataachiliwa kujikokota nje, na makada wetu watafumba macho yao mbele ya mambo haya yote, na wengi wao hata kufeli kumtofautisha adui na sisi wenyewe na badala yake wakawa wanashirikiana na adui, na wao nafsi zao kupotoshwa, kugawanywa na kuharibiwa na adui, ikiwa makada wetu wameshawishiwa kuingia kwenye kambi ya adui au maadui wameweza kujipenyeza miongoni mwetu, na ikiwa wengi wa wafanya kazi, wakulima na wataalamu wetu wameachwa bila ya kitu cha kujihami dhidi ya mbinu laini au kali za adui, basi bila ya shaka haitochukua muda mrefu, pengine miaka michache, au zaidi ya miaka kumi au kwa wingi sana makumi machache ya miaka, kabla uhuishaji wa upingaji mapinduzi katika nchi nzima kutokea kwa lazima. Na chama cha Kimarx-lenin bila ya shaka kitageuka

kuwa chama cha ubadilishaji fikra au chama cha kifashist, na China nzima itabadilika rangi.

Maelezo juu ya "Nyaraka Saba Zilizoandikwa Vyema za Jimbo la Chekiang Kuhusu Kushiriki kwa Makada Katika Kazi za Sulubu" (Mei 9, 1963), imenukuliwa katika *Juu ya Ukoministi wa Uwongo wa Kikhrushchov na Funzo Lake la Kihistoria kwa Ulimwengu.*

Udikteta wa kidemokrasi wa umma unatumia njia mbili. Kwa adui, unatumia njia ya udikteta, yaani kwa muda kama unaopasa hauwaruhusu kushiriki katika mambo ya kisiasa na unawalazimisha kutii sheria za Serikali ya Umma na kufanya kazi za sulubu na, kwa kupitia kufanya kazi, kujibadilisha kuwa watu wepya. Kwa umma, kinyume cha hivyo, unatumia sio njia ya kulazimisha bali ya kidemokrasi, yaani ni lazima uwaruhusu kushiriki katika mambo ya kisiasa na usiwalazimishe kufanya hili au lile bali utumie njia ya

kidemokrasi katika kuwaelimisha na kuwashawishi.

Hotuba ya ufungaji katika Mkutano wa Pili wa Kamiti ya Kwanza ya Taifa ya Baraza la Kushauriana Siasa la Watu wa China (Juni 23, 1950).

Chini ya uongozi wa Chama cha Kikoministi, watu wa China wamo kulifanya vugu vugu kubwa la masahihisho lenye hamasa ili kuleta maendeleo ya haraka katika jihadi ya usoshalisti kwa msingi imara zaidi. Hili ni vugu vugu la kufanya majadiliano makubwa yanayoongozwa na yalio huru na yaliotapakaa nchini kote, mijini na mashambani, juu ya masuala kama njia ya usoshalisti dhidi ya njia ya ubepari, mpango wa msingi wa dola na siasa zake kuu, mitindo ya kazi ya watumishi wa Chama na serikali pamoja na suala la welfeya ya maisha ya watu, majadiliano ambayo yanaendeshwa kwa kuweka mbele ukweli wa mambo na kutoa sababu ya kila kitu, ili kuzitanzua kwa usahihi

hitilafu zilizoko miongoni mwa umma ambazo zinahitaji kutanzuliwa kwa haraka. Hili ni vugu vugu la kisoshalisti la watu kujisomesha na kujigeuza.

"Hotuba Katika Mkutano wa Bunge Kuu la Umoja wa Soviet kwa Kusherehekea Kutimia Miaka Arobaini Tangu Mapinduzi Makubwa ya Kisoshalisti ya Oktoba" (Novemba 6, 1957).

Kazi pevu kabisa ziko mbele yetu katika juhudi kubwa ya ujenzi. Ijapokuwa wapo zaidi ya wanachama milioni kumi katika Chama chetu, bado idadi yao ni sehemu ndogo sana ya watu wa nchi nzima. Katika idara za serikali pamoja na jumuia na makazi ya aina mbali mbali ya nchi yetu inabidi kazi nyingi zifanywe na watu wasio wanachama. Hatutoweza kuzifanya vyema kazi hizi ikiwa si mahodari katika kuutegemea umma wa watu na kushirikiana na watu wasio wanachama. Wakati tunapoendelea kutilia nguvu umoja wa Chama kizima, ni lazima vile vile tuendelee kutilia nguvu umoja wa makabila yote, matabaka

ya kidemokrasi, vyama vya kidemokrasi na jumuia za umma, na tuendelee kuimarisha na kupanua umoja wa muungano wa kidemokrasi wa umma, na lazima katika sehemu yo yote ya kazi zetu kwa makini tusahihishe cho chote kile kinachodhuru umoja baina ya umma na Chama.

"Hotuba ya Ufunguzi Katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kitaifa wa Chama cha Kikomunisti cha China" (Septemba 15, 1956).

4. KUTANZUA KWA USAHIHI HITILAFU MIONGONI MWA UMMA

Tunakabiliwa na aina mbili za hitilafu za jamii — zile baina yetu sisi na adui na zile miongoni mwa umma wenyewe. Aina hizi mbili ni tofauti kabisa katika tabia zao.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Kwa ajili ya kuzifahamu vyema aina hizi mbili tofauti za hitilafu, ni lazima kwanza tuelewe nini hasa maana ya "umma" na nini maana ya "adui". . . . Katika daraja ya sasa, wakati wa kujenga

usoshalisti, matabaka, madaraja na vikundi vya jamii vinavyowafiki, kuunga mkono na kufanya kazi kwa ajili ya jihadi ya kujenga usoshalisti, wote wanaingia katika kundi la umma; na nguvu na vikundi vya jamii ambavyo vinapinga mapinduzi ya kisoshalisti na kuchukia au kuharibu ujenzi wa kisoshalisti wote ni maadui wa umma.

Kama juu.

Katika hali ya leo nchini kwetu, hitilafu miongoni mwa umma zinakusanya hitilafu ndani ya tabaka la wafanya kazi, hitilafu ndani ya tabaka la wakulima, hitilafu ndani ya wataalamu, hitilafu baina ya matabaka ya wafanya kazi na wakulima, hitilafu baina ya wafanya kazi na wakulima kwa upande mmoja na wataalamu kwa upande wa pili, hitilafu baina ya tabaka la wafanya kazi na sehemu nyenginezo za watu wanaoishi kwa jasho lao kwa upande mmoja na tabaka la mabepari wa kitaifa kwa upande mwengine, hitilafu ndani ya tabaka la mabepari wa kitaifa, na kadhalika. Serikali yetu

ya Umma ni serikali ambayo inawakilisha kikweli maslaha ya umma, ni serikali inayotumikia umma. Juu ya hivyo, bado ziko baadhi ya hitilafu baina ya serikali hii na umma. Miongoni mwa hitilafu hizi ni hitilafu kati ya maslaha ya dola, maslaha ya shirika na maslaha ya mtu binafsi; baina ya demokrasi na uongozi; baina ya viongozi na wanaoongozwa; na hitilafu zinazotokana na mtindo wa kufanya kazi wa kibwana-serikali wa baadhi ya watumishi wa serikali katika maingiliano yao na umma. Zote hizi pia ni hitilafu miongoni mwa umma. Kwa jumla, hitilafu miongoni mwa umma wenyewe ni hitilafu zinazotokana na maslaha ya msingi wa namna moja.

Kama juu.

Hitilafu baina yetu sisi na adui ni hitilafu za hasama. Kuhusu umma wenyewe, hitilafu miongoni mwa watu wanaoishi kwa jasho lao wenyewe si za hasama; lakini hitilafu baina ya matabaka yanayonyonywa damu na matabaka ya wanyonyaji damu

licha ya kuwa na upande wa hasama, zina ule usio wa hasama vile vile.

Kama juu.

Katika maisha ya kisiasa ya watu wetu, namna gani mambo sahihi yapambanuliwe na yale ya makosa katika maneno na vitendo vyetu? Kwa msingi wa Katiba ya nchi yetu, matakwa ya umati mkubwa kabisa wa watu wetu na misimamo ya pamoja ya kisiasa, ambayo inatajwa mara nyingi na vyama na vikundi vya kisiasa katika nchi yetu, tunafikiria kuwa kwa jumla mipambanuo iwe kama ifuatayo:

(1) Maneno na vitendo lazima visaidie kuwaunganisha, sio kuwagawanya, watu wa mataifa mbali mbali ya nchi nzima.

(2) Yawe ya manufaa, sio ya madhara, kwa mabadiliko ya kisoshalisti na ujenzi wa kisoshalisti.

(3) Yasaidie kuimarisha, sio kubomoa au kudhoofisha, udikteta wa kidemokrasi wa umma.

(4) Yasaidie kuimarisha, sio kubomoa au kudhoofisha mpango wa demokrasi-uongozi.

(5) Yasaidie kuimarisha, sio kuondoa au kudhoofisha, uongozi wa Chama cha Kikoministi.

(6) Yawe ya manufaa, sio ya madhara, kwa umoja wa kisoshalisti wa ulimwengu na umoja wa watu wapendao amani wa dunia nzima.

Kati ya mipambanuo hii sita, muhimu kuliko yote ni njia ya kisoshalisti na uongozi wa Chama.

Kama juu.

Suala la kuwafagia wapinga mapinduzi ni suala la mapigano kuhusu hitilafu baina yetu sisi na adui. Miongoni mwa umma, kuna baadhi ya watu wanaolizingatia suala hili kwa namna nyengine. Ziko aina mbili za watu wenye maoni tofauti na yetu. Wale wenye fikra za Upande wa Kulia hawaweki tofauti baina yetu sisi na adui na wanawachukulia maadui kama ni watu wetu wenyewe. Wao wanawachukulia kama marafiki wale watu ambao umma mkubwa wa watu wanawachukulia kuwa ni

maadui. Wale watu wenye fikra za "Upande wa Kushoto" wanazikuza hitilafu baina yetu sisi na adui hata kufikilia kiwango ambacho wanazifanya hitilafu fulani miongoni mwa umma kuwa ni hitilafu baina yetu sisi na adui na kuwafikiria watu fulani kuwa ni wapinga mapinduzi ilhali kwa kweli wao si wapinga mapinduzi. Fikra zote hizi mbili ni makosa. Hapana moja katika hizi inayoweza kuleta utanzuaji sahihi wa suala la kuwafagia wapinga mapinduzi au makadirio sahihi ya kazi hii.

Kama juu.

Hitilafu zenye tabia tofauti haziwezi kutanzuliwa isipokuwa kwa njia za tabia tofauti. Kwa mfano, hitilafu baina ya tabaka la kifanya kazi na tabaka la kibepari zinatanzuliwa kwa njia ya mapinduzi ya kisoshalisti; hitilafu baina ya umma mkubwa wa watu na mpango wa kimwinyi zinatanzuliwa kwa njia ya mapinduzi ya kidemokrasi; hitilafu baina ya makoloni na ubeberu zinatanzuliwa kwa njia ya vita vya

kimapinduzi vya kitaifa; hitilafu baina ya tabaka la wafanya kazi na tabaka la wakulima katika jamii ya kisoshalisti zinatanzuliwa kwa njia ya kulima kwa ujima na kutumia mashine katika kilimo; hitilafu ndani ya Chama cha Kikoministi zinatanzuliwa kwa njia ya kutoa makosa na kujitoa makosa; hitilafu baina ya jamii na maumbile zinatanzuliwa kwa njia ya kuzikuza nguvu za uchumi. . . . Msingi wa kutumia njia tofauti katika kutanzua hitilafu tofauti ni msingi ambao lazima wafuasi wote wa Umarx-lenin waufuate barabara.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Ilivyokuwa hitilafu baina yetu sisi na adui na hitilafu miongoni mwa umma zina tabia tofauti, basi ni lazima zitanzuliwe kwa njia tofauti. Kwa ufupi, lile la kwanza ni suala la kufanya mpambanuo wazi baina yetu sisi na adui, na la pili ni la kufanya mpambanuo wazi baina ya mambo sahihi na makosa. Bila ya shaka, ni kweli kwamba mpambanuo baina yetu

sisi na adui vile vile ni suala la mambo sahihi na makosa. Kwa mfano, suala kama nani yuko katika upande wa haki, sisi au wapinga maendeleo wa ndani na wa nje — wabeberu, mamwinyi na mabepari mabwana-serikali — vile vile ni suala la mambo sahihi na makosa, lakini kwa tabia ni aina tofauti na suala la mambo sahihi na makosa miongoni mwa umma.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Njia ya pekee ya kutanzua masuala ya kifikra au mambo ya mabishano miongoni mwa umma ni njia ya kidemokrasi, ya kujadiliana, ya kutoana makosa, ya kushawishiana na kuelimishana, na sio kwa njia ya kutumia nguvu na ukandamizi.

Kama juu.

Kwa ajili ya kuendeleza kazi zao za uchumi na masomo yao vilivyo na kuyapanga maisha yao vizuri, umma unaitaka

serikali yao na wale wasimamizi wa uchumi na viongozi wa jumuia za utamaduni na elimu kutoa amri na sheria zinazofaa ambazo hazina budi kufuatwa. Ni kitu kinachojulikana na wote kuwa ni muhali kuweka utulivu nchini bila ya amri kama hizo za serikali. Amri za serikali na njia ya kushawishi na kuelimisha ni mambo yanayosaidiana katika kutanzua hitilafu miongoni mwa umma. Hata amri zilizotolewa kwa ajili ya kuweka utulivu nchini lazima zifuatwe na njia ya kushawishi na kuelimisha, kwani mara nyingi amri pekee hazifai kitu.

Kama juu.

Haiwezi kuepukika kuwa mabepari na mabepari wadogo watafanya mambo ya kumathilisha fikra zao. Lazima wao kwa ukaidi watajibainisha nafsi zao katika masuala ya siasa na fikra kwa kila njia inayoyumkinika. Usiwatarajie kufanya vyengine. Tusitumie njia ya ukandamizi na kuwazuia wasijionyeshe, bali tuwaachilie kufanya hivyo na kwa wakati huo huo tujadiliane

nao na tuwatoe makosa kama inavyotakikana. Bila ya shaka ni lazima tuzitoe makosa fikra mbaya za kila aina. Bila ya shaka itakuwa sivyo kujizuia kutoa makosa, kuangalia tu wakati fikra mbaya zinatapakaa bila ya kuzuiliwa na kuziwacha kuhodhi uwanja. Makosa lazima yapondwe na magugu ya sumu yafyekwe kila yanapochomoza. Juu ya hayo, utoaji makosa huo usiwe wa kufuata maneno ya vitabuni kikasuku, na njia ya *metaphysics* isitumiwe, bali iwepo jitihada ya kutumia njia ya upembuzi. Kinachotakiwa ni uchambuzi wa kisayansi na sababu madhubuti za kumsadikisha mtu.

Kama juu.

Kutoa makosa upungufu wa umma ni jambo la lazima. . : . lakini, katika kufanya hivyo, ni lazima tuuchukue kikweli msimamo wa kiumma na tuyaseme maneno kwa dhati ya moyo ya kuwahifadhi na kuwaelimisha. Kuwachukulia makomredi

kama maadui ni kwenda katika msimamo wa adui.

"Mazungumzo Katika Mkutano wa Yenan wa Mambo ya Uandishi na Sanaa" (Mei 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Hitilafu na mapigano ni mambo yaliopo po pote ulimwenguni na mambo haya ni ya hakika kabisa, lakini njia za kutanzulia hitilafu, yaani aina za mapigano, zinatofautika kwa mujibu wa tofauti ya tabia ya hitilafu. Baadhi ya hitilafu zinachukua tabia ya uhasama ya wazi wazi, nyinginezo si hivyo. Kwa mujibu wa mambo yanavyokwenda hasa, baadhi ya hitilafu ambazo zilianzia kuwa si za uhasama huenda zikageuka kuwa za uhasama, ilhali nyingine ambazo mwanzo zilikuwa za uhasama huenda zikageuka kuwa si za uhasama.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Katika hali ya kawaida, hitilafu miongoni mwa umma si za uhasama. Lakini

kama hazikutanzuliwa vyema, au kama tunaregeza uangalifu wetu na kutochukua hadhari, uhasama huenda ukaanza. Katika nchi za kisoshalisti, kwa desturi, hali ya namna hii huwa ni jambo la mahala pamoja au la muda tu. Sababu ni kuwa katika nchi za kisoshalisti, mpango wa unyonyaji damu wa mtu kwa mtu umeondoshwa na maslaha ya umma kwa msingi ni ya namna moja.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Katika nchi yetu, hitilafu baina ya tabaka la wafanya kazi na tabaka la mabepari wa kitaifa inaingia katika hesabu ya hitilafu miongoni mwa umma. Kwa jumla, mapigano ya kitabaka baina ya matabaka haya mawili ni mapigano ya kitabaka miongoni mwa umma, kwa sababu tabaka la mabepari wa kitaifa wa Kichina lina tabia mbili. Katika wakati wa mapinduzi ya kidemokrasi ya kibepari wao walikuwa na

tabia ya kimapinduzi na ya kupatana na adui. Katika wakati wa mapinduzi ya kisoshalisti, kuwanyonya damu wafanya kazi kwa ajili ya kujipatia faida ni tabia yao moja, na kuunga mkono Katiba na kukubali mageuzo ya kisoshalisti ni tabia yao nyingine. Tabaka la mabepari wa kitaifa linatofautiana na ubeberu, tabaka la mabwana-shamba na tabaka la mabepari mabwana-serikali. Hitilafu zilizoko baina ya tabaka la wafanya kazi na tabaka la mabepari wa kitaifa ni zile za baina ya wanyonyaji damu na wanyonywaji damu, na kwa asili ni za uhasama. Lakini katika hali maalum ya China hitilafu hizi za uhasama zinaweza, kwa kupata uongozi barabara, kugeuzwa kuwa si za uhasama na kutanzuliwa kwa njia ya amani. Juu ya hivyo, hitilafu zitabadilika kuwa hitilafu baina yetu sisi na adui pindi ikiwa hatukuziongoza vyema na hatukufuata siasa ya kuungana na, kutoa makosa na kuelimisha tabaka la mabepari wa kitaifa, au kama tabaka la mabepari wa kitaifa halikubali siasa yetu hii.

Kama juu.

Wapinga maendeleo ndani ya nchi ya kisoshalisti walioshirikiana na wabeberu, wanajaribu kuzipata azma zao mbovu kwa kuchukua fursa ya hitilafu miongoni mwa umma na kuleta mfarikiano na mchafuko. Funzo hili la tukio la Hungary [lililotokea mwaka 1956] linastahili kuangaliwa na watu wote.

Kama juu.

5. VITA NA AMANI

Vita — umbo la juu kabisa la jihadi ya kutanzua hitilafu, zinapofikilia daraja fulani, baina ya matabaka, mataifa, madola, au makundi ya kisiasa, na vimekuwapo tangu kuchomoza umilikaji wa kibinafsi na matabaka.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

"Vita ni maendelezo ya siasa." Kwa maana hii, vita ni siasa na vita vyenyewe ni kitendo cha kisiasa; tangu zama za kale hapajatokea vita ambavyo havikuwa na tabia ya kisiasa. . . .

Lakini vita vina tabia zake maalum na kwa upande huu haviwezi kuwa sawa

sawa na siasa ya kawaida. "Vita ni maendelezo ya siasa kwa njia nyengine maalum." Wakati siasa inapoendelea na kufikia daraja fulani ambapo haiwezi kuendelea kwa njia za kawaida, basi hapo tena hutokea vita ili kuviondoa vipingamizi njiani. ... Vipingamizi vinapokwishaondolewa na madhumuni ya kisiasa kupatikana, hapo tena vita humalizika. Lakini kama vipingamizi havijaondolewa kwa ukamilifu, basi itabidi vita viendelee mpaka madhumuni hayo yapatikane kwa ukamilifu. ... Kwa hivyo inawezekana kusemwa kwamba siasa ni vita bila ya kumwaga damu na vita ni siasa ya kumwaga damu.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika historia vita vimegawika kuwa aina mbili, vya haki na visivyo vya haki. Vita vyote vya maendeleo ni vya haki na vita vyote vinavyozuia maendeleo si vya haki. Sisi Wakoministi tunapinga vita vyote visivyo vya haki ambavyo vinayazuia

maendeleo, lakini hatupingi vita vya maendeleo vilivyo vya haki. Si kama sisi Wakoministi hatupingi tu vita vya haki, bali hushiriki kwa juhudi katika vita kama hivyo. Ama kuhusu vita visivyo vya haki, Vita vya Kwanza vya Dunia ambavyo pande zote mbili zilipigania maslaha ya ubeberu, kwa hivyo Wakoministi wa dunia nzima walivipinga kwa uthabiti. Njia ya kuvipinga vita kama hivi ni kujaribu kufanya kila linaloyumkinika kuvizuia kabla havijaanza na, vikishaanza, kupinga vita kwa vita, kupinga vita visivyo vya haki kwa vita vya haki, kila inapowezekana.

Kama juu.

Mapinduzi na vita vya kimapinduzi ni vitu visivyoweza kuepukika katika jamii ya matabaka, na bila ya kuwepo ni muhali kupata mchupo wo wote katika maendeleo ya jamii na kuyapindua matabaka yanayotawala ya wapinga maendeleo na kwa hivyo ni muhali kwa umma kupata hatamu za serikali.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu I.

Vita vya kimapinduzi ni dawa ya kuzuia sumu ambayo si kama inaitoa sumu ya adui tu bali vile vile inatusafisha uchafu wetu. Kila vita vya kimapinduzi vya haki vina nguvu kubwa sana na vinaweza kugeuza mambo mengi au kusafisha njia kwa ajili ya kuyageuza. Vita baina ya China na Japani vitazigeuza nchi zote mbili za China na Japani; ikiwa China itaendelea na Vita vya Kupinga Japani na muungano wa pamoja, basi Japani kongwe bila ya shaka itageuzwa kuwa Japani mpya na China kongwe kuwa China mpya, na watu na kila kitu katika China na Japani vitabadilika katika wakati wa vita na baadaye.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kila Mkoministi lazima aujue ukweli huu, "Hatamu za serikali zinatokana na mdomo wa bunduki."

"Matatizo ya Vita na Hila ya Jumla ya Vita" (Novemba 6, 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kuchukua hatamu za serikali kwa nguvu za silaha, kulitanzua jambo kwa njia ya vita, ndio kazi kuu na umbo la juu kabisa la mapinduzi. Kanuni hii ya mapinduzi ya Kimarx-lenin ni ukweli unaofaa katika ulimwengu mzima, katika China na nchi zote nyenginezo.

Kama juu.

Bila ya mapigano ya silaha, si tabaka la wafanya kazi, wala umma, wala Chama cha Kikoministi, wote hawatokuwa na satwa yo yote katika China na itakuwa muhali kwa mapinduzi kufaulu. Katika miaka hii kumi na nane [toka kuasisiwa Chama], maendeleo, maimarisho, na matendo ya kukifanya Chama chetu kuwa cha kibolshevik yameendelea katika hali ya vita vya kimapinduzi; bila ya mapigano ya silaha, Chama cha Kikoministi hakika kisingelikuwa kilivyo hivi leo. Makomredi wote katika Chama wasisahau daima maarifa haya tuliyoyapata kwa kumwaga damu.

"Utangulizi wa *Gazeti la Mkoministi*" (Oktoba 4, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kwa mujibu wa mtizamo wa mafunzo ya Umarx kuhusu dola, jeshi ndio sehemu muhimu ya hatamu za serikali. Ye yote anayetaka kuchukua na kudumisha hatamu za serikali lazima awe na jeshi lenye nguvu. Baadhi ya watu wanatukejeli kuwa watetezi wa "vita ndivyo vikatavyo shauri kila kitu". Ndio, sisi ni watetezi wa vita vya kimapinduzi kukata shauri kila kitu; hivyo ni vizuri, si vibaya, ni mafunzo ya Umarx. Bunduki za Chama cha Kikoministi cha Urusi ziliunda usoshalisti. Sisi tutaunda jamhuri ya kidemokrasi. Maarifa ya mapigano ya kitabaka katika zama za ubeberu yanatufundisha kwamba ni kwa nguvu za bunduki tu ndio tabaka la wafanya kazi na umma wanaoishi kwa jasho lao wanaweza kuwashinda mabepari na mabwana-shamba wenye silaha; kwa upande huu tunaweza kusema kwamba ni kwa bunduki tu ndio dunia nzima inaweza kugeuzwa.

"Matatizo ya Vita na Hila ya Jumla ya Vita" (Novemba 6, 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Sisi ni watetezi wa kuondoshwa vita, hatutaki vita; lakini vita vinaweza kuondoshwa kwa vita tu, na kwa ajili ya kuondoa bunduki ni lazima kuchukua bunduki.

Kama juu.

Vita, zimwi hili linaloleta binaadamu kuchinjana litafyekwa mwishowe na maendeleo ya jamii ya binaadamu, na wala jambo hilo haliko mbali. Lakini iko njia moja tu ya kuliondosha jambo hili, nayo ni kupinga vita kwa vita, kupinga vita vya kipinga mapinduzi kwa vita vya kimapinduzi, kupinga vita vya kitaifa vya kipinga mapinduzi kwa vita vya kitaifa vya kimapinduzi, na kupinga vita vya kitabaka vya kipinga mapinduzi kwa vita vya kitabaka vya kimapinduzi. ... Wakati jamii ya binaadamu itapofikilia kiwango ambacho hapatokuweko matabaka na madola, basi hapatokuweko tena vita vyo vyote, vya kipinga mapinduzi au vya kimapinduzi, visivyo vya haki au vya haki; hizo zitakuwa zama za amani ya kudumu kwa binaadamu. Masomo yetu kuhusu mwenendo wa vita

vya kimapinduzi yanatokana na nia yetu ya kuondosha vita vyote; hapa ndipo ulipo mpambanuo baina yetu sisi Wakoministi na matabaka yote ya wanyonyaji damu.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Nchi yetu na nchi zote za kisoshalisti zinataka amani; watu wa nchi zote za dunia pia wanataka amani. Wale wanaomezea mate vita na wasiotaka amani ni vikundi fulani vya mabepari wanaohodhi rasilmali katika nchi chache tu za kibeberu ambazo zinategemea ushambulizi kwa ajili ya kujitajirisha.

"Hotuba ya Ufunguzi Katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kitaifa wa Chama cha Kikoministi cha China" (Septemba 15, 1956).

Kwa ajili ya kuipata amani ya kudumu ya dunia, ni lazima tukuze zaidi urafiki

na mashirikiano yetu na nchi zote za kidugu katika kambi ya kisoshalisti na kuimarisha umoja wetu na nchi zote zipendazo amani. Lazima tujitahidi kuanzisha mahusiano ya kawaida ya kiserikali na nchi zote ambazo ziko tayari kuishi pamoja nasi kwa amani, kwa msingi wa kuheshimiana kuhusu mipaka na mamlaka ya nchi na wa usawa na faida kwa pande zote mbili. Lazima tuunge mkono kwa juhudi vugu vugu la uhuru na ukombozi wa kitaifa la nchi zote za Asia, Afrika na Latin Amerika pamoja na vugu vugu la amani na mapigano ya haki katika nchi zote za dunia.

Kama juu.

Ama kuhusu nchi za kibeberu, inatupasa tuungane na watu wa nchi hizo na tupiganie kuishi pamoja nazo kwa amani, tufanye biashara nazo na tuzuie vita vyo vyote vinavyoonyesha ishara ya kutokea, lakini kwa namna yo yote tusiwe na fikra za ndoto juu yao.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Tunataka amani. Lakini ikiwa ubeberu unashikilia kupigana vita, basi hatuna budi kuwa na azimio thabiti la kupigana mpaka mwisho kabla ya kuendelea na ujenzi wetu. Ikiwa unaogopa vita siku nenda siku rudi, nini utafanya kama vita mwishowe vitakuja? Hapo kabla nilisema kuwa Upepo wa Mashariki unavuma juu ya Upepo wa Magharibi na kwamba vita havitatokea, na sasa hivi nimeongeza maelezo haya juu ya hali ya mambo pindi vita vikitokea. Kwa hivyo mawezekano yote mawili yamezingatiwa.

Hotuba katika Mkutano wa Moscow wa Vyama vya Kikomunisti na Kifanya Kazi (Novemba 18, 1957), imenukuliwa katika "Taarifa ya Msemaji wa Serikali ya China" (Septemba 1, 1963).

Watu wa nchi zote za dunia sasa wanajadiliana kama vitatokea au la vita vya tatu vya dunia. Juu ya suala hili, vile vile inatulazimu kuzitayarisha akili zetu na kufanya uchambuzi kidogo. Tunasimama imara

kwa ajili ya amani na kupinga vita. Lakini ikiwa wabeberu watashikilia kuanzisha vita vingine, tusiviogope. Msimamo wetu juu ya suala hili ni kama ule kuhusu mchafuko wo wote: kwanza, tunavipinga; pili, hatuviogopi. Vita vya Kwanza vya Dunia vilifuatwa na kuzaliwa kwa Umoja wa Soviet wenye watu milioni 200. Vita vya Pili vya Dunia vilifuatwa na kuchomoza kwa kambi ya kisoshalisti yenye idadi ya jumla ya watu milioni 900. Ikiwa wabeberu wanashikilia kuanzisha vita vya tatu vya dunia, ni hakika kwamba milioni mia kadha zaidi za watu watageukia upande wa usoshalisti, na hapo tena hapatobakia nafasi kubwa kwa wabeberu katika dunia; pia inaelekea kwamba jengo lote la ubeberu litaporomoka moja kwa moja.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Fanya matata, feli, fanya matata tena, feli tena . . . mpaka kuangamia kwao; hivi ndivyo zifanyavyo kazi akili za wabeberu na wapinga maendeleo wote wa dunia

katika kupambana na jihadi ya umma, na daima hawatakwenda kinyume na mwendo huu. Hii ni kanuni ya Kimarx. Tunaposema kuwa "ubeberu ni katili", tunakusudia kwamba tabia yake ya maumbile haitobadilika, kwamba wabeberu hawataweka chini majisu yao ya kuchinjia, kwamba hawatakuwa Mabuda abadan, mpaka kuangamia kwao.

Pigana, feli, pigana tena, feli tena, pigana tena . . . mpaka kushinda kwao; hivi ndivyo zifanyavyo kazi akili za umma, na wao pia milele hawatakwenda kinyume na mwendo huu. Hii ni kanuni nyengine ya Kimarx. Mapinduzi ya watu wa Urusi yalifuata kanuni hii, mapinduzi ya watu wa China pia yamefuata kanuni hii.

"Ondosheni Ndoto, Jitayarisheni kwa Mapigano" (Agosti 14, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Ushindi kwa hali yo yote ile usitufanye tupunguze uangalifu wetu kwa

majungu ya kiwazimu ya kulipiza kisasi yapikwayo na wabeberu na vijibwa vyao. Ye yote atakayepunguza uangalifu wake atajivunja nguvu katika upande wa kisiasa na kujitia katika hali ya kutoweza kufanya lo lote.

"Hotuba Kwenye Kamiti ya Matayarisho ya Baraza Jipya la Kushauriana Siasa" (Juni 15, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Wabeberu na vijibwa vyao — wapinga maendeleo wa Kichina — hawatoridhika na kushindwa kwao katika ardhi hii ya China. Wataendelea kujikusanya pamoja dhidi ya watu wa China kwa kila njia inayoyumkinika. Kwa mfano, watawapenyeza vibaraka vyao katika China ili kuleta mafarikiano na kufanya mchafuko. Hiyo ni hakika, daima hawatopuuza mambo haya. Tukichukua mfano mwengine, wabeberu watawachochea wapinga maendeleo wa Kichina, na hata kutumia nguvu zao wenyewe, kuweka vipingamizi kwenye

bandari za China. Watafanya hivi kama inavyoyumkinika. Zaidi ya hayo, ikiwa bado wanataka kufanya ujasiri, wataleta vikosi vyao kushambulia na kufanya uchokozi kwenye mipaka ya China, hili pia ni jambo linalowezekana. Yote haya lazima tuyafikiri kwa ukamilifu.

Kama juu.

Dunia inasonga mbele, mustakbala ni mzuri na hapana anayeweza kuugeuza muelekeo huu wa jumla wa historia. Inatupasa mara kwa mara tueneze habari miongoni mwa umma kuhusu maendeleo ya ulimwengu na mustakbala wake mzuri ili tuwafanye wawe na imani zaidi juu ya ushindi.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Makamanda na wapiganaji wote wa Jeshi la Ukombozi la Umma la China

lazima wasiregeze hata kidogo nia yao ya kupigana; fikra yo yote inayoregeza nia ya kupigana na kumdharau adui ni ya makosa.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

6. WABEBERU NA WAPINGA MAENDELEO WOTE NI CHUI WA KARATASI

Wapinga maendeleo wote ni chui wa karatasi. Kwa wajihi, wapinga maendeleo wanatisha, lakini kwa kweli hawana nguvu namna hivyo. Tukitizama mbali, tutaona kuwa si wapinga maendeleo bali ni umma ambao una nguvu kubwa za kikweli.

"Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kimarekani Anna Louise Strong" (Agosti 1946), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kama ilivyokuwa hapana hata kitu kimoja duniani kisicho na tabia mbili (hii

ni kanuni ya muungano wa vitu vinavyopingana), kwa hivyo pia wabeberu na wapinga maendeleo wote wana tabia mbili — wao ni chui wa kweli na kwa wakati huo huo ni chui wa karatasi. Katika historia ya siku za nyuma, kabla ya kujipatia nguvu za utawala na kwa muda baadaye, tabaka la wamilikiaji watumwa, tabaka la mabwana-shamba wa kimwinyi na tabaka la mabepari walikuwa ni wenye juhudi na wana-mapinduzi na wapenda maendeleo; walikuwa chui wa kweli. Lakini baada ya kupita muda, kwa sababu wapinzani wao — tabaka la watumwa, tabaka la wakulima na tabaka la wafanya kazi — kuengezeka nguvu hatua kwa hatua, kupigana nao kwa ukali zaidi na zaidi, matabaka haya ya watawala yakageuka hatua baada ya hatua kwenda nyuma na kuwa wapinga maendeleo, kuwa watu walio nyuma, kuwa chui wa karatasi. Na mwishowe matabaka haya yalipinduliwa, au yatapinduliwa na umma. Matabaka ya wapinga maendeleo, yaliyo nyuma, na yanayooza huendelea kuwa na tabia hizi mbili hata katika mapigano ya umma ya mwisho ya kufa kupona dhidi yao.

Kwa upande mmoja, yalikuwa chui wa kweli, ambao walimeza watu, walimeza watu kwa mamilioni na makumi ya mamilioni. Jihadi ya mapigano ya umma ilipitia nyakati za taabu na shida na njiani kulikuweko mazonge mazonge mengi. Kwa ajili ya kuubomoa utawala wa mabeberu, mamwinyi na mabepari mabwana-serikali katika China, iliwachukua watu wa China zaidi ya miaka mia na kuwagharimu makumi ya mamilioni ya roho kabla ya kuupata ushindi mnamo mwaka 1949. Angalia! Jee hawa hawakuwa chui wahai, chui wa chuma, chui wa kweli? Lakini mwishowe waligeuka kuwa chui wa karatasi, chui maiti, chui wa *bean-curd*. Huu ni ukweli wa historia. Jee watu hawajayaona na kuyasikia mambo haya? Hakika yamekuwepo maelfu na makumi ya maelfu ya mambo haya! Maelfu na makumi ya maelfu! Kwa hivyo, wabeberu na wapinga maendeleo wote, wakiangaliwa kwa tabia hasa ya mambo, kwa kutizama mbali, kwa muangalio wa hila ya jumla ya vita, lazima watizamwe kama walivyo hasa — chui wa karatasi. Kwa msingi huu ndiyo tujenge fikra zetu za hila

ya jumla ya vita. Kwa upande mwengine, wao vile vile ni chui wahai, chui wa chuma, chui wa kweli ambao wanaweza kuwameza watu. Juu ya msingi huu tuzijenge fikra zetu kuhusu mbinu na njia za kivita.

Hotuba katika Mkutano wa Wuchang wa Ofisi Kuu ya Siasa ya Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China (Desemba 1, 1958), imenukuliwa katika maelezo ya kufahamisha ya "Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kimarekani Anna Louise Strong", *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Nimesema kuwa wapinga maendeleo wote wenye sifa ya kuwa na nguvu nyingi ni chui wa karatasi tu. Sababu ya hivyo ni kuwa wamejitenga na umma. Angalia! Jee, Hitler hakuwa chui wa karatasi? Hitler hakupinduliwa? Vile vile nilisema kuwa *tsar* wa Urusi, mfalme mkuu wa China na ubeberu wa Kijapani wote ni chui wa karatasi. Kama tujuavyo, wote walipinduliwa. Ubeberu wa Kimarekani bado haujapinduliwa na una bomu la atomik.

Naamini kwamba nao vile vile utapinduliwa. Nao pia ni chui wa karatasi.

Hotuba katika Mkutano wa Moscow wa Vyama vya Kikomi-nisti na Kifanya Kazi (Novemba 18, 1957).

"Kunyanyua jabali kujibwaga nalo miguuni" ni fumbo la Kichina linaloeleza tabia ya wapumbavu fulani. Wapinga maendeleo wa nchi zote ni wapumbavu wa aina hii. Katika uchambuzi wa mwisho, mateso yao ya kila aina wanayowafanyia watu wa kimapinduzi yanasaidia tu katika kuharakisha mapinduzi ya umma kuwa ya kiwango kikubwa zaidi na makali zaidi. Jee mateso yaliyofanywa na *tsar* 'wa Urusi na Chiang Kai-shek juu ya watu wa kimapinduzi hayakufanya kazi hii katika mapinduzi makubwa ya Urusi na China?

"Hotuba Katika Mkutano wa Bunge Kuu la Umoja wa Soviet kwa Kusherehekea Kutimia Miaka Arobaini Tangu Mapinduzi Makubwa ya Kisoshalisti ya Oktoba" (Novemba 6, 1957).

Ubeberu wa Kimarekani umeishambulia Taiwan ambayo ni sehemu ya nchi yetu, na umeitawala kwa nguvu kwa muda wa miaka tisa iliopita. Hivi karibuni ulipeleka vikosi vya kijeshi kuishambulia na kujitwalia Lebanon. Marekani imeweka mamia ya vituo vya kijeshi katika nchi nyingi za dunia. Sehemu ya nchi yetu Taiwan, Lebanon na vituo vyote vya kijeshi vyenginevyo vya Marekani katika nchi za kigeni ni vitanzi kadha shingoni mwa ubeberu wa Kimarekani. Vitanzi hivi vimetengezwa na Wamarekani wenyewe na wala si ye yote mwengineo, na ni wao wenyewe waliojitia vitanzi hivyo shingoni mwao, wakiwapa ncha za kamba watu wa China, watu wa nchi za Kiarabu na watu wote wa dunia nzima wanaopenda amani na kupinga ushambulizi. Kila washambulizi wa Kimarekani watapoendelea kubakia katika mwahala humo, ndipo vitanzi vilivyopo shingoni mwao vitapozidi kukaza.

Hotuba katika Baraza Kuu la Dola (Septemba 8, 1958).

Wabeberu hawatodumu kwa muda mrefu kwa sababu daima wanafanya maovu ya kila aina. Wanashikilia kuwalea na kuwasaidia wapinga maendeleo wanaopinga umma katika nchi zote, wamenyakua kwa nguvu makoloni na nusu-makoloni mengi na vituo vyingi vya kivita, na wanahatarishā amani kwa vita vya atomik. Kwa hivyo, kwa kulazimishwa na wabeberu, zaidi ya 90 katika 100 ya watu wa dunia wanainuka au watainuka kuwapinga. Juu ya hivyo, wabeberu bado wahai, bado wanafanya maovu kijanda wazimu katika Asia, Afrika na Latin Amerika. Katika nchi za Magharibi, wabeberu bado wangali wakikandamiza watu wa nyumbani kwao. Hali hii lazima ibadilike. Ni kazi ya umma wa dunia nzima kukomesha ushambulizi na ukandamizi unaofanywa na ubeberu, hususan ubeberu wa Kimarekani.

Mazungumzo na mwandishi habari wa Shirika la Habari la Hsinhua (Septemba 29, 1958).

Kwa kuranda randa kijanda wazimu kila mwahala, ubeberu wa Kimarekani umejifanya kuwa ni adui wa watu wa dunia na umezidi kujitenga. Watu wote wanaokataa kutiwa utumwani milele hawatotishwa na mabomu ya atomik na *hydrogen* yaliomo katika mikono ya wabeberu wa Kimarekani. Wimbi kali la watu wa dunia dhidi ya washambulizi wa Kimarekani halizuiliki. Mapigano yao ya kupinga ubeberu wa Kimarekani na vibaraka vyake hakika yatapata mafanikio makubwa zaidi.

"Mazungumzo ya Kuunga Mkono Mapigano ya Haki ya Kiwananchi ya Watu wa Panama Dhidi ya Ubeberu wa Kimarekani" (Januari 12, 1964), *Watu wa Ulimwengu, Unganeni na Muwashinde Washambulizi wa Kimarekani na Vibaraka Vyao Vyote.*

Ikiwa makundi ya mabepari wanaohodhi rasilmali ya Kimarekani yatashikilia kuendeleza siasa zake za kishambulizi na kivita, siku itakuja ambapo yatatiwa kitanzi shingoni mwao na watu wa dunia nzima. Hivyo

pia ndivyo watavyoishia washiriki wa Marekani.

Hotuba katika Baraza Kuu la Dola (Septemba 8, 1958).

Kwa ajili ya kupigana na adui, kwa muda mrefu tumeikuza fikra hii ifuatayo: katika hila ya jumla ya vita tuwadharau maadui zetu wote, lakini katika mambo ya mbinu tuwaangalie kwa hadhari. Jambo hili vile vile lina maana ya kwamba tumdharau adui kuhusu mambo yote kwa jumla, lakini tumwangalie kwa hadhari kuhusu kila jambo maalum. Ikiwa hatumdharau adui kuhusu mambo yote kwa jumla, basi tutafanya makosa ya upotovu. Marx na Engels walikuwa ni watu wawili tu lakini hata katika siku hizo walitangaza kwamba ubepari utapinduliwa duniani kote. Lakini tunapoangalia matatizo maalum na maadui maalum tutafanya makosa ya ujasiri iwapo hatutowaangalia kwa hadhari. Katika vita, mapigano yanaweza kufanywa moja baada ya moja tu na nguvu za adui zinaweza kuvunjwa sehemu moja baada ya nyengine tu. Makarahana

yanaweza kujengwa moja baada ya moja tu. Wakulima wanaweza kuilima ardhi konde moja baada ya moja tu. Jambo hili ni kweli hata katika kula chakula. Katika hila ya jumla kuhusu kula, huchukulia kukila chakula hicho kama ni jambo la wepesi — tunajua tutakisha. Lakini kuhusu namna ya kula, hula tonge baada ya tonge. Ni muhali kukila chakula chote cha karamuni kwa tonge moja. Hii inajulikana kama ni tanzuo la hatua kwa hatua. Kwa lugha ya kijeshi, njia hii inajulikana kama kuyafyeka majeshi ya adui moja baada ya moja.

Hotuba katika Mkutano wa Moscow wa Vyama vya Kikoministi na Kifanya Kazi (Novemba 18, 1957).

Ni fikra yangu kwamba hali ya ulimwengu sasa imefikia kiwango kipya cha mabadiliko. Hivi leo, katika dunia, kuna pepo mbili — Upepo wa Mashariki na Upepo wa Magharibi. Kuna msemo wa Kichina usemao "Ama Upepo wa Mashariki unavuma juu ya Upepo wa Magharibi au Upepo

wa Magharibi unavuma juu ya Upepo wa Mashariki." Naamini tabia maalum ya hali ya mambo hivi leo ni kwamba Upepo wa Mashariki unavuma juu ya Upepo wa Magharibi. Hii ni kusema kwamba nguvu za kisoshalisti ni kubwa zaidi sana kuliko nguvu za ubeberu.

Kama juu.

7. KUTHUBUTU KUPIGANA NA KUTHUBUTU KUSHINDA

Watu wa dunia nzima, unganeni na muwashinde washambulizi wa Kimarekani na vijibwa vyao vyote! Watu wa dunia nzima, kuweni mashujaa, thubutuni kupigana, msiziogope shida na msonge mbele wimbi juu ya wimbi. Hapo tena dunia yote itakuwa ya umma. Majinamizi ya kila namna yataangamizwa.

"Taarifa ya Kuwaunga Mkono Watu wa Kongo (L.) Dhidi ya Ushambulizi wa Marekani" (Novemba 28, 1964), *Watu wa Ulimwengu, Unganeni na Muwashinde Washambulizi wa Kimarekani na Vibaraka Vyao Vyote.*

Chama cha Kikoministi cha China, baada ya kufanya makadirio ya makini ya hali ya ulimwengu na ya ndani ya nchi kwa msingi wa sayansi ya Kimarx-lenin, kimetambua kwamba mashambulizi yote ya wapinga maendeleo wa nchini na nchi za ng'ambo ni lazima yashindwe na yanawezekana kushindwa. Mawingu meusi yalipotokeza mbinguni, tulisema kwamba yalikuwa ya muda tu, kwamba giza mara litaondoka na jua litachomoza.

"Hali ya Mambo ya Sasa na Kazi Zetu" (Desemba 25, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika historia ya binadamu, nguvu zote za kipinga maendeleo zinapokuwa karibu na kuangamia haziwachi kufanya pigano la mwisho la kukata tamaa dhidi ya nguvu za kimapinduzi, na baadhi ya wana-mapinduzi watadanganyika kwa muda na hali hii ya nguvu za nje lakini dhaifu ndani, wakiwa hawafaulu kufahamu undani wa jambo kuwa

adui anakaribia kuangamia na wao wenyewe wanaujongelea ushindi.

"Kiwango cha Mgeuko Katika Vita vya Pili vya Dunia" (Oktoba 12, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ikiwa wao [Kuomintang] watapigana, tutawafyeka kwa ukamilifu. Hivi ndivyo mambo yalivyo: ikiwa watatushambulia na sisi kuwafyeka, basi wataridhika. Tukiwafyeka wachache, wataridhika kwa uchache; tukiwafyeka zaidi, wataridhika zaidi; tukiwafyeka wote, wataridhika kwa ukamilifu. Matatizo ya China yana mazonge mengi, na ubongo wetu lazima nao pia uwe na mazonge kidogo. Ikiwa wataanza kupigana, basi sisi turejeshe hujma, tupigane ili tupate amani.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Ikiwa mtu ye yote atatushambulia na kama hali yenyewe ni nzuri kwa mapigano, bila ya

shaka Chama chetu kitachukua msimamo wa kujihami na kumfyeka kwa uthabiti, moja kwa moja, wote na kwa ukamilifu (hatupigi ovyo ovyo, lakini tunapopiga, lazima tushinde). Tusitishwe kabisa na majigambo ya wapinga maendeleo.

"Juu ya Mazungumzo ya Amani na Kuomintang — Taarifa ya Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China" (Agosti 26, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kwa kadiri ya matakwa yetu sisi wenyewe, hatutaki kupigana hata kwa siku moja. Lakini kama hali zinatulazimisha kupigana, basi tunaweza kupigana mpaka mwisho.

"Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kimarekani Anna Louise Strong" (Agosti 1946), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Sisi tunataka amani. Lakini madhali ubeberu wa Kimarekani unakataa kuwacha

madai yake ya kijeuri na yasiyo na sababu na jungu lake la kupanua ushambulizi wake, njia ya pekee iliopo kwa watu wa China ni kubaki na azma ya kuendelea kupigana bega kwa bega pamoja na watu wa Korea. Sio kama sisi tunapenda vita, sisi tuko tayari kusita vita mara moja na kuyawacha masuala yaliobakia kutanzuliwa baadaye. Lakini ubeberu wa Kimarekani hauko tayari kufanya hivyo. Basi vizuri, wacha mapigano yaendelee. Kwa miaka yo yote ile ambayo ubeberu wa Kimarekani unataka kupigana, sisi tuko tayari kupigana nao mpaka utakapokuwa tayari kuwacha vita, mpaka wakati wa ushindi kamili kwa watu wa China na Korea.

Hotuba katika Mkutano wa Nne wa Kamiti ya Kwanza ya Taifa ya Baraza la Kushauriana Siasa la Watu wa China (Februari 7, 1953).

Lazima tuziondoshe fikra zote za kujidharau na kujidunisha miongoni mwetu. Mawazo yo yote yale ya kukadiria nguvu za

adui kuwa ni kubwa kuliko zilivyo na kuzikadiria nguvu za umma kuwa ni ndogo kuliko zilivyo ni ya makosa.

"Hali ya Mambo ya Sasa na Kazi Zetu" (Desemba 25, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Watu na mataifa yanayokandamizwa wasiyaweke matumaini yao ya ukombozi juu ya "busara" ya ubeberu na vibaraka vyake. Watafaulu kwa kuimarisha umoja wao na kuendeleza mapigano yao tu.

"Taarifa ya Kupinga Ushambulizi na Uuaji Uliofanywa na Marekani — Kikundi cha Ngo Dinh Diem Juu ya Watu wa Vietnam ya Kusini." (Agosti 29, 1963), *Watu wa Ulimwengu, Unganeni na Muwashinde Washambulizi wa Kimarekani na Vibaraka Vyao Vyote.*

Haidhuru lini vita vya ndani vya kiwango cha nchi nzima vitatokea, lazima tuwe tumeshajitayarisha vilivyo. Ikiwa vitaanza mapema, tuseme kesho asubuhi, basi vile

vile tuwe tayari. Hili ni jambo la kwanza. Kwa hali ya hivi sasa ya ulimwengu na ya nchini inayumkinika kuwa vita vya ndani ya nchi kwa muda vitakuwa si vikubwa na vitakuwa vya mahala fulani tu. Hili ni jambo la pili. Jambo la kwanza ni lile ambalo tujitayarishe nalo, jambo la pili ndilo lililokuwepo kwa muda mrefu. Kwa ufupi, lazima tuwe tumejitayarisha. Tukiwa tumeshajitayarisha tutaweza kupambana barabara na kila namna ya hali za mazonge.

"Hali ya Mambo na Siasa Yetu Baada ya Ushindi Katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Agosti 13, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

8. VITA VYA UMMA

Vita vya kimapinduzi ni vita vya umma, vinaweza kufanywa kwa kutia hamasa na kuutegemea umma tu.

"Shughulikia Maisha ya Umma na Angalia Namna za Kufanya Kazi" (Januari 27, 1934), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Nini ngome ya kweli ya chuma? Ni umma, ni mamilioni ya umma ambao kwa kweli na udhati wa nyoyo zao wanaunga mkono mapinduzi. Hiyo ndio ngome ya kweli ya chuma ambayo ni muhali, na ni muhali kabisa, kubomolewa na nguvu za namna yo yote. Wapinga mapinduzi hawawezi kutubomoa; kinyume, sisi tutawabomoa wao. Kwa kuyakusanya mamilioni kwa mamilioni ya umma kuwa pamoja na serikali ya kimapinduzi na kwa kuvipanua vita vyetu vya

kimapinduzi, tutaweza kuwafyeka wapinga maendeleo wote na kuitia China yote katika mikono yetu.

Kama juu.

Chemchemu kubwa kabisa ya nguvu za kufanya vita iko katika umma wa watu. Sababu kubwa kwa nini Japani inathubutu kutuonea ni kwamba umma wa China haujakusanywa. Upungufu huu utakapowekwa sawa, basi mshambulizi wa Kijapani — akiwa kama gombe jandawazimu linalojitia katika mzunguko wa moto — atazungukwa na mamia ya milioni ya watu wetu waliosimama imara, hata sauti yao peke yake tu itamtia hofu, na atateketezwa.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Jinsi wabeberu wanavyotuonea, hata itatubidi kupambana nao kwa vilivyo. Si kama tu ni lazima tuwe na jeshi la kawaida

lenye nguvu, lazima vile vile tujenge *division* za askari wa kujitolea wa umma [*militia*] kwa kiwango kikubwa. Kwa kufanya hivi itawawia taabu wabeberu kuweza kwenda hata inchi moja katika nchi yetu, endapo wakifanya ushambulizi.

Mazungumzo na mwandishi habari wa Shirika la Habari la Hsinhua (Septemba 29, 1958).

Kwa kuvikadiria vita vya kimapinduzi kwa jumla, vita vya kupigana hapa na hapa [*guerrilla*] vya umma na vile vya Jeshi Jekundu lililo nguvu kuu vinasaidiana kama mkono wa kulia na wa kushoto wa mtu, na kama tungelikuwa na Jeshi Jekundu peke yake lililo nguvu kuu bila ya vita vya kupigana hapa na hapa wa umma, tungelikuwa kama shujaa mwenye mkono mmoja. Kwa maneno ya wazi, na hususan kuhusu mapigano ya kijeshi, tunapotaja juu ya watu walioko katika maeneo ya vituo kama ni kitu muhimu, tunakusudia kwamba tunao watu wenye silaha. Hiyo ndio sababu muhimu kwa

nini adui anaogopa kuyasogelea maeneo ya vituo vyetu.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Bila ya suala lo lote, kushinda au kushindwa katika vita kunaamuliwa hasa na mambo ya kijeshi, siasa, uchumi na hali za maumbile za pande zote mbili. Lakini sio hizi tu. Uwezo wa pande zote mbili zenyewe katika kuongoza vita pia huleta uamuzi huo. Katika jitihada yake ya kutaka kushinda katika vita, bingwa wa kijeshi hawezi kukipindukia kikomo kilichowekwa na vitu vilivyopo; juu ya hivyo, katika kikomo hiki, anaweza na ni lazima apiganie ushindi. Jukwaa la vitendo la bingwa wa kijeshi limejengwa juu ya vitu hasa vilivyopo, lakini katika jukwaa hilo anaweza kuongoza michezo mingi, yenye sauti na nuru, yenye nguvu na fahari.

Kama juu.

Madhumuni hasa ya vita ni "kujilinda na kumwangamiza adui" (kumwangamiza adui ina maana ya kumnyang'anya silaha au "kumnyang'anya nguvu za upinzani", na haikusudii kuangamiza kiwiliwili cha kila adui). Katika vita vya siku za kale, ilitumiwa mkuki na ngao, mkuki kwa kumhujumu na kumwangamiza adui, na ngao kwa kujitetea na kujihifadhi. Mpaka hivi leo, silaha zote ni uendelezaji wa mkuki na ngao. Ndege ya kupiga mabomu, bunduki ya mtambo, mzinga wa kupiga masafa marefu na hewa ya sumu ni maendeleo ya mkuki; pahala pa kujificha wakati wa hujma kutoka hewani, kofia ya chuma, ngome ya saruji, na kifuniko cha uso cha kukinga hewa ya sumu ni maendeleo ya ngao. Tenki ni silaha ya kisasa inayochanganya kazi za mkuki na ngao. Kuhujumu ndio njia kuu ya kumwangamiza adui, lakini kujihami vile vile ni jambo la lazima. Katika kuhujumu, kusudio hasa ni kumwangamiza adui, lakini kwa wakati huo huo ni kujihifadhi, kwa sababu kama adui hajaangamizwa, utaangamizwa wewe. Katika kujihami, azimio hasa ni kujihifadhi, lakini kwa wakati

huo huo kujihami ni njia moja inayosaidia kuhujumu au kujitayarisha kuendea kuhujumu. Kurudi nyuma inahesabiwa katika kujihami na ni maendelezo ya kujihami; kufukuzia ni maendelezo ya kuhujumu. Ni lazima tuseme kwamba kumwangamiza adui ndio lengo la kwanza katika vita na kujihifadhi ni lengo la pili, kwa sababu ni kwa kumwangamiza adui kwa wingi tu ndio mtu anaweza kujihifadhi kikweli. Kwa hivyo, kuhujumu — njia kuu ya kumwangamiza adui — ndio jambo la kwanza, na kujihami — njia ya kusaidia kumwangamiza adui na njia ya kujihifadhi — ni jambo la pili. Katika vita hasa, kazi muhimu inafanywa katika kujihami kwa wakati mwingi na kufanya hujma kwa wakati uliobakia, lakini ukivichukulia vita kwa jumla, hujma ndio jambo lenye umuhimu wa kwanza.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu II.

Kanuni zote za uelekezo katika vitendo vya kijeshi zinatokana na kanuni moja ya

msingi: kujitahidi kwa kikomo cha nguvu zako kuhifadhi nguvu zako na kuziangamiza za adui. . . . Vipi basi tunahalalisha kuhimiza watu kujitolea mhanga kwa kishujaa katika vita? Kila vita vinatoa malipo yake, wakati mwengine ni makubwa sana. Jee jambo hili si kinyume na "kujihifadhi"? Kwa kweli, mambo haya hayatofautiani hata kidogo; kwa kusema kwa usahihi zaidi, kujitolea mhanga na kujihifadhi, mambo haya yanapingana na yanategemeana. Kwani mhanga kama huo ni jambo la lazima sio kwa kumwangamiza adui tu bali vile vile kwa kujihifadhi — "kutojihifadhi" kidogo na kwa muda (kutoa mhanga au malipo) na jambo la lazima kwa ajili ya hifadhi ya jumla na ya kudumu. Kutokana na kanuni hii ya msingi tunapata kanuni kadha wa kadha za uongozi katika hatua za kijeshi — kutoka kanuni za kupiga risasi (kujificha ili kujihifadhi, kutumia vilivyo nguvu za silaha ili kumwangamiza adui) mpaka kanuni za hila ya jumla ya vita — zote zimetawaliwa na kanuni hii ya msingi. Kanuni zote zilizohusu ufundi, mbinu, kampeni, hila ya jumla ya vita,

zinawakilisha utekelezaji wa kanuni hii ya msingi. Kanuni ya kujihifadhi na kumwangamiza adui ndio msingi wa kanuni zote za kijeshi.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya *Guerrilla* Dhidi ya Japani" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kanuni zetu za kijeshi ni:

(1) Kwanza shambulia vikosi vya adui vilivyotawanyika na vilivyotengana; baadaye shambulia vikosi vya adui vilivyokusanyika na vyenye nguvu.

(2) Kwanza iteke miji midogo na ya wastani na maeneo makubwa ya mashamba; baadaye iteke miji mikubwa.

(3) Lengo letu kubwa liwe kufyeka nguvu za adui zenye uwezo wa kupigana; tusifanye, kushika au kuteka mji au mahala, kuwa ni lengo letu kubwa. Kushika au kuteka mji au pahala ni matokeo ya kuzifyeka nguvu kubwa za adui, na mara nyingi mji au pahala huweza kushikwa au kutekwa moja kwa

moja baada ya kubadilishana mikono kwa mara nyingi.

(4) Katika kila mapigano, tumilia nguvu kubwa kabisa (mara mbili, tatu, nne, na mara nyengine hata tano au sita kuliko zile za adui), vizunguke vikosi vya adui kwa ukamilifu, jitahidi kuvifyeka kwa ukamilifu na usimwachie hata mmoja wao kukimbia. Katika hali maalum, tumilia njia ya kumpiga adui pigo la uangamizi, yaani kusanya nguvu zote katika kufanya ushambulizi wa uso kwa uso na vile vile mshambulie adui kwa upande mmoja au pande mbili, kwa makusudio ya kufyeka sehemu moja ya adui na kuiporomosha nyengineo ili jeshi letu liweze kupeleka vikosi vyake upesi upesi kwenda kuangamiza nguvu nyengine za adui. Jaribu kuviepuka vita vya kuchokesha ambavyo ndani yake tunapata hasara zaidi kuliko faida au hasara na faida kuwa sawa. Kwa njia hii, ingawa sisi ni dhaifu kwa jumla (kwa kuchukulia idadi), tutakuwa na nguvu kubwa kabisa katika kila sehemu moja na kila kampeni maalum, na njia hii inahakikisha

ushindi wa kampeni. Kila wakati ukipita, tutaweza kuwa na nguvu kubwa kwa jumla na mwishowe kuwafyeka maadui wote.

(5) Usifanye mapigano yo yote bila ya kujitayarisha, usifanye mapigano yo yote ambayo huna hakika ya kushinda; fanya kila jitihada ya kuwa tayari kwa kila pigano, fanya kila jitihada ya kuhakikisha kupata ushindi kwa kulinganisha hali zetu na za maadui.

(6) Ukuze vilivyo mtindo wetu wa kupigana — ushujaa katika mapigano, kutoogopa kujitolea mhanga, kutoogopa machofu na kupigana kwa mfululizo (yaani kufanya mapigano kwa mfululizo katika muda mfupi bila ya kupumzika).

(7) Jitahidi kumfyeka adui wakati anapokuwa mwendoni. Kwa wakati huo huo, angalia vizuri mbinu za kushambulia kutoka mahali fulani na kuteka vituo vya kivita vya adui na miji ya adui.

(8) Kuhusu upande wa kuishambulia miji, viteke kwa uthabiti vituo vyote vya kivita na miji yote ya adui yenye

himaya dhaifu. Katika nyakati zinazofaa, teka vituo vyote vya kivita na miji yote ya adui yenye himaya ya wastani, ikiwa hali ya mambo inaruhusu. Kuhusu vituo vyote vya kivita na miji yote ya adui yenye himaya kubwa, ngoja mpaka wakati utakapopevuka na hapo tena uviteke.

(9) Tuzijalize nguvu zetu kwa silaha zote na wingi wa mateka kutoka kwa adui. Chanzo kikuu cha watu na zana za vita kwa jeshi letu kiko kwenye medani.

(10) Tumilia vizuri wakati baina ya kampeni moja na nyengine kwa ajili ya kupumzika, kufanya mazoezi ya kijeshi na kuviimarisha vikosi vyetu. Nyakati za mapumziko, mazoezi na maimarisho kwa kawaida zisiwe ndefu sana, na adui kwa kiasi kinachoyumkinika asiwachiliwe nafasi hata ya kupumua.

Hizi ndio njia muhimu lilizozitumia Jeshi la Ukombozi la Umma kumshindia Chiang Kai-shek. Ni matokeo ya kushajiishwa kwa Jeshi la Ukombozi la Umma katika miaka mingi ya mapigano dhidi ya adui wa

ndani ya nchi na nje na zinafaa kabisa katika hali yetu ya hivi sasa. . . . Hila yetu ya jumla na mbinu zetu za vita zimejengwa juu ya msingi wa vita vya umma; jeshi lo lote linalopinga umma haliwezi kutumilia hila yetu ya jumla na mbinu zetu za vita.

"Hali ya Mambo ya Sasa na Kazi Zetu" (Desemba 25, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Bila ya kujitayarisha, kuzidi nguvu si kuzidi nguvu kwa kweli na wala hapana juhudi ya kuanza jambo. Baada ya kulifahamu jambo hili, nguvu dhaifu lakini zilizojitayarisha, mara nyingi zinaweza kumshinda adui mwenye nguvu kwa hujma ya ghafla.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

9. JESHI LA UMMA

Bila ya jeshi la umma, hapana cho chote cha umma.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Jeshi hili lina nguvu kwa sababu watu wake wote wana fahamu ya nidhamu; wamekusanyika pamoja na wanapigania sio maslaha ya kibinafsi ya watu wachache au kikundi kidogo, bali maslaha ya umma mkubwa wa watu na ya taifa zima. Azma pekee ya jeshi hili ni kusimama imara pamoja na watu wa China na kuwatumikia kwa moyo mmoja.

Kama juu.

Jeshi Jekundu la China ni kundi lenye silaha la kutekeleza kazi za kisiasa za mapinduzi. Hasa katika wakati tulio nao, kazi za Jeshi Jekundu sio kupigana tu; zaidi ya kupigana kuziangamiza nguvu za kijeshi za adui, lazima lichukue majukumu muhimu kama vile kueneza siasa miongoni mwa umma, kuwakusanya kwa nidhamu, kuwapa silaha na kuwasaidia kuanzisha serikali ya kimapinduzi na matawi ya Chama cha Kikoministi. Jeshi Jekundu halipigani kwa ajili ya kupigana tu, bali kwa sababu ya kueneza siasa miongoni mwa umma, kuwakusanya kwa nidhamu, kuwazatiti kwa silaha na kuwasaidia kuanzisha serikali ya kimapinduzi. Bila ya malengo yalioelezwa juu, vita vinapoteza maana yake na Jeshi Jekundu linakuwa halina sababu ya kuweko kwake.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Jeshi la Ukombozi la Umma siku zote ni kikosi cha mapigano. Hata baada ya kupatikana ushindi nchini kote, jeshi letu

litaendelea kuwa ni kikosi cha mapigano katika kipindi cha historia ambapo matabaka hayajaondolewa nchini kwetu na mpango wa kibeberu bado unaendelea duniani. Juu ya jambo hili pasiwe na kutofahamu au kuyumba yumba hata kidogo.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Sisi tunalo jeshi la kupigana na vile vile tunalo jeshi la kufanya kazi za sulubu. Kwa mapigano, tunalo Jeshi la Njia ya Nane na Jeshi Jipya la Nne; lakini hata wao wanafanya kazi mbili, mapigano na uchumi. Kwa majeshi ya aina hizi mbili, na kwa jeshi lililokuwa na ustadi katika kazi hizi mbili pamoja na katika kazi kuhusu umma, tunaweza kuzivuka shida zetu na kuushinda ubeberu wa Kijapani.

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ulinzi wa taifa letu utaimarishwa na hapana beberu atayewachiliwa kuishambulia nchi yetu tena. Nguvu zetu za silaha za umma lazima ziendelezwe na zikuzwe, na Jeshi la Ukombozi la Umma la kishujaa na lililopitia mitihani mingi likiwa ndio msingi wake. Sio kama tutakuwa na jeshi lenye nguvu la nchi kavu tu bali vile vile jeshi la hewani lenye nguvu na jeshi la wanamaji lenye nguvu.

Hotuba ya ufunguzi katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Baraza la Kushauriana Siasa la Watu wa China (Septemba 21, 1949).

Kanuni yetu ni kuwa Chama kinaamuru bunduki, na daima bunduki isiruhusiwe kuamuru Chama.

"Matatizo ya Vita na Hila ya Jumla ya Vita" (Novemba 6, 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Maofisa na wapiganaji wetu wote lazima daima wakumbuke kwamba sisi ni Jeshi

la Ukombozi la Umma lililo tukufu, sisi ni vikosi vinavyoongozwa na Chama cha Kikoministi cha China kitukufu. Madhali siku zote tunafuata maongozi ya Chama, hakika tutashinda.

"Tangazo Kuu la Jeshi la Ukombozi la Umma la China" (Oktoba 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

10. UONGOZI WA KAMITI ZA CHAMA

Mpango wa kamiti za Chama ni mpango muhimu wa Chama kwa ajili ya kuhakikisha uongozi wa pamoja na kuzuia uendeshaji wa kazi kuhodhiwa na mtu fulani binafsi. Hivi karibuni imegundulikana kwamba katika baadhi (bila ya shaka sio yote) ya maidara ya uongozi ni kawaida ya mtu fulani kuhodhi uendeshaji wa kazi na kukata shauri juu ya matatizo muhimu. Matanzuo ya matatizo muhimu yanakatwa shauri sio na mikutano ya kamiti ya Chama bali na mtu mmoja, na uwanachama katika kamiti ya Chama umebaki jina tu. Maoni tofauti kati ya wanachama wa kamiti hayawezi kutanzuliwa na yameachwa kwa muda mrefu bila ya kutanzuliwa. Wanachama wa

kamiti ya Chama wanakuwa na umoja wa kiwanachama tu, na wala hapana umoja wa kweli. Hali hii lazima ibadilike. Kutoka sasa, mpango madhubuti wa mikutano ya kamiti ya Chama lazima uanzishwe katika maidara yote ya uongozi, kutoka ofisi kuu za mikoa za Kamiti Kuu mpaka kamiti za Chama za utawala wa wilaya; kutoka kamiti za Chama za medani mpaka kamiti za Chama za *brigade* na maeneo ya kijeshi (tume ndogo za Tume ya Kijeshi ya Kimapinduzi au vikundi vya uongozi); na vikundi vinavyowakilisha Chama katika maidara ya serikali, jumuiya za umma, shirika ya utoaji habari na ofisi za magazeti. Matatizo yote muhimu (bila ya shaka, si matatizo madogo madogo yasio muhimu, au matatizo ambayo yamekwisha jadiliwa na kukatwa shauri katika mikutano na iliobaki ni kutekelezwa tu) yapelekwe kujadiliwa kwenye kamiti, na wanachama wa kamiti waliohudhuria watoe maoni yao kwa ukamilifu na wafikilie maazimio halisi na tena yatekelezwe na wanachama wanaohusika. . . . Mikutano ya kamiti za Chama igawiwe namna mbili,

mikutano ya kamiti ya kawaida na mikutano mikuu, na namna hizi mbili zisibabaishwe. Zaidi ya hayo, tuchukue hadhari kati ya uongozi wa pamoja na dhamana ya mtu, kisitiliwe nguvu kimoja na kupuuzwa cha pili. Katika jeshi, yule mtu mwenye amri anayo haki ya kuchukua hatua linapotokea jambo la haraka wakati wa mapigano na wakati hali ya mambo inapohitajia.

"Juu ya Kuimarisha Mpango wa Kamiti za Chama" (Septemba 20, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katibu wa kamiti ya Chama lazima awe hodari katika kuwa "mkuu wa skodi". Kamiti ya Chama ina wanachama kumi mpaka ishirini; ni kama skodi moja katika jeshi, na katibu ni kama "mkuu wa skodi". Hakika kabisa si rahisi kuiongoza skodi hii barabara. Kila ofisi kuu au ofisi ndogo ya mkoa ya Kamiti Kuu sasa inaongoza eneo kubwa na inabeba majukumu mazito sana. Kazi za kuongoza

hazikusudiwi kuamua siasa kuu au siasa maalum tu, bali vile vile kuvumbua njia barabara za kufanyia kazi. Hata tukiwa na siasa kuu na siasa maalum zilizo barabara, matata yanaweza kutokea ikiwa njia za kufanyia kazi zitapuuzwa. Kwa ajili ya kutekeleza kazi yake ya kutoa uongozi, kamiti ya Chama lazima iwategemee "wanachama wa skodi" na kuzitumia nguvu zao kwa ukamilifu. Ili kuwa "mkuu wa skodi" mzuri, katibu inampasa ajifunze kwa bidii na afanye uchunguzi kwa ukamilifu. Katibu au katibu mdogo atahisi taabu sana kuiongoza "skodi" yake vyema kama hakuchukua hadhari ya kufanya kazi ya uenezi siasa na matengenezo miongoni mwa "wanachama wa skodi" yake mwenyewe, kama si hodari wa kuangalia mahusiano yake na wanachama wa kamiti au hajifunzi namna ya kuongoza mikutano vyema. Kama "wanachama wa skodi" hawafuati hatua sawa sawa, basi hawawezi kutarajiwa asilani kuongoza makumi ya mamilioni ya watu katika mapigano na ujenzi. Bila ya shaka, mahusiano baina ya katibu na wanachama

wa kamiti ni yale ya wachache kuwasikiliza wengi, kwa hivyo ni tofauti na mahusiano baina ya mkuu wa skodi na maaskari. Hapa tunasema kwa njia ya kufananisha tu.

"Njia za Kufanyia Kazi za Kamiti za Chama" (Machi 13, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Weka matatizo juu ya meza. Jambo hili sio lifanywe na "mkuu wa skodi" peke yake tu, bali vile vile na wanachama wa kamiti. Usiwaseme watu nyuma ya mgongo wao. Wakati wo wote yanapotokea matatizo, ita mkutano, yawekwe matatizo juu ya meza kwa ajili ya majadiliano, kata maazimio na matatizo yatatanzuliwa. Ikiwa yapo matatizo na hayawekwi mezani, basi yatabaki kwa muda mrefu, hata kuendelea kwa miaka, bila ya kutanzuliwa. "Mkuu wa skodi" na wanachama wa kamiti wafahamiane katika mahusiano yao. Hapana kitu muhimu zaidi kama vile kuwepo hali ya kufahamiana, kusaidiana na kupendana baina ya katibu na wanachama wa kamiti, baina ya Kamiti Kuu na ofisi kuu za mikoa

na baina ya ofisi kuu za mikoa na kamiti za Chama za eneo.

Kama juu.

"Peaneni habari". Hii ina maana kwamba wanachama wa kamiti ya Chama wapeane habari na kubadilishana maoni juu ya mambo waliyoyasikia. Jambo hili lina umuhimu mkubwa katika kupata lugha ya kufahamiana. Baadhi ya watu hawafanyi hivyo, wao ni kama wale watu aliowasema Lao Tzu, "hawatembeleani maisha yao yote, ijapokuwa muwiko wa majogoo wao na mikemeo ya mbwa wao inaweza kusikilikana kutoka kwa mmoja kwenda kwa mwengine". Matokeo yake ni kwamba wanakuwa hawana lugha ya kufahamiana.

Kama juu.

Waulize walio chini yako mambo usiyoyafahamu au usiyoyajua, na usionyeshe kukubali au kutokubali kwako kwa upesi upesi. . . . Tusijidai asilani kujua tusichokijua, "tusione haya kuuliza na kujifunza kutoka

kwa watu walio chini yetu" na tusikilize kwa makini maoni ya makada wa daraja za chini. Kuwa mwanafunzi kabla ya kuwa mwalimu; jifunze kutoka kwa makada wa daraja za chini kabla ya kutoa amri. . . . Maoni yao yanaweza kuwa barabara au si barabara; baada ya kusikiliza, lazima tuyachambue. Lazima tuyasikilize maoni mema na kuyatekeleza. . . . Sikiliza vile vile maoni yenye makosa yanayotoka chini; ni kosa kutoyasikiliza kabisa. Juu ya hivyo, maoni kama hayo yasifuatwe bali yatolewe makosa.

Kama juu.

Jifunze "kupiga piano". Katika kupiga piano vidole vyote kumi huwa kazini; haina faida kuvisogeza baadhi ya vidole na kuviacha vingine. Lakini ikiwa vidole vyote kumi vitapiga kwa pamoja, hapatakuwa na muziki. Ili kuleta kupiga muziki mtamu, vidole vyote kumi havina budi kupiga kwa mpango na kwa kushirikiana. Kamiti ya Chama lazima iishike barabara kazi yake kuu na kwa wakati huo huo,

pamoja na kazi yake kuu, ianze kazi katika mambo mengine. Hivi sasa, inatulazimu kuangalia mambo mengi; lazima tuangalie kazi iliopo katika maeneo, majeshi na maidara yote, kwa hivyo tusijishughulishe na matatizo machache tu, na kuyaacha mengineo. Po pote penye matatizo, lazima tuyabane na njia hii tujifunze barabara. Baadhi ya watu hupiga piano vizuri na wengine vibaya, na iko tofauti kubwa katika muziki wanaopiga. Wanachama wa kamiti za Chama lazima wajifunze "kupiga piano" vizuri.

Kama juu.

"Shika vyema." Hiyo ni kusema kwamba kamiti ya Chama si kama lazima "ishike" tu, bali lazima "ishike vyema" kazi zake muhimu. Mtu hawezi kukidhibiti kitu mpaka awe anakishika vizuri, bila ya kuachia hata kidogo. Kutoshika vyema ni sawa sawa na kutoshika kabisa. Bila ya shaka, mtu hawezi kushika kitu kwa kiganja kilichotanuliwa. Mkono unapofumbwa kama unataka kukamata kitu lakini ikiwa haukufumbatwa vizuri, basi

bado hapana kitu kinachokamatwa. Baadhi ya makomredi wetu hushika kazi zao kuu, lakini kushika kwao si imara na kwa hivyo hawawezi kufaulu katika kazi zao. Haitofaa kutoshika kabisa, na wala haitofaa kama ushikaji wenyewe si imara.

Kama juu.

"Kuwa na kichwa cha hesabu." Hii ina maana ya kusema kwamba, lazima tuangalie upande wa idadi ya hali ya mambo na tatizo na tufanye uchambuzi wa msingi wa idadi. Kila ubora wa vitu hujidhihirisha kwa idadi fulani, na bila ya idadi hapawezi kuwa na ubora. Mpaka hivi leo makomredi wetu wengi bado hawajafahamu kwamba lazima waangalie upande wa idadi ya vitu — hesabu ya msingi, kadiri kwa kila mia ya hesabu muhimu na kiwango cha idadi kinachokata shauri juu ya ubora wa vitu. Hawana "hesabu" kichwani mwao na matokeo ni kwamba hawawezi kuepuka kufanya makosa.

Kama juu.

"Taarifa ya Kuwapa Moyo Watu." Taarifa ya mkutano itolewe kabla; hii ni kama kutoa "Taarifa ya Kuwapa Moyo Watu", ili kila mmoja ajue nini kitazungumzwa na matatizo gani yanataka kutanzuliwa na apate kujitayarisha mapema. Baadhi ya mwahala, mikutano ya makada hufanywa kabla kwanza kutayarisha ripoti na kuandika muswada wa maazimio, na ni baada ya watu kufika kwenye mkutano tu ndio mambo yanatungwa papo hapo; jambo hili ni kama ule msemo, "Vikosi na farasi wamefika, chakula na ukoka bado si tayari", na hilo si jambo zuri. Usifanywe mkutano kwa haraka kama matayarisho hayajakamilika.

Kama juu.

"Vikosi vya kijeshi vichache vilivyo bora na kurahisisha kazi za utawala." Mazungumzo, hotuba, makala na maazimio yote yawe mafupi na fasaha. Mikutano vile vile isiendelee kwa muda mrefu sana.

Kama juu.

Shughulikia kuungana na kufanya kazi pamoja na walė makomredi wanaohitilafiana nawe. Jambo hili linataka liangaliwe katika serikali za kienyeji na jeshi. Vile vile ni mwafaka kwa mahusiano na watu walio nje ya Chama. Tumekusanyika kutoka kila pembe ya nchi na inatupasa tuwe mahodari kwa kuungana katika kazi zetu sio na wale makomredi wenye maoni sawa na yetu tu lakini vile vile na wale wenye maoni tofauti.

Kama juu.

Jihadhari na majivuno. Kwa mtu ye yote mwenye madaraka ya uongozi, hili ni jambo la kanuni na pia ni kitu muhimu kwa ajili ya kuudumisha umoja. Hata wale ambao hawakufanya makosa makubwa na wamepata mafanikio makubwa katika kazi zao wasiwe na majivuno.

Kama juu.

Weka mipaka miwili ya mpambanuo. Kwanza, baina ya mapinduzi na upingaji

mapinduzi, baina ya Yenan na Sian.[1] Baadhi ya watu hawaelewi kwamba lazima waweke mpaka huu wa mpambanuo. Kwa mfano, wanapopinga ubwana-serikali, wanazungumza juu ya Yenan kama vile "hapana lo lote lililokuwa sawa" kule na hawafaulu kulinganisha na kupambanua ubwana-serikali wa Yenan na wa Sian. Hii kwa msingi ni makosa. Pili, miongoni mwa wana-mapinduzi ni wajibu kuweka mpambanuo safi baina ya haki na makosa, baina ya mafanikio na upungufu na kuweka wazi lipi ni kubwa na lipi ni dogo kati yao. Kwa mfano, mafanikio yanatimia 30 katika mia au 70 katika mia ya mambo yote kwa jumla? Haitoleta maana kupunguza sana

---

[1] Yenan ilikuwa ndio makao makuu ya Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China kutoka Januari mwaka 1937 mpaka Machi mwaka 1947; Sian ilikuwa ndio kiini cha utawala wa wapinga maendeleo wa Kuomintang katika China ya kaskazini ya magharibi. Komredi Mao Tsetung ameitaja miji hii miwili kama ni mfano wa mapinduzi na upingaji mapinduzi.

au kuzidisha sana. Lazima tuwe na msingi wa kukadiria kazi ya mtu na kusema kama mafanikio yake ni 30 katika mia na makosa yake ni 70 katika mia, au kinyume cha hivyo. Ikiwa mafanikio yake yanafikia 70 katika mia ya yote, basi kazi yake kwa jumla isifiwe. Itakuwa ni makosa kabisa kuisema kazi ambayo mafanikio ni makubwa kuwa makosa ndio makubwa. Katika kuyakabili matatizo kabisa tusisahau kuweka mipaka hii miwili ya mpambanuo baina ya mapinduzi na upingaji mapinduzi na baina ya mafanikio na upungufu. Tutaweza kuendesha mambo vizuri ikiwa tutaiweka akilini mipambanuo hii miwili; kama si hivyo tutababaisha tabia ya matatizo. Kwa ajili ya kufanya mipambanuo hii vyema, bila ya shaka inahitaji kujifunza kwa uangalifu na kufanya uchambuzi. Tabia yetu kuhusu kila mtu na kila jambo iwe ile ya kufanya uchambuzi na kusoma kwa makini.

Kama juu.

Katika upande wa matengenezo, hakikisha kwa dhati udemokrasi chini ya uongozi. Ufanywe kwa misimamo ifuatayo:

(1) Idara za uongozi za Chama lazima zitoe misimamo sahihi ya uongozi na zitafute njia za kutanzulia matatizo yanapotokea, ili kujengwa kuwa ndio kiini cha uongozi.

(2) Idara za juu ziijue hali ilivyo katika idara za chini na maisha ya umma ili ziwe na msingi wa uongozi sahihi uliojengwa juu ya hali ya mambo ilivyo hasa.

(3) Idara ya Chama ya daraja yo yote isikate maazimio katika kutanzua matatizo bila ya kufikiri vizuri. Mara baada ya maazimio kukatwa, lazima yatekelezwe kwa dhati.

(4) Idara za juu za Chama zinapokwisha kata shauri lo lote muhimu lazima zizipelekee azimio lao bila ya kuchelewa idara za chini na umati wa wanachama wa Chama. . . .

(5) Idara za chini za Chama na umati wa wanachama wa Chama lazima wazungumze kwa urefu juu ya maongozi ya

idara za juu ili kufahamu vyema madhumuni yake na kukata shauri juu ya njia za kuyatekeleza.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

11. MSIMAMO WA KIUMMA

Umma, na ni umma tu, ndio nguvu za kusonga mbele katika kufanya historia ya ulimwengu.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Umma ndio mashujaa wa kikweli, na sisi wenyewe mara nyingi huwa na mambo ya kitoto na wajinga, na bila ya kulifahamu jambo hili ni muhali kupata hata ule ujuzi wa mwanzo kabisa.

"Dibaji na Maelezo Zaidi Juu ya *Uchunguzi wa Mashambani*" (Machi na Aprili 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Umma wa watu una busara zenye uwezo usio na kikomo. Wanaweza kujikusanya na wakashughulikia kila mwahala na idara ya kazi ambamo wanaweza kuzitumia nguvu zao barabara; wanaweza kujishughulisha kwa marefu na mapana katika mambo ya uchumi na kufanya mambo mengi zaidi na zaidi ya kuinua maisha yao.

Maelezo ya utangulizi katika "Mfuriko wa Nguvu za Kazi Umepata Njia ya Kutumika" (1955).

Muinuko wa hivi sasa wa vugu vugu la wakulima ni tukio kubwa kabisa. Baada ya muda mfupi tu ujao, katika majimbo ya kati, kusini na kaskazini ya China, mamia kadha ya mamilioni ya wakulima watainuka kama dharuba kubwa, kama kimbunga, nguvu iendao mbio sana na kubwa mno hata hapana nguvu yo yote ilio kubwa vipi itayoweza kuizuia. Wakulima wataivunjilia mbali minyororo yote inayowafunga na watasonga mbele kwa haraka kuendea kwenye njia ya ukombozi. Watawasukuma kaburini

wabeberu, mabwana-vita, maofisa waovu walao rushwa, wakandamizi wa kienyeji na mabwanyenye waovu wote. Kila chama cha kimapinduzi na kila komredi wa kimapinduzi atatiwa mtihanini, kukubaliwa au kukataliwa nao watakavyokata shauri. Kuna mambo matatu ya kuyachagua. Jee utasonga mbele na kuwaongoza? Utawafuata nyuma ukifanya ishara za dharau na kuwaponda? Au utawaziba njia na kuwapinga. Kila Mchina ni huru kuchagua atakavyo, lakini matukio ya mambo yatamlazimisha kuchagua kwa haraka jambo moja katika hayo matatu.

"Ripoti Juu ya Uchunguzi wa Vugu Vugu la Wakulima wa Hunan" (Machi 1927), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Wimbi kubwa la mabadiliko ya kijamii katika mashamba, wimbi kubwa la ushirika, limekwisha fika baadhi ya mwahala na karibu litaikumba nchi nzima. Hili ni vugu vugu kubwa la mapinduzi ya kisoshalisti

linalohusu umati wa mashambani uliopindukia watu 500 milioni, na lina umuhimu mkubwa kabisa kwa ulimwengu mzima. Inatuwajibikia tuliongoze vugu vugu hili kwa nguvu, bidii na kwa mpango, na wala tusilirejeshe nyuma kwa njia hii au ile. Baadhi ya makosa hayaepukiki katika mwenendo huu; hili ni jambo linalofahamika, na haitokuwa taabu kuyasahihisha. Mambo ya upungufu au makosa yaliopo miongoni mwa makada na wakulima yanaweza kutibiwa au kusahihishwa iwapo tutawapa msaada wa kufaa.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Umma una mapenzi yaliojaa bidii kubwa kabisa kwa usoshalisti. Wale wanaoweza kufuata tu kawaida za kizamani za kufanya kazi hawawezi kabisa katika nyakati hizi za kimapinduzi kuona hamasa hii. Wao ni vipofu, na mbele yao ni kiza kitupu. Baadhi ya wakati hata wanafika hadi ya kupindua mambo chini juu na cheusi kukigeuza cheupe. Jee hatukuwaona watu kama hao

kwa kutosha? Watu kama hao wanaofuata kawaida za kizamani siku zote huikadiria hamasa ya umma kuwa ni ndogo kuliko ilivyo. Kinapotokea kitu kipya wao huwa hawakikubali na hukazana kukipinga. Baadaye, inawabidi wakubali kwamba wameshindwa na kujitoa makosa kidogo. Lakini mara kinapotokea kitu kipya chengine, wao huyafanya yale yale. Huu ni mpango wa tabia yao katika kukikabili kitu cho chote kinachotokea. Watu kama hao siku zote huwa hawana la kufanya wanapokabiliwa na tatizo, siku zote hushindwa kusonga mbele katika wakati wa shida, na siku zote lazima wasukumwe kwa nguvu kabla hawajaenda mbele hatua moja.

Maelezo ya utangulizi katika "Mji Mdogo Huu Wote Umeingia Katika Ushirika Mnamo Muda wa Miaka Miwili Tu" (1955).

Kwa muda wa zaidi ya miaka ishirini Chama chetu kila siku kimekuwa kikifanya kazi ya kiumma, na kwa zaidi ya miaka kumi iliopita kimekuwa kikikariri kusema

juu ya msimamo wa kiumma. Daima tumeshikilia kwamba mapinduzi lazima yategemee umma wa watu, kila mtu ashiriki, na tumepinga kuachiliwa watu wachache tu kutoa amri. Lakini juu ya hivyo, msimamo wa kiumma bado haujatekelezwa kwa ukamilifu katika kazi za baadhi ya makomredi; bado wangali wakitegemea watu wachache wanaofanya kazi peke yao. Sababu moja ni kwamba wao siku zote hawataki kulieleza lo lote walifanyalo kwa watu wanaowaongoza na kwamba wao hawafahamu kwa nini na vipi wazitumie juhudi na busara zenye uwezo za wale wanaowaongoza. Kwa kufikiri tu, wao pia wanataka kila mtu ashiriki katika kazi, lakini hawawaachilii watu wengine kujua jambo gani linataka kufanywa au vipi kulifanya. Mambo yakiwa ni hivyo, namna gani anaweza kila mtu kutarajiwa kuingia mbioni na vipi kinaweza cho chote kufanywa vyema? Ili kulitanzua tatizo hili, bila ya shaka, ni jambo la msingi kuwapa mafunzo ya kifikra juu ya msimamo wa kiumma, lakini kwa wakati huo huo hatuna budi

kuwafundisha makomredi hawa njia nyingi hasa za kufanyia kazi.

"Mazungumzo na Wahariri wa *Gazeti la Kila Siku la Shansi-Suiyuan*" (Aprili 2, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Maarifa ya miaka ishirini na nne yanatusomesha kwamba kazi sahihi, siasa sahihi na mtindo barabara wa kazi siku zote hulingana na matakwa ya umma ya wakati na mwahala maalum na siku zote hutilia nguvu mahusiano yetu na umma, na kazi isio sahihi, siasa isio sahihi na mtindo wa kazi usio sahihi siku zote ni mambo yasiokubaliana na matakwa ya umma kwa wakati na mwahala maalum, na siku zote yanatengana na umma. Sababu kwa nini maovu kama mambo ya kufuata kikasuku maneno ya vitabuni, kufuata maarifa ya zamani tu, mambo ya kuamrisha-amrisha, kufuata kama mkia, fikra za kufuata madhehebu, ubwana-mkubwa wa kiofisi na tabia ya majivuno katika kazi

hakika ni mambo yenye madhara na hayawezi kuvumiliwa, kwa hivyo ye yote anayekumbwa na maradhi haya lazima ayashinde, kwa sababu mambo haya yanatutenga na umma.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kwa ajili ya kujifungamanisha na umma, mtu ni lazima atende kwa mujibu wa haja na hiari ya umma. Kazi yo yote inayofanywa kwa ajili ya umma haina budi itokane na haja zao na sio kutokana na nia ya mtu fulani, hata ikiwa nia hiyo ni nzuri vipi. Mara nyingi inatokea kuwa, kwa mujibu wa hali ya mambo, umma unahitajia mabadiliko fulani, lakini kwa ndani ya roho zao bado hawajaitambua haja ile, bado hawakuwa tayari au hawana azimio la kuleta mabadiliko hayo. Katika hali kama hiyo, inatubidi tungoje kwa subira. Tusifanye mabadiliko hayo mpaka, kwa kupitia kazi yetu, sehemu kubwa ya umma wawe wametambua haja ile na wana nia na azimio la kuitekeleza. Kama si hivyo

tutajitenga na umma. Madhali hawajafahamu na wakawa na nia, basi kazi inayowataka washiriki itakuwa ni jambo la kufuata tu na haitofaulu. . . . Kuna kanuni mbili hapa: moja ni haja hasa za umma na wala sio tunalofikiria kwamba wanalihitaji, na pili ni hiari ya umma ambayo ni juu yao wenyewe kukata shauri badala ya sisi kuwakatia shauri.

"Muungano wa Pamoja Katika Kazi ya Utamaduni" (Oktoba 30, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mkutano wetu unahitajika kutoa mwito kwa Chama kizima kuwa macho na kuangalia kwamba hapana komredi katika kazi yo yote ambaye amejitenga na umma. Hauna budi umfunze kila komredi kuupenda umma wa watu na kuisikiliza vyema sauti ya umma; ajitambulishe nafsi yake na umma po pote anapokwenda na, badala ya kujiweka juu yao, ajitie miongoni mwao; na kwa mujibu wa daraja yao ya sasa, awaamshe au ainue fahamu yao ya siasa na awasaidie kidogo

kidogo kujikusanya kwa hiari yao na kuendeleza hatua kwa hatua mapigano yote yanayohitajika ambayo yanaruhusiwa na hali ya mambo ya ndani na ya nje ya wakati na mwahala maalum.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ikiwa tunajaribu kuhujumu katika wakati ambapo umma bado haujaamka, jambo hilo litakuwa ni ujasiri. Ikiwa tunashikilia kuongoza umma kufanya jambo lo lote lile lisilokubaliwa nao, bila ya shaka hatutofaulu. Ikiwa hatusongi mbele wakati umma unataka kusonga mbele, jambo hilo litakuwa ni upotovu wa Upande wa Kulia.

"Mazungumzo na Wahariri wa *Gazeti la Kila Siku la Shansi-Suiyuan*" (Aprili 2, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Mambo ya kuamrisha-amrisha ni makosa katika aina yo yote ya kazi, kwa sababu kufanya hivyo ni kupindukia kiwango cha

ufahamu wa siasa wa umma na ni kwenda kinyume na kanuni ya umma kushiriki katika vitendo kwa hiari zao, jambo hili linadhihirisha ugonjwa wa papara papara. Makomredi wetu lazima wasifikirie kuwa umma unafahamu kila kitu wanachokifahamu wao. Ni lazima tuingiliane na umma na tufanye uchunguzi ili tupate kugundua kwamba umma umelifahamu jambo hilo au la na wako au hawako tayari kuchukua hatua. Ikiwa tutafanya hivyo, tutaweza kuepusha mambo ya uamrishaji. Kufuata kama mkia katika aina yo yote ya kazi vile vile ni makosa, kwa sababu kufanya hivyo ni kwenda chini kuliko daraja ya ufahamu wa siasa wa umma na kuivunja kanuni ya kuuongoza mbele umma, basi unajidhihirisha ugonjwa wa uzembe. Makomredi wetu inawawajibikia kutochukulia kwamba umma haufahamu yale ambayo wao wenyewe hawayafahamu. Mara nyingi hutokea kwamba umma mkubwa unatupita sisi na una hamu zaidi ya kusonga mbele hatua moja na kwamba juu ya yote hayo makomredi wetu hawafaulu kuwa viongozi wa umma mkubwa bali wanawafuata kama mikia baadhi ya watu

walio nyuma kwa fikra, wakiyaleta maoni ya watu wale na, zaidi ya hayo, kufanya makosa ya kuyafikiria maoni hayo kama ni ya umma mkubwa.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Yachukue maoni ya umma na yakusanye pamoja, halafu nenda kwa umma, yashikilie maoni hayo na uyatekeleze, ili upate kuunda maoni sahihi ya uongozi — hii ndio njia ya msingi ya uongozi.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Katika kazi zote za vitendo za Chama chetu, uongozi ulio sahihi ni lazima "kutoka kwa umma, kurejea kwa umma". Hii ina maana kwamba: chukua fikra za umma (fikra zilizotawanyika na zisizo na mpango) na zikusanye (kwa kupitia mwenendo wa kufanya uchunguzi juu yake na kuzigeuza kuwa zilizokusanyika pamoja na zenye

mpango) halafu nenda kwa umma na uzitapakaze na kuzifahamisha fikra hizi mpaka umma wazikubali kama ni zao, wazikamate barabara na wazigeuze na kuzitumia katika vitendo, na pima usahihi wa fikra hizi katika vitendo hivyo. Tena kwa mara nyingine kusanya fikra kutoka kwa umma na kwa mara nyingine nenda kwa umma ili fikra zile zishikiliwe na kutekelezwa. Na kadhalika, tena na tena, kama damu inavyozunguka mwilini bila ya mwisho, na kwa namna hiyo fikra hizo zitazidi usahihi wake, zitazidi kuwa na uhai na zitazidi kukuzwa kwa kila mzunguko. Hii ndio nadharia ya Kimarx kuhusu ujuzi.

Kama juu.

Inatuwajibikia tuende kwa umma na tusome kutoka kwao, tuyakusanye maarifa yao kuwa kanuni na njia bora zenye mpango zaidi, baadaye tuueleze umma mambo haya kwa kupitia uenezi siasa miongoni mwao, na tuwatolee mwito wa

kuzitumia kanuni na njia hizi katika kutanzua matatizo yao na kuwasaidia kupata ukombozi na furaha.

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kuna watu katika idara za uongozi katika baadhi ya mwahala ambao wanafikiria kwamba inatosha kwa viongozi peke yao kujua siasa za Chama na kwamba hapana haja ya kuufanya umma wazijue. Hii ni mojawapo ya sababu za msingi kwa nini baadhi ya kazi zetu haziwezi kufanywa vyema.

"Mazungumzo na Wahariri wa *Gazeti la Kila Siku la Shansi-Suiyuan*" (Aprili 2, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika mavugu vugu yote ya umma ni lazima tufanye uchunguzi na uchambuzi wa msingi kuhusu idadi ya watu wanaounga mkono kwa dhati, wanaopinga au walioko kati kati na tusikate shauri juu ya matatizo

kwa kuzingatia fikra zetu tu na bila ya msingi.

"Njia za Kufanyia Kazi za Kamiti za Chama" (Machi 13, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Umma katika mwahala po pote pale kwa kawaida huwa umegawika sehemu tatu, wale ambao kwa kulinganishwa na wengine wana harakati, wale ambao wako kati kati na wale ambao kwa kulinganishwa wako nyuma. Kwa hivyo, ni lazima viongozi wawe na ustadi wa kuwaunga wale wachache wenye bidii kuwa uti wa mgongo wa uongozi na kuwategemea watu hawa katika kuinua daraja ya wale walio kati kati na kuwavuta wale walio nyuma.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kuwa hodari katika kuzigeuza siasa za Chama kuwa vitendo vya umma, kuwa

hodari katika kuwafanya si makada wanaoongoza peke yao bali vile vile umma mkubwa kufahamu na kuelewa vilivyo kila vugu vugu na kila jihadi tunayoianzisha — huu ndio ustadi wa uongozi unaotokana na Umarx-lenin. Vile vile huu ndio mstari wa mpambanuo kuonyesha tuko upande wa makosa au la katika kazi yetu.

"Mazungumzo na Wahariri wa *Gazeti la Kila Siku la Shansi-Suiyuan*" (Aprili 2, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kikundi cha uongozi hata kikiwa na bidii vipi, shughuli zake zitaishia kuwa ni jitihada za watu wachache zisizoleta maana isipokuwa shughuli hizo zichanganywe na shughuli za umma mkubwa. Kwa upande mwengine, ikiwa ni umma mkubwa tu ndio uliojishughulisha bila ya kuwa na kikundi madhubuti cha uongozi kinachozipanga vyema shughuli zao, shughuli hizo haziwezi kuendelezwa kwa muda mrefu, au kupelekwa

mbele katika njia inayofaa, au kunyanyuliwa kuendea daraja ya juu.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Nyenendo za uchumi zifanywazo na umma, maslaha ya umma, maarifa na hisia za umma, yote haya ni mambo ambayo makada wanaoongoza lazima wayaangalie daima.

Maandishi yaliyoandikwa kwa ajili ya maonyesho ya uchumi yaliyofanywa na jumuia zilioko chini ya Kamiti Kuu ya Chama na Makao Makuu ya Jeshi la Njia ya Nane, *Gazeti la Kila Siku la Ukombozi* la Yenan, Novemba 24, 1943.

Tuangalie sana suala la maisha ya umma, kutoka matatizo ya ardhi na kazi mpaka matatizo ya kuni, mchele, mafuta ya kupikia na chumvi. . . . Matatizo yote kama haya yanayohusu maisha ya umma lazima yatiwe

katika orodha ya mambo ya kuzingatiwa. Lazima tuyajadili matatizo haya, tukate shauri, tuyatekeleze mashauri yetu na tuyakague matokeo yake. Lazima tuufanye umma utambue kwamba tunawakilisha maslaha yao na kwamba maisha yetu yamefungamana na maisha yao. Lazima tuufanye umma — kutokana na mambo haya — ufahamu kazi kubwa zaidi tulizoziweka, yaani kazi za vita vya kimapinduzi, na kwa njia hii, umma utaunga mkono mapinduzi, na kuyaeneza mapinduzi nchini kote, umma utaitikia mwito wetu wa kisiasa na utapigania ushindi wa mapinduzi mpaka mwisho.

"Shughulikia Maisha ya Umma na Angalia Namna za Kufanya Kazi" (Januari 27, 1934), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

12. KAZI YA KISIASA

Mpango wa wajumbe wa Chama na idara za siasa, ulioanzishwa [mnamo wakati wa Vita vya Kwanza vya Kinchini vya Kimapinduzi, 1924-1927 — mtengenezaji] kwa mara ya kwanza katika historia ya China, umebadilisha kabisa sura ya majeshi haya. Jeshi Jekundu, lililoundwa tangu mwaka 1927, na Jeshi la Njia ya Nane la hivi sasa yameurithi mpango huu na kuukuza.

"Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kiingereza James Bertram" (Oktoba 25, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Jeshi la Ukombozi la Umma limekuza kazi yake imara ya kisiasa ya kimapinduzi juu ya msingi wa vita vya umma na wa kanuni za umoja baina ya jeshi na umma, umoja baina ya makamanda na wapiganaji

na kanuni ya kuvigawanyisha vikosi vya adui. Jambo hili ni muhimu kwa ajili ya kumshinda adui.

"Hali ya Mambo ya Sasa na Kazi Zetu" (Desemba 25, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Jeshi hili limeanzisha mpango wa kazi ya kisiasa ambao ni lazima kwa ajili ya vita vya umma, mpango ambao una shabaha ya kuleta umoja miongoni mwa wanajeshi wenyewe, umoja na majeshi ya kirafiki na umma na kuvigawanyisha vikosi vya adui na kuhakikisha ushindi katika vita.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kazi ya kisiasa ndio damu ya uhai wa kazi zote za uchumi. Jambo hili ni kweli hasa katika wakati ambapo mpango wa jamii-uchumi umo katika mabadiliko ya msingi.

Maelezo ya utangulizi katika "Funzo Kubwa" (1955).

"Matawi ya Chama yameanzishwa katika kila kampuni ya kijeshi"; hii ndio sababu muhimu ya kwa nini Jeshi Jekundu limeweza kuendeleza mapigano magumu bila ya kugawanyika.

"Mapigano Katika Milima ya Chingkang" (Novemba 25, 1928), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Kazi ya kisiasa ya Jeshi la Njia ya Nane inaongozwa na kanuni tatu za msingi. Kwanza, kanuni ya usawa baina ya maofisa na maaskari ambayo ina maana ya kuondosha tabia za kimwinyi katika jeshi, kukataza mambo ya kupiga na kutukana, kuijenga fahamu ya nidhamu, na kuwa pamoja katika furaha na dhiki — mambo ambayo yameleta jeshi zima kuungana. Pili, kanuni ya mafungamano baina ya jeshi na umma yenye maana ya kuweka nidhamu inayokataza kuyavunja hata kidogo maslaha ya umma, kufanya uenezi siasa miongoni mwa umma, kuwakusanya na kuwapa silaha, kuwapunguzia mizigo yao ya kiuchumi na kuwakandamiza mahaini na washiriki

wa adui wanaoleta madhara katika jeshi na umma — mambo ambayo yameleta jeshi kuungana vyema na umma na kukaribishwa po pote linapokwenda. Tatu, kanuni ya kuvigawanyisha vikosi vya adui na kuwaangalia kwa huruma mateka wa vita. Ushindi wetu hautegemei mapigano yafanywayo na jeshi letu tu bali vile vile unategemea kazi ya kuvigawanyisha vikosi vya adui.

"Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kiingereza James Bertram" (Oktoba 25, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Vikosi vyetu lazima vifuate kanuni sahihi zinazoongoza mahusiano baina ya jeshi na umma, baina ya jeshi na serikali, baina ya jeshi na Chama, baina ya maofisa na maaskari, na baina ya kazi ya kijeshi na kazi ya kisiasa, na mahusiano miongoni mwa makada, na daima visifanye makosa ya kibwana-vita. Maofisa lazima wawatendee wema maaskari wao na wasiwe hawayajali maisha yao au kuwapa adabu ya kupigwa viboko; jeshi lazima liwatendee wema

umma na daima lisiyadhuru maslaha yao; jeshi lazima liheshimu serikali na Chama na lising'ang'anie kudai "uhuru".

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Siasa yetu kuhusu mateka waliokamatwa kutoka vikosi vya Kijapani, vya kikaragosi au vinavyopinga Ukoministi ni kuwaachilia huru wote, isipokuwa wale ambao wamechukiza sana kwa umma na lazima wapate adabu ya kifo na ambao hukumu zao za kuuawa zimeshakubaliwa na wakuu. Inatupasa tuwavute kwa wingi kutumikia jeshi letu wale mateka ambao walilazimishwa kuingia katika majeshi ya wapinga maendeleo, lakini ingawaje wana kiwango fulani cha hisia za kimapinduzi. Waliobaki waachiliwe huru na, ikiwa watapigana nasi na kukamatwa tena, waachiliwe huru tena. Tusiwatukane, tusivichukue vitu vyao na tusijaribu kuwalazimisha watubie, bila ya mbaguo wo wote, tuwaangalie kwa dhati na wema. Hii iwe ndio siasa yetu, hata ikiwa

watu hao ni wapinga maendeleo vipi. Hii ndio njia yenye nguvu sana katika kuitenga kambi ya wapinga maendeleo.

"Juu ya Siasa" (Desemba 25, 1940), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Silaha ni kitu muhimu katika vita, lakini sicho kinachokata shauri; ni umma, na wala si vitu, ndio wanaokata shauri. Mashindano ya nguvu sio mashindano ya nguvu za kijeshi na uchumi tu, bali vile vile ni mashindano ya nguvu za binadamu na ushujaa. Nguvu za kijeshi na uchumi hazina budi kuendeshwa na umma.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Bomu la atomik ni chui wa karatasi ambaye anatumiwa na wapinga maendeleo wa Kimarekani katika kuwatisha watu. Kwa wajihi linatisha, lakini kwa kweli halitishi. Bila ya shaka, bomu la atomik ni silaha ya mauaji makubwa, lakini matokeo

ya vita yanaamuliwa na umma, na wala sio na aina moja au mbili mpya za silaha.

"Mazungumzo na Mwandishi Habari wa Kimarekani Anna Louise Strong" (Agosti 1946), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Askari ndio msingi wa jeshi; bila ya kuwa na hisia za kisiasa za kimaendeleo katika jeshi, na bila ya hisia hizo kukuzwa kwa kazi ya kisiasa ya maendeleo, itakuwa ni muhali kuupata umoja wa kweli baina ya maofisa na maaskari, muhali kuwafanya wawe na bidii kamili katika Vita vya Kupinga Ushambulizi, na itakuwa ni muhali kuweka msingi mzuri kabisa wa kutumia barabara zana za ufundi na mbinu zetu za kivita.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mawazo ya kufikiria mambo ya kijeshi tu yamewajaa sana baadhi ya makomredi

katika Jeshi Jekundu. Mawazo haya yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

1. Makomredi hawa wanaangalia mambo ya kijeshi na mambo ya kisiasa kama ni vitu vinavyopingana na wanakataa kutambua kwamba mambo ya kijeshi ni mojawapo tu ya njia za kuzitekeleza kazi za kisiasa. Baadhi yao hata wanasema "Ukiwa hodari katika mambo ya kijeshi, inafuata kwamba ni hodari katika mambo ya kisiasa; kama si hodari katika mambo ya kijeshi, huwezi kuwa na uhodari wo wote katika mambo ya kisiasa" — hii ni kwenda hatua moja zaidi katika kufikiri kwamba mambo ya kijeshi yanaongoza siasa.

. . . .

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Maelimisho ya kifikra ndio kiungo kikuu cha kukiunganisha Chama chote katika kufanya mapigano makubwa ya kisiasa. Bila ya kufanya jambo hili, Chama hakiwezi

kutimiza hata moja katika kazi zake za kisiasa.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Hivi karibuni kazi ya kifikra na kisiasa imeregea miongoni mwa wanafunzi vijana na wataalamu, na baadhi ya mambo mabaya yamechomoza. Baadhi ya watu wanaonyesha kwamba wanafikiri kuwa hapana tena haja ya kujishughulisha na siasa au mustakbala wa nchi yetu na matumainio ya juu kabisa ya binadamu. Inaonyesha kuwa Umarx zamani ulishitadi lakini sasa hauko tena machoni. Kwa ajili ya kuipinga mielekeo hii, ni lazima tutilie mkazo kazi ya kifikra na ya kisiasa. Wataalamu na wanafunzi vijana wote lazima wajifunze kwa bidii. Zaidi ya kujifunza masomo yao maalum, lazima wapate maendeleo katika upande wa fikra na pia upande wa siasa, jambo ambalo lina maana kwamba wajifunze Umarx, mambo yanayotokea hivi sasa na siasa. Kutokuwa na mtizamo sahihi

wa kisiasa ni kama kutokuwa na roho. . . . Idara na jumuia zote zichukue majukumu yao katika kazi ya kifikra na kisiasa. Jambo hili linahusu Chama cha Kikoministi, Umoja wa Vijana, idara za serikali zinazoshughulikia kazi hii, na hasa wakuu wa shule na waalimu.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Baada ya kupata elimu ya kisiasa, maaskari wa Jeshi Jekundu wamekuwa na ufahamu wa kitabaka na wamekuwa na ujuzi wa mambo kuhusu ugawaji ardhi, kuanzisha utawala wa kiserikali, kuwapa silaha wafanya kazi na wakulima, n.k., na wote wanajua kwamba wanapigana kwa faida yao wenyewe, kwa ajili ya tabaka la wafanya kazi na tabaka la wakulima. Na kwa hivyo, wao wanaweza kuvumilia shida za mapigano makali bila ya manung'uniko. Kila kampuni, betalini au rejimenti ina kamiti yake ya askari ambayo inawakilisha

maslaha ya askari na inafanya kazi ya kisiasa na ya kiumma.

"Mapigano Katika Milima ya Chingkang" (Novemba 25, 1928), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Uanzishaji sahihi wa vugu vugu la kuyatoa machungu yalioko moyoni (dhulma walizofanyiwa watu walioishi kwa jasho lao na jamii kongwe na wapinga maendeleo) na mikaguo mitatu (juu ya asili ya kitabaka ya mtu, ufanyaji kazi wake na ushujaa wake wa kupigana) umeinua sana ufahamu wa kisiasa wa makamanda na wapiganaji wa jeshi lote katika mapigano ya kuukomboa umma mkubwa wa wafanyao kazi walionyonywa damu, ya ugawaji ardhi nchini kote na ya kumwangamiza adui wa pamoja wa umma, kikundi cha kiharamia cha Chiang Kai-shek. Vile vile umetilia nguvu sana umoja imara wa makamanda na wapiganaji wote chini ya uongozi wa Chama cha Kikoministi. Kwa msingi huu, jeshi limekuwa safi zaidi, limetilia nguvu nidhamu, limeanzisha vugu vugu la umma kufanya

mazoezi ya kijeshi, na limekuza zaidi demokrasi yake katika mambo ya kisiasa, uchumi na ya kijeshi kwa njia ilioongozwa vizuri na kwa mpango kamili. Na kwa namna hii, jeshi limeungana kuwa kitu kimoja, kila mtu akitoa mchango wake wa mawazo na nguvu, jeshi lisiloogopa kujitolea mhanga na lenye uwezo wa kuzishinda taabu za ukosefu wa vitu na lenye ushujaa mkubwa wa kuthubutu kumbomoa adui. Jeshi kama hilo litakuwa halishindiki.

"Juu ya Ushindi Mkubwa Katika Kaskazini ya Magharibi na Juu ya Aina Mpya ya Vugu Vugu la Elimu ya Kisiasa Katika Jeshi la Ukombozi" (Machi 7, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika miezi michache iliopita takriban vikosi vyote vya Jeshi la Ukombozi la Umma vimetumia wakati wa baina ya mapigano kwa ajili ya mafundisho na maimarisho ya kijeshi ya kiwango kikubwa. Jambo hili limefanywa kwa njia ilioelekezwa vyema, yenye mpango na ya kidemokrasi. Kwa hivyo limechechemua hamu

ya kimapinduzi ya umma mkubwa wa makamanda na wapiganaji, limewawezesha kuelewa vyema madhumuni ya vita, limeondosha baadhi ya mielekeo isio sahihi ya kifikra na mambo yasiopendeza katika jeshi, limewaelimisha makada na wapiganaji na limezidisha sana uwezo wa kupigana wa jeshi. Kuanzia sasa, lazima tuendelee kufanya aina hii mpya ya vugu vugu la elimu ya kisiasa katika jeshi, vugu vugu ambalo lina umbo la kidemokrasi na la kiumma.

"Hotuba Kwenye Mkutano wa Makada Katika Eneo Lililokombolewa la Shansi-Suiyuan" (Aprili 1, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Siasa ya elimu ya Chuo Kikuu cha Kijeshi na Siasa Dhidi ya Japani ni kuukuza muelekeo madhubuti na barabara wa kisiasa, mtindo wa kufanya kazi kwa juhudi, kwa unyenyekevu na bila ya ubadhirifu pamoja na hila ya jumla na mbinu za kijeshi zinazojirekibisha kufuata

hali ya mambo. Haya ni mambo matatu ya lazima katika kumfanya mtu awe mwanajeshi wa kimapinduzi dhidi ya Japani. Ni kwa kutokana na mambo haya ya lazima ndio waalimu na makarani wanafanya matengenezo ya masomo na wanafunzi wanasoma.

Kupingwa na Adui Si Jambo Baya, Bali Ni Jambo Zuri (Mei 26, 1939).

Taifa letu siku zote limekuwa na tabia ya kiasili ya kupigana kwa jitihada bila ya kujali shida kubwa, tabia ambayo inataka tuikuze. . . . Zaidi ya hayo ni kuwa Chama cha Kikoministi siku zote kimekuwa kikihubiri muelekeo madhubuti na barabara wa kisiasa. . . . Muelekeo huu hauwezi kutengana na tabia ya kufanya kazi kwa jitihada na ushupavu. Bila ya muelekeo madhubuti na barabara wa kisiasa, ni muhali kuikuza tabia hii ya kufanya kazi. Bila ya kuwa na tabia ya kufanya kazi kwa jitihada na ushupavu, pia ni muhali kuendeleza

muelekeo madhubuti na barabara wa kisiasa.

"Hotuba Katika Maandamano ya Yenan kwa Kusherehekea Siku ya Wafanya Kazi wa Ulimwengu" (Mei 1, 1939).

Kuweni wamoja, kuweni macho, wenye juhudi na wachangamfu.

Usemi kwa Chuo Kikuu cha Kijeshi na Siasa Dhidi ya Japani.

Kitu chenye thamani hasa duniani ni mtu kuwa na bidii. Chama cha Kikoministi kinaangalia kabisa kuwa na bidii.

Mazungumzo katika mkutano na wanafunzi na wafanya kazi wa Kichina wanaoongeza maarifa katika Moscow (Novemba 17, 1957).

13. MAHUSIANO BAINA YA MAOFISA NA MAASKARI

Jeshi letu siku zote limekuwa na siasa mbili. Kwanza, lazima tusiwe na huruma kwa maadui zetu, lazima tuwazidi nguvu na tuwaangamize. Pili, lazima tuwe na huruma kwa watu wetu wenyewe, kwa umma, kwa makomredi wetu na kwa wakubwa wetu na walio chini yetu, na tuungane nao.

Hotuba katika tafrija iliofanywa na Kamiti Kuu ya Chama kwa ajili ya wajumbe wa kupigiwa mfano katika kusoma wa *Corps* za Jeshi la Nyuma (Septemba 18, 1944).

Sisi tunatoka pande mbali mbali za nchini na tumeungana pamoja kwa ajili ya lengo

la pamoja la mapinduzi. . . . Makada wetu lazima wamshughulikie kila askari, na watu wote miongoni mwa wana-mapinduzi lazima wafikiriane, watendeane wema na wasaidiane.

"Tumikia Umma" (Septemba 8, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Vugu vugu la kuwaunga mkono makada na kuwatendea wema maaskari linahitaji kuanzishwa katika kila kikosi cha jeshi, kwa kuwatolea mwito makada wawatendee wema maaskari na maaskari kuwaunga mkono makada. Kila mmoja amuonyeshe mwenzake upungufu na makosa yake na wayasahihishe kwa upesi. Kwa njia hii wataweza kuupata umoja wa ndani mzuri sana.

"Kazi za Mwaka 1945" (Desemba 15, 1944).

Watu wengi wanafikiria kwamba ni njia mbaya ambazo zinadhoofisha mahusiano baina ya maofisa na maaskari na baina ya

jeshi na umma, lakini siku zote mimi nawaambia kwamba hili ni suala la tabia ya msingi (au kanuni ya msingi) ya kuwaheshimu maaskari na umma. Ni kutokana na tabia hii ndio siasa, njia na maumbo mbali mbali yanatokea. Tukiiwacha tabia hii, basi siasa, njia na maumbo yatakuwa bila ya shaka ya makosa, na mahusiano baina ya maofisa na maaskari na baina ya jeshi na umma hayana budi kutotosheleza. Kanuni zetu kuu tatu kwa kazi ya siasa ya jeshini ni: kwanza, umoja baina ya maofisa na maaskari; pili, umoja baina ya jeshi na umma; na tatu, kuvigawanyisha vikosi vya adui. Kwa ajili ya kuzitekeleza vilivyo kanuni hizi, ni lazima tuwe na tabia hii ya msingi ya kuwaheshimu maaskari na umma, na kuwapa mateka wa vita heshima ya kibinaadamu mara baada ya kuweka chini silaha zao. Wale wanaoyachukulia yote haya kama ni mambo ya ustadi tu na si mambo yanayohusu tabia ya msingi hakika wanakosea, na inahitaji wasahihishe mawazo yao.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Wakoministi lazima watumie njia ya kidemokrasi ya kushawishi na kuelimisha wakati wanapofanya kazi miongoni mwa umma wa wafanyao kazi, na kwa hali yo yote wasiichukue njia ya kuamrisha na kulazimisha. Chama cha Kikoministi cha China kinafuata kwa udhati kanuni hii ya Kimarx-lenin.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Makomredi wetu lazima wafahamu kwamba ugeuzaji wa fikra ni kazi ya muda mrefu, ya subira na bidii, na wasijaribu kugeuza fikra za watu, ambazo zimejengwa kwa makumi ya miaka katika maisha yao, kwa kutoa hotuba chache au kwa kufanya mikutano michache. Kushawishi, sio kulazimisha, ndio njia pekee ya kuwavuta. Ulazimishaji maisha hautokuwa na matokeo ya kuwavuta. Kujaribu kuwavuta kwa nguvu haitofaa kitu. Njia ya namna hii inaruhusika katika mahusiano na adui, lakini hairuhusiki hata

kidogo katika mahusiano na makomredi na marafiki.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Lazima tuweke mpambanuo baina ya adui na sisi wenyewe, na tusiuchukue msimamo wa kiadui kwa makomredi na kuwatendea kama vile tunavyowatendea maadui. Katika kusema, mtu inahitaji awe na hamu kubwa ya kuihami jihadi ya umma na kuinua daraja yao ya ufahamu wa kisiasa na pasiweko tabia ya kuwakejeli au kuwashambulia.

Kama juu.

14. MAHUSIANO BAINA YA JESHI NA UMMA

Jeshi lazima liwe kitu kimoja na umma ili walione kama ni jeshi lao wenyewe. Jeshi kama hilo litakuwa halishindiki. . . .

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kila komredi lazima asaidiwe kufahamu kwamba madhali tunautegemea umma, tunaziamini kwa dhati busara za umma zenye uwezo usiokuwa na kikomo na kwa hivyo kuwaamini na kujifungamanisha nao, tutaweza kuikiuka taabu yo yote na hapana adui ye yote anayeweza kutushinda ilhali sisi tutaweza kumshinda adui ye yote.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Po pote wanapokwenda makomredi wetu, ni lazima wayajenge mahusiano mazuri na umma, wawashughulikie na wawasaidie kuziondosha taabu zao. Lazima tuungane na umma mkubwa; kila tukiungana nao zaidi ndio bora zaidi.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Jeshi katika Maeneo Yaliyokombolewa lazima liunge mkono serikali na liwatendee wema umma, na serikali za kidemokrasi lazima ziwaongoze umma katika kazi ya kuliunga mkono jeshi na kuzipendelea koo za askari wanaopigana na Japani. Kwa njia hii mahusiano baina ya jeshi na umma yatakuwa mazuri zaidi.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Katika jeshi, lazima tuwasaidie kila kamanda na mpiganaji waufahamu vyema

umuhimu wa kazi ya kuunga mkono serikali na kuwatendea wema umma kwa njia ya uelimishaji wa kifikra ili wote waufahamu vyema umuhimu wake. Madhali jeshi kwa upande wake linafanya kazi hii vyema, serikali ya kienyeji na umma nao hakika watafanya mahusiano yao na jeshi kuwa bora zaidi.

"Siasa ya Kazi ya Mwaka 1946 Katika Maeneo Yaliyokombolewa" (Desemba 15, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika mwenendo wa mavugu vugu haya,[1] jeshi kwa upande wake na Chama na serikali kwa upande wao lazima wakague kwa vilivyo upungufu na makosa ya mwaka 1943, na kwa dhati wayasahihishe katika mwaka 1944. Kuanzia sasa, inahitaji mavugu vugu haya yaanzishwe kila mwahala mnamo mwezi wa mwanzo wa kila mwaka

[1] Mavugu vugu ya "kuunga mkono serikali na kuwatendea wema umma" na "kuunga mkono jeshi na kuzipendelea koo za askari wanaopigana na Japani". — Maelezo ya mfasiri.

wa kienyeji na mnamo mavugu vugu hayo zisomwe mara kwa mara ahadi za "kuunga mkono serikali na kuwatendea wema umma" na "kuunga mkono jeshi na kuzipendelea koo za askari wanaopigana na Japani". Inahitaji kujitoa upungufu na makosa mbele ya umma tena na tena kuhusu jambo lo lote la uonevu kwa Chama, serikali au kwa umma, lililofanywa na vikosi katika maeneo ya vituo vyetu, au kuhusu uangalifu usio wa kutosha uliotendwa na Chama au serikali au umma kwa vikosi vya jeshi (kila upande ukijitoa makosa wenyewe tu wala sio kuutoa makosa upande mwengine) ili upungufu na makosa haya yasahihishwe barabara.

"Tapakaza Mavugu Vugu ya Kupunguza Kodi, Kuongeza Uchumi na 'Kuunga Mkono Serikali na Kuwatendea Wema Umma' Katika Maeneo ya Vituo Vyetu" (Oktoba 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

15. DEMOKRASI KATIKA MAMBO MATATU MUHIMU

Mpango wa demokrasi unataka uwekwe kwa kiasi katika jeshi, hususan kwa kuondoa tabia ya kimwinyi ya kuwaonea na kuwapiga askari na kwa kuwafanya maofisa na askari wa kawaida kuwa pamoja katika raha na shida. Mambo haya yakifanywa, umoja baina ya maofisa na askari utapatikana, nguvu za mapigano katika jeshi zitakuzwa sana, na hapatokuwa na shaka yo yote ya kuwa tutaweza kuendelea na vita hivi virefu na vikatili.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu II.

Mbali na kazi iliyofanywa na Chama, sababu kwa nini Jeshi Jekundu limeweza

kuendelea, ijapokuwa hali yao ya maisha ni mbaya na mapigano yanafanywa mara kwa mara, ni kuwa linatekeleza udemokrasi. Maofisa hawawapigi askari; maofisa na askari wanaangaliwa sawasawa; askari wana uhuru wa kufanya mikutano na kusema waliyo nayo; kawaida zisizokuwa na maana zimeondolewa; na kila mtu anaweza kuangalia jinsi pesa zinavyotumiliwa. . . . Katika China jeshi linahitaji udemokrasi kama wanavyohitaji umma. Udemokrasi katika jeshi letu ni silaha muhimu kwa kulibomoa jeshi la askari wa kukodiwa la kimwinyi.

"Mapigano Katika Milima ya Chingkang" (Novemba 25, 1928), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Kanuni ya kazi za kisiasa katika vikosi vya jeshi letu ni kuwatia hamasa maaskari, makamanda na watenda kazi wote katika jeshi kwa njia ya vugu vugu la kidemokrasi chini ya uongozi ili kuyapata malengo makuu matatu, yaani umoja wa kisiasa

wa daraja ya juu, hali bora zaidi za maisha, na ufundi na mbinu za kijeshi zilizo bora zaidi. Mikaguo Mitatu na Maendeleo Matatu[1] yanayofanywa kwa hima hivi sasa katika vikosi vyetu vya jeshi yamekusudiwa kuleta malengo mawili ya mwanzo kwa njia ya udemokrasi wa siasa na wa uchumi.

Kuhusu udemokrasi wa uchumi, wajumbe waliochaguliwa na askari lazima wahakikishiwe haki ya kusaidia (lakini sio kuupita) uongozi wa kampuni ya jeshi katika kusimamia vifaa na chakula cha kampuni.

---

[1] "Mikaguo Mitatu" na "Maendeleo Matatu" ilikuwa ni vugu vugu muhimu katika kuimarisha Chama na kwa elimu ya kifikra katika jeshi yaliyofanywa na Chama chetu yakifungamana na ugawaji wa ardhi mnamo wakati wa Vita vya Ukombozi vya Umma. Mitaani, "Mikaguo Mitatu", ilikuwa na maana ya kuchungua asili ya tabaka, fikra na namna ya kufanya kazi; katika vikosi vya jeshi, mikaguo ilikuwa juu ya asili ya tabaka, utekelezaji wa kazi na moyo wa kupigana. "Maendeleo Matatu" maana yake ni uimarishaji wa matengenezo, elimu ya kifikra na usahihishaji wa namna ya kufanya kazi.

Kuhusu udemokrasi wa kijeshi, katika nyakati za mazoezi ya kijeshi lazima yawepo mafundishano baina ya maofisa na askari na kati ya askari wenyewe; na katika nyakati za mapigano, kampuni zilizopo kwenye medani lazima zifanye mikutano mikubwa na midogo ya namna mbali mbali. Chini ya uongozi wa wakuu wa kampuni, askari watiwe hamasa kufanya majadiliano juu ya namna gani kufanya hujma na kuziteka ngome za adui na namna gani kutekeleza kazi nyinginezo za mapigano. Wakati mapigano yanapoendelea kwa siku kadha, mikutano kadha ya namna hiyo ifanywe. Aina hii ya udemokrasi wa kijeshi ilitekelezwa kwa mafanikio makubwa katika vita vya Panlung katika Shensi ya kaskazini na katika vita vya Shihchiachuang katika eneo la Shansi-Chahar-Hopei. Imethibitishwa kwamba kufanya hivyo huleta faida tu na hakuwezi kuleta dhara yo yote.

"Vugu Vugu la Kidemokrasi Katika Jeshi" (Januari 30, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika jihadi kubwa ya hivi sasa, Chama cha Kikoministi cha China kinataka idara zake zote za uongozi na wanachama na makada wake wote waonyeshe juhudi yao vilivyo, hivyo tu ndivyo inavyoweza kuhakikisha ushindi. Juhudi hii ionyeshwe kwa vitendo katika uwezo wa idara za uongozi, makada na wanachama kufanya kazi kwa busara, na vile vile katika moyo wao wa kuwa tayari kuchukua dhamana, hamasa yao katika kazi, ushujaa na uwezo wao wa kutoa masuala, kutoa maoni yao na kutoa makosa penye upungufu, na katika uangalizi wa kikomredi unaofanywa juu ya idara za uongozi na makada wanaoongoza. Kama si hivyo, "juhudi" itakuwa kitu kisichokuwa na maana. Lakini kuonyeshwa juhudi kama hiyo inategemea utapakaaji wa udemokrasi katika maisha ya Chama. Juhudi haiwezi kuonyeshwa vilivyo iwapo hapana demokrasi ya kutosha katika maisha ya Chama.

Ni katika hali ya kidemokrasi tu ndio idadi kubwa ya watu wenye uwezo inaweza kuletwa mbele.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mtu ye yote yule aruhusiwe kusema, bila ya kujali yeye ni nani, madhali si adui na hafanyi ushambulizi muovu, na si neno kama anasema jambo lisilo barabara. Viongozi wa daraja zote wanalo jukumu la kusikiliza watu wengine. Kanuni mbili lazima zifuatwe: (1) Sema kila unalolijua na bila ya kubania; (2) Usimlaumu msemaji bali chukulia maneno yake kama ni onyo. Kama kanuni ya "Usimlaumu msemaji" haikufuatwa kwa uthabiti wa moyo bali kwa udanganyifu, basi matokeo hayatokuwa "Sema kila unalolijua na bila ya kubania".

"Kazi za Mwaka 1945" (Desemba 15, 1944).

Elimu juu ya maisha ya kidemokrasi lazima ifanywe ndani ya Chama ili wanachama

waweze kufahamu nini maana yake, nini maana ya mahusiano baina ya demokrasi na uongozi, na njia ya kutekeleza mpango wa demokrasi-uongozi. Ni kwa njia hii tu ndio tutaweza kueneza kwa ukweli demokrasi ndani ya Chama na kwa wakati huo huo kuiepuka demokrasi iliyopita mpaka na kuwa kila mtu awe huru kufanya anavyotaka, mambo ambayo yanaharibu nidhamu.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika jeshi na pia katika matengenezo ya kienyeji, demokrasi ya ndani ya Chama inakusudiwa kuimarisha nidhamu na kuongeza nguvu za kupigana, na sio kuyadhoofisha mambo hayo.

Kama juu.

Katika upande wa nadharia, ing'oe mizizi ya demokrasi iliyopita mpaka. Kwanza,

ifahamishwe kwamba hatari ya demokrasi iliyopita mpaka ipo katika uwezekano wa kuharibu au hata kubomoa kabisa matengenezo ya Chama na kudhoofisha au hata kuvunja kabisa uwezo wa kupigana wa Chama, kukifanya Chama kisiweze kutekeleza kazi zake za mapigano na kwa hivyo kusababisha kushindwa kwa mapinduzi. Pili, ifahamishwe kwamba chanzo cha demokrasi iliyopindukia mpaka ni chuki za kibinafsi za tabaka la mabepari wadogo kuhusu nidhamu. Tabia kama hii inapoingizwa katika Chama, inaendelea kuwa fikra ya demokrasi iliyopita mpaka katika upande wa kisiasa na wa kimatengenezo. Fikra hizi hazipatani hata kidogo na kazi za mapigano za tabaka la kifanya kazi.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

16. UELIMISHAJI NA UFUNDISHAJI WA VIKOSI

Siasa yetu ya elimu lazima imuwezeshe kila mmoja anayepata elimu kuwa na tabia nzuri, akili timamu na afya njema na kuwa mfanya kazi mwenye ufahamu wa kisoshalisti na utamaduni.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Ama kuhusu elimu ya makada ikiwa wako kazini au katika skuli za makada, iwekwe siasa ya kusoma mambo hasa kuhusu matatizo ya mapinduzi ya China kuwa ni kiini na kutumia kanuni za msingi za Umarx-lenin kuwa ni uongozi, na iondolewe njia ya kusoma Umarx-lenin kama

yalivyoandikwa vitabuni tu na kutoambatana na hali ya maisha.

"Geuza Masomo Yetu" (Mei 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kwa skuli ya kijeshi, kitu muhimu kabisa ni kuchagua mkurugenzi na waalimu na kuweka siasa ya elimu.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Skuli ya watu mia bila ya shaka haitoendeshwa vizuri kama haina kikundi cha uongozi cha watu wachache, au zaidi ya kumi, ambacho kimeundwa kwa mujibu wa hali ya mambo hasa (na sio kukusanyika pamoja kijuu juu tu) na kuwa na waalimu, wafanya kazi na wanafunzi walio na juhudi, walionyoka na walio macho kuliko wote.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Maofisa na wapiganaji wote wa jeshi letu lazima waendeleze ustadi wao wa kijeshi, wasonge mbele kwa ushujaa katika vita vitakavyoleta ushindi wa hakika na wawafyeke maadui kwa uthabiti, moja kwa moja, wote na kwa ukamilifu.

"Tangazo Kuu la Jeshi la Ukombozi la Umma la China" (Oktoba 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Tutilie nguvu sawasawa katika upande wa kijeshi na wa kisiasa katika mpango wa mwaka mmoja ulioanza hivi sasa wa uimarishaji na ufundishaji. Na pande hizi mbili za kijeshi na kisiasa ziunganishwe. Mwanzo, mkazo uwe juu ya upande wa kisiasa, juu ya kuzidisha mahusiano baina ya maofisa na maaskari kuwa mazuri, kuimarisha umoja wa ndani na kuamsha juhudi ya daraja ya juu kati ya makada na umma wa wapiganaji. Hivyo tu ndio kazi za uimarishaji na ufundishaji wa kijeshi zitaendelea kwa urahisi na kupata matokeo mazuri zaidi.

"Kazi za Mwaka 1945" (Desemba 15, 1944).

Ama kuhusu njia ya mazoezi ya kijeshi, lazima tufanye vugu vugu la mazoezi ya kijeshi kwa kiwango cha umma. Katika vugu vugu hilo maofisa wawafundishe askari, askari wawafundishe maofisa na askari wafunzane wenyewe kwa wenyewe.

"Siasa ya Kazi ya Mwaka 1946 Katika Maeneo Yaliyokombolewa" (Desemba 15, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Mwito wetu katika mazoezi ya kijeshi uwe, "Maofisa wawafundishe askari, askari wawafundishe maofisa na askari wafunzane wenyewe kwa wenyewe". Wapiganaji wana maarifa mengi ya kupigana yanayotokana na mapigano hasa. Maofisa wajifunze kutoka kwa wapiganaji, na baada ya kuyafanya maarifa ya wengine kuwa ni yao wenyewe, watakuwa na uwezo mkubwa zaidi.

"Mazungumzo na Wahariri wa *Gazeti la Kila Siku la Shansi-Suiyuan*" (Aprili 2, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Ama kuhusu mafunzo ya kijeshi, lengo kuu bado liwe kuinua daraja ya ustadi wa kupiga shabaha, kuchoma singe, kurusha mabomu ya mkono na mambo kama hayo, lengo lifuatalo liwe kuinua daraja ya mbinu za kivita, lakini mkazo maalum utiliwe juu ya mazoezi ya mapigano ya usiku.

"Siasa ya Kazi ya Mwaka 1946 Katika Maeneo Yaliyokombolewa" (Desemba 15, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

17. KUTUMIKIA UMMA

Tuwe wanyenyekevu, wenye hadhari, tujiepushe na majivuno na papara, na tuutumikie umma wa China kwa moyo wote na nia safi.

"Mustakbala wa Aina Mbili wa China" (Aprili 23, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Shina la vitendo vyetu ni kutumikia umma kwa moyo wote na hata dakika moja tusiwachane na umma; katika kila jambo tuanzie kwa kufikiria maslaha ya umma na sio maslaha ya mtu binafsi au maslaha ya kikundi kidogo; na lazima tuulete umoja baina ya jukumu letu kwa umma na jukumu letu kwa maidara ya uongozi ya Chama.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Maidara ya dola lazima yatekeleze mpango wa demokrasi-uongozi, lazima yategemee umma wa watu, na watumishi wake lazima watumikie umma.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Moyo wa Komredi Bethune wa kujisabilia moja kwa moja kwa wengine, bila ya kujifikiria binafsi hata chembe, ulionekana kwa jinsi alivyokuwa akifanya kazi yake kwa madaraka makubwa kabisa na ukunjufu wake usio na kikomo kwa makomredi na umma. Kila Mkoministi lazima ajifunze kutoka kwake.

. . . .

Lazima sote tujifunze kutokana na moyo wake wa kutojifikiria binafsi hata kidogo. Kwa moyo huu, kila mmoja wetu anaweza kuwa mtu wa manufaa makubwa kwa umma. Uwezo wa mtu unaweza kuwa mkubwa au mdogo, lakini akiwa na moyo kama huu, mtu huyo keshakuwa mtu mwenye mawazo matukufu na msafi, mtu mwadilifu, mtu

asiyeshughulikia mambo ya upuuzi upuuzi na mtu mwenye thamani kwa umma.

"Kwa Ajili ya Ukumbusho wa Norman Bethune" (Desemba 21, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Chama chetu cha Kikoministi pamoja na majeshi yanayoongozwa na Chama chetu — Jeshi la Njia ya Nane na Jeshi Jipya la Nne ni vikosi vya mapinduzi. Vikosi vyetu hivi vimejisabilia moja kwa moja kwa ajili ya ugombozi wa umma na kutumikia kwa ukamilifu maslaha ya umma.

"Tumikia Umma" (Septemba 8, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Makada wetu wote, bila ya kujali vyeo vyao, ni watumishi wa umma, na kila tunalolifanya ni kwa ajili ya kutumikia umma. Basi vipi tusiwe radhi kuitupa tabia yetu yo yote mbaya?

"Kazi za Mwaka 1945" (Desemba 15, 1944).

Jukumu letu ni kuwa wenye dhamana kwa umma. Kila neno, kila kitendo na kila siasa lazima iambatane na maslaha ya umma, na kama makosa yanatokea, lazima yasahihishwe—hii ndio maana ya kuwa na dhamana kwa umma.

"Hali ya Mambo na Siasa Yetu Baada ya Ushindi Katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Agosti 13, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kila penye jihadi, kuna kujitolea mhanga; na kifo ni matokeo ya kidesturi. Lakini sisi tunafikiria maslaha ya umma na shida za wingi mkubwa wa umma nyoyoni mwetu, na tunapokufa kwa ajili ya umma ni kifo cha thamani. Hata hivyo, lazima tujitahidi, kama iwezekanavyo, kuepusha kujitolea mhanga kusiko lazima.

"Tumikia Umma" (Septemba 8, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Watu wote lazima kufa, lakini kifo kinaweza kubadilika katika umuhimu wake.

Mwandishi wa zamani wa Kichina, Szuma Chien alisema, "Ingawa kifo kinawaangukia watu wote sawasawa, lakini kinaweza kuwa kizito kuliko Mlima Tai au kuwa chepesi kuliko unyoya." Kufa kwa ajili ya maslaha ya umma ni jambo zito kuliko Mlima Tai, lakini kufanya kazi kwa ajili ya mafashisti na kufa kwa ajili ya wanyonyaji damu na wakandamizi ni kitu chepesi kuliko unyoya.

Kama juu.

18. HISIA ZA KIWANANCHI NA UDUGU WA KILIMWENGU

Jee anaweza Mkoministi, ambaye ana hisia za udugu wa kilimwengu, kwa wakati huo huo kuwa na hisia za kiwananchi? Tunazingatia kuwa sio kama anaweza tu bali lazima awe. Maana hasa ya hisia za kiwananchi inategemea hali ya mambo ya historia. Kuna "hisia za kiwananchi" za washambulizi wa Kijapani na za Hitler, na kuna hisia zetu za kiwananchi. Wakoministi lazima wazipinge kwa uthabiti "hisia za kiwananchi" za washambulizi wa Kijapani na za Hitler. Wakoministi wa Kijapani na wa Jarumani ni wenye fikra za kukubali kushindwa kuhusu vita vifanywavyo na nchi zao. Kuleta kushindwa vita vya washambulizi wa Kijapani na Hitler kwa kila njia

inayoyumkinika ni jambo la maslaha kwa watu wa Japani na Jarumani, na kila wakishindwa kwa ukamilifu zaidi basi ni bora zaidi. . . . Kwani vita vilivyoanzishwa na washambulizi wa Kijapani na Hitler vinawadhuru watu wa nchi zao kama vile vinavyowadhuru watu wa dunia. Lakini, hali ya China ni tofauti, kwa sababu China ndio inayoshambuliwa. Kwa hivyo, Wakoministi wa China lazima wachanganye hisia za kiwananchi na udugu wa kilimwengu. Sisi ni wenye hisia za udugu wa kilimwengu na za kiwananchi kwa wakati huo huo, na mwito wetu ni "Pigana kuihami nchi dhidi ya washambulizi." Kwetu sisi, fikra za kukubali kushindwa ni uhalifu na kupigania ushindi katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani ni wajibu wetu mkuu usioepukika. Kwani ni kwa kupigana kuihami nchi yetu tu ndio tunaweza kuwashinda washambulizi na kuupata ukombozi wa taifa letu. Na ni kwa kuupata ukombozi wa taifa tu ndio itayumkinika kwa tabaka la wafanya kazi na wengineo wanaotumia jasho lao kuweza kujigomboa nafsi

zao. Ushindi wa China na kushindwa kwa wabeberu wanaoishambulia China ni jambo litalowasaidia watu wa nchi nyenginezo. Kwa hivyo uwananchi ni udugu wa kilimwengu unaotekelezwa katika vita vya ukombozi wa kitaifa.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Jee huu ni moyo gani unaomfanya mtu wa nchi nyengine kutojifikiria binafsi na kuifanya jihadi ya ugombozi wa watu wa China kama ni jihadi yake mwenyewe? Ni moyo wa udugu wa kilimwengu, hisia ya kikoministi — jambo ambalo linamwajibikia kila Mwanachama wa Chama cha Kikoministi cha China ajifunze. . . . Ni lazima tuungane na tabaka la wafanya kazi wa nchi zote za kibepari, ni lazima tuungane na tabaka la wafanya kazi wa Japani, Uingereza, Marekani, Jarumani, Italy na wa nchi zote

nyenginezo za kibepari kabla ya kuweza kuupindua ubeberu, kuligomboa taifa letu na watu wetu, na kuyagomboa mataifa na watu wengineo wa dunia. Huu ndio udugu wetu wa kilimwengu, udugu wa kilimwengu tunaoutumia katika kupinga uwananchi mbovu wa mtu kupendelea taifa lake tu na nchi yake tu.

"Kwa Ajili ya Ukumbusho wa Norman Bethune" (Desemba 21, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika kupigania ukombozi kamili, watu wanaokandamizwa kwanza wategemee jihadi zao wenyewe, na baadaye ndio msaada wa kilimwengu. Watu ambao wamekwishafaulu katika mapinduzi yao wenyewe inawabidi wawasaidie wale ambao bado wanapigania ukombozi. Hili ni jukumu letu la udugu wa kilimwengu.

Mazungumzo na marafiki wa Afrika (Agosti 8, 1963).

Nchi za kisoshalisti ni madola ya aina mpya kabisa ambamo matabaka ya wanyonyaji damu yamepinduliwa na watu wanaoishi kwa jasho lao wamekamata hatamu za serikali. Kanuni ya kuunganisha hisia za udugu wa kilimwengu na hisia za kiwananchi inatekelezwa katika mahusiano kati ya nchi hizi. Tumeungana vyema kwa maslaha ya pamoja na matumainio ya juu ya pamoja.

"Hotuba Katika Mkutano wa Bunge Kuu la Umoja wa Soviet kwa Kusherehekea Kutimia Miaka Arobaini Tangu Mapinduzi Makubwa ya Kisoshalisti ya Oktoba" (Novemba 6, 1957).

Watu wa nchi zilizoko katika kambi ya kisoshalisti unganeni, watu wa nchi za Asia, Afrika na Latin Amerika unganeni, watu wa makontinenti yote ya dunia unganeni, nchi zote zipendazo amani ziungane, na nchi zote zinazoshambuliwa, kutawaliwa, kuingiliwa kati na kuonewa na Marekani ziungane, na kufanya muungano mkubwa kabisa

wa pamoja katika kupinga siasa za kishambulizi na za kivita za ubeberu wa Kimarekani na kuihami amani ya dunia.

> "Mazungumzo ya Kuunga Mkono Mapigano ya Haki ya Kiwananchi ya Watu wa Panama Dhidi ya Ubeberu wa Kimarekani" (Januari 12, 1964), *Watu wa Ulimwengu, Unganeni na Muwashinde Washambulizi wa Kimarekani na Vibaraka Vyao Vyote.*

Mambo yanaendelea bila ya kusita. Ni miaka arobaini na tano tu tangu kufanywa Mapinduzi ya 1911, lakini uso wa China umeshabadilika kabisa. Baada ya miaka arobaini na tano mingine, yaani, katika mwaka 2001, au mwanzo wa karne ya 21, China itakuwa imepata mabadiliko makubwa zaidi. Itakuwa imeshakuwa nchi yenye nguvu ya kisoshalisti ya makarahana. Na hivyo ni lazima iwe. China ina ardhi yenye eneo la kilomita za mraba 9,600,000 na umati wa watu 600 milioni, na inahitaji itoe mchango mkubwa zaidi kwa binaadamu. Mchango wake kwa muda mrefu

ulikuwa ni mdogo mno. Kwa jambo hili sisi tunasikitika.

Lakini lazima tuwe wanyenyekevu. Sio sasa tu, lakini hata baada ya miaka arobaini na tano vile vile. Siku zote tuwe wanyenyekevu. Katika mahusiano yetu ya kilimwengu, sisi watu wa China lazima kwa dhati, moja kwa moja, kabisa na kwa ukamilifu tuyafyeke mawazo ya uonevu [*chauvinism*] wa nchi kubwa.

"Kwa Ajili ya Ukumbusho wa Dr. Sun Yat-sen" (Novemba 1956).

Lazima tusichukue tabia ya majivuno ya uonevu wa nchi kubwa na kujiona kwa sababu ya ushindi wa mapinduzi yetu na mafanikio fulani katika ujenzi wetu. Kila taifa, kubwa au dogo, lina ubora wake na upungufu wake.

"Hotuba ya Ufunguzi Katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kitaifa wa Chama cha Kikoministi cha China" (Septemba 15, 1956).

19. USHUJAA WA KIMAPINDUZI

Jeshi hili lina moyo usioshindika na limeazimu kuwashinda maadui wote, na daima halitokubali kushindwa. Hata zikiwepo taabu na shida za namna gani, madhali amebaki mtu japo mmoja, ataendelea kupigana.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ukuze vilivyo mtindo wetu wa kupigana — ushujaa katika mapigano, kutoogopa kujitolea mhanga, kutoogopa machofu na mapigano ya mfululizo (yaani kufanya

mapigano kwa mfululizo katika muda mfupi bila ya kupumzika).

"Hali ya Mambo ya Sasa na Kazi Zetu" (Desemba 25, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Maelfu kwa maelfu ya majabari wamejitolea maisha yao kwa ushujaa kwa ajili ya maslaha ya umma; natunyanyue juu bendera yao na tusonge mbele kwenye njia iliyorowa damu yao!

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kuweni imara, msiogope kujitolea mhanga na zishindeni shida zote ili kupata ushindi.

"Mzee Mpumbavu Aliyeiondosha Milima" (Juni 11, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Katika wakati muhimu wa maendeleo ya Vita vya Msafara wa Kaskazini, . . . siasa za kihaini dhidi ya umma za "kusafisha chama" na uchinjaji zilizochukuliwa na wakuu wa Kuomintang zimeuharibu muungano huu wa pamoja wa taifa — muungano wa pamoja wa Kuomintang, Chama cha Kikoministi na watu wa madaraja yote, ambao uliwakilisha jihadi ya ukombozi wa watu wa China — na siasa zake zote za kimapinduzi. . . . Hapo tena vita vya ndani ya nchi vikachukua pahala pa umoja, udikteta ukachukua pahala pa demokrasi, na China ya giza ikachukua pahala pa China ya mng'aro. Lakini Chama cha Kikoministi cha China na watu wa China hawakutishika wala kushindwa wala kuangamizwa. Walijiinua, wakapangusa damu, wakawazika makomredi wao waliokufa na wakaingia tena vitani. Wakinyanyua juu bendera kuu ya mapinduzi, waliinuka kufanya upinzani wa kisilaha na katika sehemu kubwa ya China waliweka serikali za umma, kufanya ugawaji wa ardhi, na kujenga jeshi la umma — Jeshi Jekundu la China — na wakahifadhi na

kupanua nguvu za kimapinduzi za watu wa China.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mnazo sifa nzuri nyingi na mmetoa sehemu kubwa, lakini siku zote mkumbuke msije mkawa na majivuno. Mnaheshimiwa na wote, na jambo hilo ni sawa, lakini ni rahisi kuleta kiburi vile vile. Ikiwa mtajivuna, kama si wanyenyekevu na kutojitahidi, na ikiwa hamuwaheshimu watu wengine, hamuwaheshimu makada na umma, basi hamtakuwa tena mashujaa na watu wa kupigiwa mfano. Walikuwepo watu kama hao zamani, na ninatumai hamtofuata mfano wao.

"Lazima Tujifunze Kufanya Kazi ya Uchumi" (Januari 10, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Katika mapigano ya kumfyeka adui na kujitahidi kuhuisha na kuongeza uchumi wa kazi za makarahana na kilimo, mmezishinda taabu na shida nyingi na mmeonyesha

ushujaa, busara na juhudi kubwa. Nyie ni watu wa kupigiwa mfano kwa taifa lote la China, uti wa mgongo wa kupeleka mbele kwa ushindi jihadi ya watu katika pande zote, nguzo imara za kusimamisha Serikali ya Umma na daraja zinazoiunga Serikali ya Umma na umma mkubwa wa watu.

Salamu za pongezi kwa niaba ya Kamiti Kuu ya Chama cha Kikoministi cha China kwa Mkutano wa Wajumbe, wa Mashujaa wa Vita na Wafanya Kazi wa Kupigiwa Mfano Kutoka Taifa Zima (Septemba 25, 1950).

Sisi taifa la China tuna moyo wa kupigana na adui mpaka tone la mwisho la damu yetu, azma ya kurejesha mikononi mwetu kwa bidii zetu wenyewe ardhi yetu iliyopokonywa na sifa ya taifa letu, na uwezo wa kusimama wenyewe katika mataifa ya dunia.

"Juu ya Mbinu Dhidi ya Ubeberu wa Kijapani" (Desemba 27, 1935), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

20. KUJENGA NCHI YETU KWA BIDII NA BILA YA ISIRAFU

Lazima tuangalie kwamba makada wetu wote na watu wetu wote daima wanakumbuka kuwa nchi yetu ni nchi kubwa ya kisoshalisti, lakini ni nchi masikini iliyo nyuma katika uchumi, na kuwa hii ni hitilafu kubwa sana. Kwa ajili ya kuifanya China kuwa tajiri na yenye nguvu inahitaji makumi kadha ya miaka ya juhudi kubwa pamoja na juhudi za uangalifu mkubwa katika matumizi na kupigana na ubadhirifu, yaani siasa ya kujenga nchi kwa njia ya bidii na kutofanya isirafu.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Bidii na kutofanya isirafu lazima kutekelezwa katika kuendesha makarahana, maduka, makazi yote yanayomilikiwa na serikali, vyama vya ushirika, na makazi mengineo. Kanuni ya kufanya bidii na kuepusha isirafu inahitaji kufuatwa katika kila jambo. Kanuni hii ya uangalifu katika matumizi ni mojawapo ya kanuni za msingi za uchumi wa kisoshalisti. China ni nchi kubwa lakini hivi leo bado ni masikini sana. Itachukua makumi kadha ya miaka kuifanya China kuwa yenye neema. Hata hapo baadaye itatubidi tufuate kanuni ya kufanya bidii na kuepusha isirafu. Lakini ni katika makumi machache ya miaka ijayo, katika wakati wa kutekeleza mkururo tulio nao wa mipango ya miaka mitano, ndio itatubidi hasa kupiga makelele juu ya kufanya kazi kwa bidii na kuepusha isirafu, kwamba lazima tufanye uangalifu sana katika matumizi.

Maelezo ya utangulizi katika "Kuendesha Chama cha Ushirika kwa Bidii na kwa Kuondosha Isirafu" (1955).

Po pote tulipo ni lazima tuthamini sana nguvu zetu za kazi na vifaa tulivyo navyo na tusiwe tusiofikiria mbali na tukafanya upotevu na isirafu. Po pote tulipo, tangu mwaka wa kwanza wa kazi yetu lazima tufikirie miaka mingi ijayo, vita virefu ambavyo lazima viendelezwe, urejeshaji hujma, na kazi ya ujenzi baada ya kuwafurusha maadui. Kwa upande mmoja, milele tusiwe na upotevu na isirafu; kwa upande mwengine, lazima kwa bidii tuupanue uchumi. Zamani, katika baadhi ya mwahala, watu walipata taabu sana kwa sababu hawakufikiria mbali na walipuuza kufanya uangalifu juu ya nguvu za kazi na vifaa walivyo navyo na upanuaji wa uchumi. Funzo hili liko, na sasa watu lazima waamshwe kuliangalia.

"Lazima Tujifunze Kufanya Kazi ya Uchumi" (Januari 10, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ili kuharakisha uhuishaji na ukuaji wa uchumi wa kilimo na uchumi wa makarahana katika miji midogo, ni lazima, katika

mapigano yetu ya kuondosha mpango wa kimwinyi, tutumie kikomo cha uwezo wetu kuvihifadhi vifaa vyote vinavyotumika vya uchumi na maisha, tuchukue hatua kali kupinga ye yote anayeviharibu au kuvitupa, tupinge ulaji na unywaji wa isirafu na tuangalie kutofanya ubadhirifu na tuweke akiba.

"Hotuba Kwenye Mkutano wa Makada Katika Eneo Lililokombolewa la Shansi-Suiyan" (Aprili 1, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kutofanya ubadhirifu iwe ndio kanuni ya uongozi katika matumizi ya pesa ya serikali. Ni lazima iwekwe wazi kwa watumishi wote wa serikali kwamba upotofu na ufujaji ni uhalifu mkubwa sana. Mapigano yetu ya kupinga upotofu na ufujaji yameshapata mafanikio ya kiasi, lakini juhudi zaidi zinahitajika siku zijazo. Mpango wetu wa kuweka hesabu lazima uongozwe na kanuni ya kuweka akiba kila senti moja kwa ajili ya

juhudi za vita, kwa ajili ya jihadi ya kimapinduzi na ujenzi wetu wa uchumi.

"Siasa Yetu ya Uchumi" (Januari 23, 1934), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Mwelekeo wa hatari umejitokeza hivi karibuni miongoni mwa watumishi wetu wengi — kutotaka kuwa pamoja na umma katika furaha na shida, kushughulikia fahari na faida za kibinafsi. Hili ni jambo baya sana. Njia moja ya kuushinda mwelekeo huu wa hatari ni kurahisisha matengenezo ya maidara katika vugu vugu la kuukuza uchumi na kuweka akiba, na kuwapeleka makada katika daraja ya chini ili wingi mkubwa wao warejee katika kazi za uchumi.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Kazi za uchumi zinazofanywa na jeshi kwa ajili ya kujiendesha wenyewe si kama

zimefanya hali ya maisha ya wanajeshi kuwa bora na kupunguza mzigo uliowaelemea umma tu bali vile vile zimeleta uwezekano wa kulipanua jeshi. Zaidi ya hayo, zimeleta matokeo mengi ya pembezoni kwa haraka. Matokeo yenyewe ni kama yafuatayo:

(1) Mahusiano baina ya maofisa na maaskari yamekuwa mazuri zaidi. Maofisa na maaskari wanafanya kazi za uchumi kwa pamoja kama ndugu.

(2) Tabia kuhusu kazi za sulubu imekuwa nzuri zaidi. . . . Tangu jeshi lilipoanza kufanya kazi za uchumi kwa ajili ya kujiendesha wenyewe, tabia kuhusu kazi za sulubu imekuwa nzuri zaidi na mambo ya kivivu yameondoshwa.

(3) Nidhamu imetiliwa nguvu. Nidhamu katika kazi za uchumi si kama haikudhoofisha tu bali imetilia nguvu nidhamu katika vita na maisha ya kijeshi.

(4) Mahusiano baina ya jeshi na umma yamekuwa bora zaidi. Mara jeshi lilipoanza "kuangalia nyumba yake", mambo ya kuingilia mali za watu si

aghlabu kutokea au hayatokei kabisa. Ilivyokuwa jeshi na umma wanafanyiana kazi na kusaidiana katika kazi za uchumi, basi urafiki baina yao unatiliwa nguvu.

(5) Malalamiko katika jeshi kuhusu serikali yamepungua na maingiliano baina ya pande mbili hizo yamekuwa bora zaidi.

(6) Kampeni kubwa ya umma ya uchumi imezidi nguvu. Mara tu baada ya jeshi kuanza kujishughulisha na uchumi, haja ya maidara ya serikali na mengineyo kufanya hivyo inadhihirika zaidi, na yanafanya hivyo kwa nguvu zaidi; pia, haja ya kufanya kampeni kote kwa ajili ya umma wote kushiriki katika kuongeza uchumi bila ya shaka inadhihirika zaidi, na jambo hili vile vile linafanywa kwa nguvu zaidi.

"Juu ya Uchumi Unaofanywa na Jeshi kwa Kujiendesha Wenyewe na Juu ya Umuhimu wa Vugu Vugu Kubwa kwa Masahihisho na kwa Uchumi" (Aprili 27, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Baadhi ya watu wanasema kwamba ikiwa vikosi vya jeshi vitaingia katika kazi za uchumi, basi havitoweza kufanya mazoezi ya kijeshi au kupigana na kwamba ikiwa maidara ya serikali na mengineyo yatafanya hivyo, basi hayatoweza kufanya kazi zao wenyewe. Hizi ni hoja za uwongo. Katika miaka ya karibuni vikosi vyetu vya kijeshi katika Eneo la Mpakani vimefanya kazi za uchumi kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya kujipatia chakula na nguo za kutosha na kwa wakati huo huo vimefanya mazoezi yake ya kijeshi na vimefanya masomo yake ya kisiasa na mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na mengineo kwa mafanikio zaidi kuliko zamani, na kuna muungano mkubwa zaidi kuliko wakati wo wote ndani ya jeshi na baina ya jeshi na umma. Katika mwaka jana wakati ambapo palikuwepo kampeni ya kiwango kikubwa ya kazi za uchumi katika medani, mafanikio makubwa yalipatikana katika mapigano na zaidi ya hayo kampeni kubwa ya mazoezi ya kijeshi ilianzishwa. Na kwa sababu ya maidara ya serikali na mengineyo kujishughulisha na

uchumi, watumishi wao wanaishi katika hali bora zaidi na wanafanya kazi kwa bidii na uwezo zaidi; hivi ndivyo hali ilivyo katika Eneo la Mpakani na kwenye medani.

"Lazima Tujifunze Kufanya Kazi ya Uchumi" (Januari 10, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

21. KUJITEGEMEA WENYEWE NA KUFANYA JITIHADA KWA USHUPAVU

Siasa yetu iwekwe juu ya msingi gani? Inataka iwekwe juu ya msingi wa nguvu zetu wenyewe, na hiyo ina maana ya kujitegemea wenyewe. Hatuko peke yetu; nchi zote na watu wote wa dunia nzima wanaopinga ubeberu ni marafiki zetu. Hata hivyo, tunatilia mkazo kujitegemea wenyewe. Kwa kuzitegemea nguvu tunazozikusanya sisi wenyewe, tunaweza kuwashinda wapinga maendeleo wote wa Kichina na wa kigeni.

"Hali ya Mambo na Siasa Yetu Baada ya Ushindi Katika Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Agosti 13, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Sisi tunatetea kujitegemea wenyewe. Tunatumainia kupata msaada wa nchi za nje lakini hatuwezi kuutegemea msaada huo; tunategemea juhudi zetu wenyewe, nguvu za busara za jeshi lote na watu wote.

"Lazima Tujifunze Kufanya Kazi ya Uchumi" (Januari 10, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kupata ushindi wa nchi nzima ni hatua ya kwanza tu katika mwendo mrefu wa *li* elfu kumi. . . . Mapinduzi ya China ni makubwa, lakini njia ya baada ya mapinduzi itakuwa ndefu zaidi, kazi kubwa zaidi na ngumu zaidi. Jambo hili lazima sasa liwekwe wazi katika Chama. Makomredi lazima wasaidiwe kuendelea kuwa wanyenyekevu, wenye hadhari na kujiepusha na majivuno na papara katika mtindo wao wa kufanya kazi. Makomredi lazima

wasaidiwe kuendelea na mtindo wa kufanya jitihada kwa ushupavu.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Lazima tuyaondoshe kwa ukamilifu miongoni mwa makada wetu mawazo yote ya kupata ushindi kwa urahisi kwa kutegemea bahati nzuri, bila ya mapigano magumu na makali, bila ya kutoa jasho na damu.

"Jenga Maeneo ya Vituo Yalio Imara Katika Kaskazini ya Mashariki" (Desemba 28, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Inataka tufanye uenezi habari kwa mfululizo miongoni mwa umma juu ya ukweli wa maendeleo ya dunia na mustakbala mzuri ulio mbele ili wajenge imani ya ushindi. Kwa wakati huo huo, lazima tuwaambie umma na tuwaambie makomredi wetu kwamba patakuweko mazonge mengi kwenye njia yetu. Bado vipo vipingamizi

vingi na shida nyingi kwenye njia ya mapinduzi. Mkutano Mkuu wa Saba wa Chama chetu ulifikiria kwamba shida zitakuwa nyingi, kwani tunaona bora kufikiria shida nyingi zaidi kuliko kidogo. Baadhi ya makomredi hawapendelei kuzifikiria sana shida. Lakini shida ni mambo yaliopo; lazima tuzitambue shida nyingi kama zilizopo na tusifuate "siasa ya kutotambua". Lazima tuzitambue shida, tuzichambue na tupambane nazo. Hakuna njia zilizonyoka katika dunia; lazima tujitayarishe kufuata njia ambayo ina mizunguko na mipindo na tusijaribu kupata vitu kwa urahisi. Isiwazwe kwamba mnamo asubuni moja nzuri wapinga maendeleo wote watapiga magoti kwa hiari yao. Kwa ufupi, mustakbala ni mzuri, na njia ina mazonge mengi. Bado ziko shida nyingi mbele yetu, na tusizipuuze. Kwa kuungana na umma mzima katika juhudi ya pamoja, hakika tunaweza kuzishinda shida zote na kupata ushindi.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Mtu ye yote anayeona upande mzuri tu lakini haoni upande wa shida basi mtu huyo hawezi kupigana vyema katika kutimiliza kazi za Chama.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Utajiri wa jamii unaletwa na wafanya kazi, wakulima na wataalamu wafanyao kazi. Ikiwa watachukua maisha yao katika mikono yao wenyewe, wakafuata msimamo wa Kimarx-lenin na kuchukua bidii katika kuyatanzua matatizo badala ya kuyakwepa, hapatokuwa na shida yo yote katika dunia ambayo hawatoweza kuishinda.

Maelezo ya utangulizi katika "Katibu wa Chama Aongoze, na Wanachama Wote wa Chama Wasaidie Kuendesha Vyama vya Ushirika" (1955).

Makomredi katika Chama chote lazima wazizingatie vyema shida zote na kujiweka tayari kuzishinda kwa moyo usiovunjika na

kwa njia ya mpango. Nguvu za kipinga maendeleo zina shida zao na sisi tuna zetu. Lakini shida za nguvu za kipinga maendeleo haziwezi kushindwa kwa sababu hizo ni nguvu zinazokaribia kifo na hazina mwisho mwema. Shida zetu zinaweza kushindwa kwa sababu sisi ni nguvu mpya ambazo zinachomoza na zina mustakbala mzuri.

"Karibisheni Muinuko Mpya wa Mapinduzi ya China" (Februari 1, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Katika nyakati za shida, sisi makomredi tusisahau mafanikio yetu, lazima tuuone mustakbala mzuri ulio mbele yetu na tupige moyo konde.

"Tumikia Umma" (Septemba 8, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mambo mepya siku zote lazima yakutane na shida na vipingamizi wakati yanapokua. Ni ndoto tu kuwaza kwamba jihadi ya usoshaiisti itafanikiwa kwa urahisi katika

hali ya shwari, pasipo na shida na vipingamizi au bila ya kutumia jitihada kubwa.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Katika nyakati fulani za mapigano ya kimapinduzi, shida zinakuwa zimeizidi hali nzuri na kuwa ndio upande wa nguvu wa hitilafu, na hali nzuri kuwa ndio upande dhaifu. Lakini wana-mapinduzi kwa jitihada zao wanaweza kuzishinda shida hizo hatua baada ya hatua na kuleta hali mpya ya muwafaka; kwa hivyo hali ya shida inaondoka kuipisha ile ya muwafaka.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Nini kazi? Kazi ni mapigano. Po pote penye shida na matatizo, inatuwajibikia kwenda kuyatanzua. Tunakwenda kufanya kazi na kupigana ili tuzishinde shida hizo. Komredi mzuri ni yule mwenye

hamu kubwa ya kwenda pale penye shida kubwa zaidi.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Iko hekaya ya kale ya Kichina iitwayo "Mzee Mpumbavu Aliyeiondosha Milima". Hadithi hii yasimulia juu ya kizee aliyekuwa akiishi hapo kale katika kaskazini ya China ambaye alikuwa akiitwa Mzee Mpumbavu wa Milima ya Kaskazini. Nyumba yake ilikuwa ikikabili upande wa kusini, na karibu na mlango wake palikuweko milima miwili mirefu — Taihang na Wangwu — ambayo ilikuwa ikiziba njia. Mzee Mpumbavu kwa azma kubwa, aliwaongoza watoto wake wanaume kuichimba milima hiyo kwa kutumia jembe. Kizee mwengine — ajulikanaye kama Mzee Mwerevu — aliwaona wakiichimba milima hiyo na akasema kwa kejeli, "Upumbavu gani mlio nao kwa kufanya jambo hili! Ni muhali kabisa kwa nyinyi watu wachache kuweza kuichimba

milima hii miwili mikubwa." Mzee Mpumbavu akajibu, "Nitakapokufa, watoto wangu wataendelea; watakapokufa wao, wajukuu wangu wataendelea; watakapokufa wajukuu wangu, virembwe vyangu vitaendelea na kadhalika. Milima hii ingawa ni mirefu lakini haiwezi kuwa mirefu zaidi na kila kipande kidogo cha mlima tutakapokiondosha basi mlima utakuwa mfupi na mfupi zaidi. Kwa nini tusiweze kuiondosha milima hii?" Baada ya kuyakanusha mawazo ya makosa ya Mzee Mwerevu, Mzee Mpumbavu akaendelea kila siku kuichimba milima hiyo bila ya kutikisika imani yake. Mungu akavutwa na bidii hizi, na akawateremsha malaika wawili ambao waliichukua milima hiyo migongoni mwao. Hivi leo iko milima miwili mizito iliyowaelemea watu wa China. Mlima mmoja ni ubeberu na wa pili ni umwinyi. Chama cha Kikoministi cha China tokea zamani kimeazimia kuiondosha milima hii. Lazima tuvumilie na tuendelee kufanya kazi bila ya kusita ili, na sisi pia, tumfanye Mungu avutike. Mungu wetu si ye yote mwengineo isipokuwa ni umma mkubwa wa watu wa China. Ikiwa umma

utavinjari na kushirikiana nasi katika kuichimba milima hii, kwa nini tusiweze kuiondosha?

"Mzee Mpumbavu Aliyeiondosha Milima" (Juni 11, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

22. NJIA ZA KUFIKIRI NA NJIA ZA KUFANYA KAZI

Historia ya binaadamu ni ile ya maendeleo yasiosita kutoka milki ya lazima kuendea milki ya uhuru. Mwenendo huu hauna mwisho. Katika jamii yo yote ambamo matabaka bado yapo, mapigano ya kitabaka daima hayatokwisha. Katika jamii isio na matabaka, mapigano baina ya vipya na vikongwe na baina ya ukweli na uwongo daima hayatokuwa na mwisho. Katika mapigano ya kuendeleza uchumi na majaribio ya kisayansi, binaadamu anafanya maendeleo ya milele na maumbile yanapata mabadiliko yasiosita; daima hayabakii katika daraja hiyo kwa hiyo. Kwa hivyo, binaadamu inataka milele awe akikusanya maarifa na aendelee kugundua,

kuvumbua, kuunda na kusonga mbele. Fikra za kutoendelea, kutazamia misiba, kulegea legea na za kujiona na kujiridhisha zote ni za makosa. Ni makosa kwa sababu hazikubaliani na ukweli wa historia ya maendeleo ya jamii ya binaadamu ya kiasi cha miaka milioni iliopita na wala hazikubaliani na ukweli wa historia ya maumbile kama inavyojulikana nasi mpaka hivi sasa (yaani, maumbile kama yanavyofafanuliwa katika historia ya vitu vya mbinguni, dunia, maisha na ya sayansi nyinginezo za maumbile).

Maneno yaliyonukuliwa katika "Ripoti ya Waziri Mkuu Chou En-lai Juu ya Kazi ya Serikali Katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Tatu la Taifa la Umma la Jamhuri ya Watu wa China" (Desemba 21-22, 1964).

Sayansi ya kimaumbile ni mojawapo ya silaha za binaadamu za kupigania uhuru. Kwa madhumuni ya kuupata uhuru katika jamii, binaadamu lazima aitumie sayansi ya kijamii kuifahamu na kuigeuza jamii na

kutekeleza mapinduzi ya kijamii. Kwa madhumuni ya kupata uhuru katika ulimwengu wa maumbile, binaadamu lazima aitumie sayansi ya kimaumbile ili kuyafahamu, kuyashinda na kuyageuza maumbile na hivyo kuupata uhuru kutokana na maumbile.

Hotuba katika Mkutano wa Kuianzisha Jumuia ya Uchunguzi wa Sayansi ya Maumbile ya Eneo la Mpaka (Februari 5, 1940).

Falsafa ya Kimarx ya uyakinifu wa upembuzi ina tabia mbili zinazopiga sana machoni. Moja ni tabia yake ya kitabaka: inasema wazi kuwa elimu ya uyakinifu wa upembuzi ni kwa ajili ya kutumikia tabaka la kifanya kazi. Tabia yake nyengine ni kuambatana kwake na vitendo: inatilia mkazo utegemeaji wa mawazo juu ya vitendo, inatilia mkazo kwamba mawazo yanajengeka juu ya vitendo na kwa upande wake yanatumikia vitendo.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Falsafa ya Kimarx inafikiria kwamba tatizo muhimu kabisa haliko katika kuzifahamu kanuni za dunia kama ilivyo hasa na kwa hivyo kuweza kuifafanua, bali liko katika kuutumia ujuzi wa kanuni hizi kwa vitendo ili kuigeuza dunia.

Kama juu.

Mawazo barabara yanatoka wapi? Jee yanaangukia kutoka mbinguni? La. Jee, yamo akilini tangu mtu kuzaliwa? La. Mawazo barabara yanatokana na vitendo vya mtu katika jamii tu. Mawazo barabara yanatokana na aina tatu za vitendo katika jamii: mapigano ya kuendeleza uchumi, mapigano ya kitabaka na majaribio ya kisayansi.

Mawazo Barabara Yanatoka Wapi? (Mei 1963).

Ni hali ya mtu katika jamii ndio inayoamua fikra zake. Mara fikra barabara zinazowakilisha tabaka lililoendelea mbele zinapokamatwa na umma, basi fikra hizi

hugeuka kuwa nguvu hasa zinazoibadilisha jamii na kuibadilisha dunia.

Kama juu.

Katika vitendo vya kijamii, binaadamu wanafanya kila aina ya mapigano na wanajipatia maarifa mengi kutokana na mafanikio yao na pia kushindwa kwao. Mambo mengi ya ulimwengu unaotuzunguka yanaingia kwenye akili ya binaadamu kwa kupitia njia tano za fahamu: macho, masikio, pua, ulimi na mwili. Mwanzoni, ujuzi ni wa kuhisi. Baada ya kupatikana ujuzi wa kutosha wa kuhisi, panapatikana mchupo kuendea ujuzi wa kuwaza, na fikra zikapatikana. Huu ni mwenendo mmoja wa kulifahamu jambo. Hii ni daraja ya kwanza katika mwenendo mzima wa kulifahamu jambo, daraja ambayo inatokana na vitu hasa [*objective matter*] kuendea ufahamu wa mtu, yaani kutokana na kuwepo kwa vitu [*existence*] kuendea fikra. Katika daraja hii bado haiwezekani kuthibitisha kama ufahamu au fikra za mtu (pamoja na nadharia, siasa, mipango au

njia) zinamathilisha vyema kanuni za ulimwengu unaotuzunguka au la, kwani bado haiwezekani kuhakikisha kama ufahamu na fikra hizo ni barabara au la. Halafu inakuja daraja ya pili katika mwenendo wa kulifahamu jambo, yaani daraja inayoanzia ufahamu kurejea katika vitu, kutoka fikra kurejea kuwepo kwa vitu, ambamo ujuzi uliopatikana katika daraja ya kwanza unatumiwa katika vitendo vya mtu katika jamii ili kuhakikisha kama nadharia, siasa, mipango, njia na kadhalika za mtu zinapata mafanikio yaliyotumainiwa. Kwa jumla, zile fikra zilizofanikiwa ni sahihi, na zile zilizofeli si sahihi; jambo hili ni kweli hasa katika mapigano ya binaadamu na maumbile. Baadhi ya wakati, katika mapigano ya kijamii, nguvu zinazowakilisha tabaka lililoendelea mbele hushindwa si kwa sababu fikra zao si sahihi bali kwa sababu, katika mizani ya nguvu zinazopambana katika mapigano, wao kwa wakati ule hawana nguvu kama zile za wapinga maendeleo; kwa hivyo kwa muda wanashindwa; lakini hawana budi kushinda baadaye. Ujuzi wa binaadamu unafanya

mchupo mwengine kwa kupitia majaribio ya vitendo. Umuhimu wa mchupo huu ni mkubwa zaidi kuliko ule wa kabla. Kwani ni mchupo huu peke yake ndio unaoweza kuthibitisha usahihi au la wa mchupo wa kwanza, yaani fikra, nadharia, siasa, mipango, njia na kadhalika zilizotengenezwa katika mwenendo wa kumathilisha ulimwengu unaotuzunguka. Hapana njia yo yote nyengineo ya kuupima ukweli.

Kama juu.

Mara nyingi ujuzi barabara huweza tu kupatikana baada ya kurudia rudia kwa mara kadha mwenendo wa kutoka vitu kuendea ufahamu na kurejea tena kwenye vitu, yaani kutoka vitendo kuendea ujuzi na kurejea tena kwenye vitendo. Hiyo ndio nadharia ya Kimarx kuhusu ujuzi, nadharia ya uyakinifu wa upembuzi kuhusu ujuzi.

Kama juu.

Ye yote anayetaka kukijua kitu hana njia ya kufanya hivyo isipokuwa kufanya maingiliano na kitu hicho yaani kwa kuishi (kutenda) katika mastakimu yake. ... Kama unataka ujuzi, lazima ushiriki katika vitendo vya kuugeuza ukweli wa mambo. Kama unataka kujua ladha ya peya, lazima uligeuze peya kwa kulila wewe mwenyewe. ... Kama unataka kujua nadharia na njia za mapinduzi, lazima ushiriki katika mapinduzi. Ujuzi wo wote wa kweli unatokana moja kwa moja na maarifa ya mtu.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Ujuzi unaanzia kwenye vitendo, na ujuzi wa nadharia unaopatikana kwa njia ya vitendo lazima tena urejee kwenye vitendo. Kazi yenye hamasa ya ujuzi inajionyesha si katika mchupo wa vitendo kutoka ujuzi wa kuhisi kuendea ule wa kuwaza tu, bali — na muhimu zaidi — lazima ijionyeshe

katika mchupo kutoka ujuzi wa kuwaza kuendea vitendo vya kimapinduzi.

Kama juu.

Ni wazi kwamba unapofanya kitu cho chote, kama hujaifahamu hali yake hasa, tabia yake na mahusiano yake na vitu vyenginevyo, basi hutozijua kanuni zinazokiendesha kitu hicho, au kujua vipi kukifanya, au kuweza kukifanya vyema.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Ikiwa mtu anataka kufanikiwa katika kazi yake, yaani kuyapata matokeo yanaotizamiwa, lazima azifanye fikra zake ziambatane na kanuni za ulimwengu uliotuzunguka; kama haziambatani, atafeli katika vitendo vyake. Baada ya kufeli, anapata masomo, anazitengeneza fikra zake kuzifanya ziambatane na kanuni za ulimwengu uliotuzunguka, na kwa njia hii anaweza kugeuza kushindwa kuwa kufaulu; hii

ndio maana ya "kushindwa ni mzazi wa kufaulu" na "kutumbukia shimoni, huengezeka busara zaidi".

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Sisi ni wafuasi wa Umarx, na Umarx unatufunza kwamba katika kulikabili tatizo, lazima tuanzie kwenye ukweli wa mambo hasa na wala sio kutokana na tafsiri za maneno za kubuni kichwani tu na kwamba lazima tupate kanuni, siasa na njia kutokana na uchambuzi wa ukweli huu.

"Mazungumzo Katika Mkutano wa Yenan wa Mambo ya Uandishi na Sanaa" (Mei 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Njia ya msingi kabisa ya kazi ambayo Wakoministi wote lazima waitie akilini ni kuzipanga kanuni zetu za kazi kwa mujibu wa hali hasa ya mambo. Tunapochungua sababu za makosa tuliyoyafanya, tunagundua

kwamba yote yalitokea kwa sababu tulikwenda mbali na hali hasa ya mambo katika wakati maalum na mwahala maalum na tulikuwa tukichukulia fikra zetu tu za akilini katika kupanga kanuni zetu.

"Hotuba Kwenye Mkutano wa Makada Katika Eneo Lililokombolewa la Shansi-Suiyuan" (Aprili 1, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Udhanifu na *metaphysics* ndio vitu rahisi kabisa katika dunia, kwa sababu watu wanaweza kuropokwa upumbavu kama wanavyopenda bila ya kuwa na msingi wa ukweli wa mambo au kuufanya ujaribiwe na ukweli wa mambo. Uyakinifu na upembuzi, kwa upande mwengine, ni vitu vinavyotaka jitihada. Lazima viwe na msingi wa ukweli wa mambo na vijaribiwe nao. Kama mtu hajachukua jitihada, basi yumo katika hatari ya kutelezea kwenye udhanifu na *metaphysics*.

Maelezo ya utangulizi katika "Habari Kuhusu Kikundi cha Kipinga Mapinduzi cha Hu Feng" (Mei 1955).

Tunapokiangalia kitu, lazima tuchungue kiini chake na tuuchukulie wajihi wake kama ni bawabu kizingitini, na mara tu baada ya kukikiuka kizingiti, lazima tukikamate kiini cha kitu kile; hii ndio njia pekee ya kutegemewa na ya kisayansi katika kufanya uchambuzi.

"Cheche Moja Yaweza Kuanzisha Moto Mbugani" (Januari 5, 1930), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Sababu ya msingi ya ukuaji wa kitu haiko nje ya kitu kile bali ndani yake; imo katika hitilafu zilizomo katika kitu kile. Hitilafu hizi za ndani ziko katika kila kitu, ndio kila kitu kikawa kinakwenda na kukua. Hitilafu za ndani ya kitu ndio sababu ya msingi ya ukuaji wake, mahusiano yake na mivutano yake na vitu vingine ni sababu zifuatazo.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Uyakinifu wa upembuzi unazingatia kwamba sababu za nje ya kitu ndio hali

inayoleta mabadiliko na sababu za ndani ndio msingi wa mabadiliko, na sababu za ndani ndizo zinazoziwezesha sababu za nje kufanya kazi. Yai likipata joto la kutosha hugeuka kuwa kifaranga, lakini hapana joto linaloweza kulifanya jiwe kuwa kifaranga, kwa sababu kila moja lina msingi wake tofauti.

Kama juu.

Falsafa ya Kimarx inazingatia kwamba kanuni ya umoja wa vitu vinavyopingana ndio kanuni ya msingi ya ulimwengu. Kanuni hii iko katika kila kitu, ikiwa dunia ya maumbile, jamii ya kibinaadamu, au fikra ya mtu. Baina ya vitu vinavyopingana katika hitilafu huwepo umoja na mapigano kwa wakati huo huo, na ni jambo hili ambalo linasababisha vitu kusonga mbele na kugeuka. Hitilafu ziko kila pahala, lakini zinatofautika kwa mujibu wa tabia tofauti ya vitu tofauti. Katika kitu maalum cho chote, umoja wa vitu vinavyopingana ni wa hali ya wakati ule tu, wa muda na unaopita tu, na kwa hiyo huweza

kugeuka, wakati ambapo mapigano ya vitu vinavyopingana ni ya hakika kabisa.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Njia ya uchambuzi ni ile ya upembuzi. Kwa uchambuzi, tunakusudia kuchambua hitilafu za ndani ya vitu. Na uchambuzi ulio kamili hauyumkiniki kufanywa bila ya ujuzi wa ndani wa maisha na bila ya kufahamu kikweli hitilafu zinazohusika.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Uchambuzi hasa wa hali ya mambo hasa. Lenin alisema, ni "kitu cha msingi kabisa katika Umarx, ni roho inayoishi ya Umarx". Makomredi wetu wengi, wakiwa hawana mtazamo wa uchambuzi, hawataki kutafuta undani wa mambo yenye mazonge, kuyachambua na kuyasoma tena na

tena, lakini wanapenda kufikia uamuzi wa kijuu juu ambao ama wanakubali moja kwa moja au wanakataa moja kwa moja. ... Kutoka sasa lazima tuikomeshe hali hii ya mambo.

"Masomo Yetu na Hali ya Mambo" (Aprili 12, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Namna ya makomredi hawa ya kuyaangalia matatizo ni ya makosa. Hawaangalii pande za msingi au muhimu za matatizo bali wanatilia mkazo pande zile zisizo za msingi au muhimu. Lazima tufahamishe kwamba pande hizi zisizo za msingi au muhimu zisipuuzwe na lazima zikabiliwe moja baada ya moja. Lakini zisichukuliwe kama ni pande za msingi na muhimu, au tutapoteza mwelekeo wetu.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Katika dunia hii, mambo yana mazonge mazonge na huamuliwa na mambo mengi.

Tuyaangalie matatizo kutoka pande tofauti, sio kutoka upande mmoja tu.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Ni wale wanaoyatazama mambo kwa namna wanavyoyafikiria tu, kuyaangalia kwa upande mmoja na kijuu juu tu wakati wanapokabili matatizo ndio wanaotoa amri na maongozi kwa kujiamini mara tu baada ya kufika mwahala, bila ya kufikiria hali zenyewe, bila ya kuyaangalia mambo kwa jumla (historia yake na hali yake ya sasa kwa jumla) na bila ya kufikia kiini cha mambo (tabia yake na mahusiano ya ndani baina ya jambo moja na jingine). Watu kama hao hawana budi kujikwaa na kuanguka.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Katika kuyasoma matatizo, lazima tujiepushe na tabia ya kuangalia mambo kama

mtu anavyoyafikiria, kuyatazama mambo kwa upande mmoja na kwa kijuu juu tu. Kutazama mambo kama mtu anavyoyafikiria ni kutojua kuyatazama matatizo kama yalivyo hasa, yaani kutotumia mtazamo wa elimu ya uyakinifu katika kutazama matatizo. Nimezungumza juu ya hayo katika insha yangu "Juu ya Vitendo". Kutazama mambo kwa upande mmoja ina maana ya kutojua kuyatazama mambo kwa pande zote. ... Au inaweza kuitwa kuona sehemu bali sio yote, kuona miti bali sio msitu. Kwa namna hiyo ni muhali kupata njia ya kutanzua hitilafu, ni muhali kutekeleza kazi za mapinduzi, kutekeleza barabara kazi ulizopewa au kuyaendeleza vyema mapigano ya kifikra ya ndani ya Chama. Sun Wu Tzu aliposema katika kuzungumza juu ya sayansi ya kijeshi, "Mjue adui na jijue mwenyewe, na utaweza kupigana vita mara mia bila ya hatari ya kushindwa", alikuwa akigusia juu ya pande mbili za vita. Wei Cheng wa Utawala wa Nasaba ya Tang pia alifahamu kosa la kutazama jambo kwa upande mmoja aliposema, "Sikiliza pande zote mbili na utaerevuka, sikiliza upande

mmoja tu na utaingia kizani." Lakini makomredi wetu mara nyingi huyaangalia matatizo kwa upande mmoja tu, na kwa hivyo mara nyingi wanakutana na migogoro. ... Lenin alisema:

> ... ili kuweza kukijua kitu kikweli, lazima tuzikamate, tuzisome pande zote za kitu hicho, na mafungamano yake yote na "vikutanisho" vyake vyote. Daima hatutoweza kufaulu kwa ukamilifu katika jambo hili, lakini kutaka litazamwe jambo kwa pande zote kunatusaidia tujiepushe na makosa na kung'ang'anaa.

Lazima tuyakumbuke maneno yake. Kuyaangalia mambo kijuu juu ina maana ya kutozingatia tabia maalum za hitilafu kwa jumla yake wala tabia maalum za kila mmoja katika pande zake; ina maana ya kukanusha haja ya kukichungua kitu mpaka ndani na kusoma tabia maalum za hitilafu zake kwa makini sana, lakini badala yake kuangalia kutoka mbali tu na, baada ya kuona tu hali yake ya nje, hapo hapo kujaribu kutanzua hitilafu (kujibu suala,

kuamua mabishano, kuikabili kazi, au kuongoza mapigano ya kijeshi). Namna hii ya kufanya mambo haina budi kuleta matata. . . . Kuangalia jambo kwa upande mmoja na kijuu juu tu ni kwa wakati huo huo sawa na kuangalia jambo kama mtu anavyofikiri. Kwani vitu vyote vilivyopo kwa kweli vinaungana na vinaongozwa na kanuni za ndani, lakini, badala ya kuchukua kazi ya kuvionyesha vitu kama vilivyo, baadhi ya watu huangalia mambo kwa upande mmoja tu au kwa kijuu juu na wala hawajui mafungamano na kanuni za ndani za hivyo vitu, na kwa hivyo njia yao ni ya kuyatazama mambo kama wanavyoyafikiria.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu I.

·

Kutazama jambo kwa upande mmoja tu maana yake ni kufikiri kwamba kila kitu kimo katika hali isiyobadilika kabisa, yaani, kuyaangalia matatizo kwa mtazamo wa *metaphysics.* Katika kukadiria kazi yetu, ni mtazamo wa upande mmoja kuchukulia

kila kitu kama ama ni sawa kabisa au ni makosa kabisa. ... Kuchukulia kwamba kila kitu ni barabara ni kuona mazuri tu na kutoona mabaya, na ni kukubali sifa tu na kutokubali kutolewa makosa. Kuzungumza juu ya kazi yetu kama kwamba kila kitu ni kizuri kwa kila upande kunagongana na ukweli wa mambo. Si kweli kwamba kila kitu ni kizuri; bado upo upungufu na makosa. Lakini vile vile si kweli kwamba kila kitu ni kibaya, na jambo hilo pia, linagongana na ukweli wa mambo. Hapa uchambuzi unahitajika. Kukanusha kila kitu ni kufikiri, bila ya kufanya uchambuzi wo wote, kwamba hapana kitu cho chote kilichofanywa vyema na kwamba kazi kubwa ya ujenzi wa kisoshalisti, mapigano makubwa ambayo wanashiriki mamia ya mamilioni ya watu, ni mchafuko mtupu bila ya jambo lo lote linalostahiki kusifiwa. Ijapokuwa ipo tofauti baina ya watu wengi wenye mawazo kama hayo na wale ambao wanautazama mpango wa kisoshalisti kwa uadui, mawazo kama haya ni makosa makubwa na yanaleta

madhara na hayawezi kuleta cho chote isipokuwa kuwavunja moyo watu. Ni makosa kuikadiria kazi yetu ama kwa mtazamo kwamba kila kitu ni barabara au kwa mtazamo kwamba kila kitu si barabara.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Katika kukabili matatizo mfuasi wa Umarx lazima aone si kama sehemu ya jambo tu, bali vile vile jambo zima. Chura ndani ya kisima husema, "Ukubwa wa mbingu ni sawa sawa na mdomo wa kisima." Hiyo si kweli, kwani ukubwa wa mbingu si sawa sawa na mdomo wa kisima. Kama angesema, "Sehemu ya mbingu ni sawa sawa na mdomo wa kisima", hiyo ingelikuwa kweli, kwani inakubaliana na ukweli wa mambo.

"Juu ya Mbinu Dhidi ya Ubeberu wa Kijapani" (Desemba 27, 1935), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Lazima tujifunze kuangalia matatizo kwa pande zake zote, kuona upande wa mbele na pia upande wa nyuma wa kitu. Katika hali fulani, jambo baya linaweza kuleta matokeo mazuri na jambo zuri kuleta matokeo mabaya.

Juu ya Katanzua Kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Wakati tunapotambua kwamba katika maendeleo ya jumla ya historia hali ya vitu ndio inayokata shauri juu ya akili na hali ya jamii ndio inayoamua juu ya ufahamu wa jamii; vile vile — na bila ya shaka ni lazima — tutambue athari ya akili ya mtu juu ya vitu, athari ya ufahamu wa jamii juu ya hali ya jamii na ya muundo wa juu [*super-structure*] juu ya msingi wa uchumi. Hii haiendi kinyume na uyakinifu; kinyume unaepusha uyakinifu wa kimashine na kushikilia imara uyakinifu wa upembuzi.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Katika kutafuta ushindi, wale wanaoongoza vita hawawezi kukipindukia kikomo kilichowekwa na hali ya mambo ilivyo hasa; juu ya hivyo, wanaweza na lazima wachukue jukumu kubwa katika kupigania ushindi ndani ya kikomo hicho. Jukwaa la vitendo la makamanda katika vita lazima lijengwe juu ya uwezekano unaotokana na hali ya mambo, lakini juu ya jukwaa hilo wanaweza kuongoza michezo mingi, yenye sauti na nuru, yenye nguvu na fahari.

"Juu ya Vita Virefu" (Mei 1938),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu II.

Watu lazima wazifanye fikra zao ziambatane na mabadiliko ya hali. Bila ya shaka mtu ye yote asifanye ndoto za kiwazimu, au kufanya mipango yake ya vitendo isiyoruhusiwa na hali ya mambo, au kuyakamia yale yasiyoyumkinika. Lakini, matatizo yaliyopo leo ni kwamba fikra za Upande wa Kulia zisizokubali kugeuka bado zinaleta matata katika pande nyingi na kuzuia kazi katika pande hizi kufuatana

na ukuaji wa hali ya mambo hasa. Matatizo yaliyopo hivi sasa ni kwamba watu wengi wanadhania kuwa ni muhali kuyatimiza mambo ambayo kama wangefanya bidii wangeweza kuyatimiza.

Utangulizi katika *Muinuko wa Kisoshalisti Katika Mashamba ya China* (Desemba 27, 1955).

Siku zote lazima tutumie akili zetu na tufikirie kila kitu kwa makini. Msemo maarufu unasema, "Kunja uso na utagundua rai ya kufanya." Kwa maneno mengine, kufikiri sana kunaleta busara. Ili kujiondoshea upofu ambao upo kwa kiwango kikubwa katika Chama chetu, lazima tuwahimize makomredi wetu kufikiri, kujifunza njia ya uchambuzi na kukuza tabia ya kufanya uchambuzi.

"Masomo Yetu na Hali ya Mambo" (Aprili 12, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ikiwa katika mwenendo wo wote zimo hitilafu nyingi, moja katika hizo lazima iwe hitilafu kuu inayochukua mahala pa uongozi na uamuzi, na zilizobakia zinachukua mahala pa pili na kuwa chini yake. Kwa hivyo, katika kusoma mwenendo wo wote wenye mazonge ambao una hitilafu mbili au zaidi, lazima tufanye kila bidii kutafuta hitilafu yake kuu. Mara tu baada ya kuikamata hitilafu kuu, matatizo yote yanaweza kutanzuliwa upesi upesi.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937),
Maandishi Yaliyoteuliwa, Juzuu I.

Katika pande mbili zinazohitilafiana, moja lazima iwe kuu na nyingine inayofuata. Upande mkuu ndio wenye mahala pa uongozi katika hitilafu. Tabia ya kitu inategemea hasa juu ya ule upande mkuu wa hitilafu, ambao unachukua mahala pa uongozi.

Lakini hali hii haibaki papo hapo; ule upande mkuu wa hitilafu na ule upande

mwengine hubadilishana mwahala na tabia ya kitu hubadilika kwa namna hiyo hiyo.

Kama juu.

Haitoshi kuweka kazi tu, lazima vile vile tutanzue tatizo la njia ya kuzitekeleza. Ikiwa kazi yetu ni kuuvuka mto, hatuwezi kuuvuka bila ya daraja au mashua. Mpaka tatizo la daraja au mashua litakapokwisha tanzuliwa, haina maana ya kuzungumza juu ya kuuvuka mto. Mpaka itakapotanzuliwa tatizo la njia, kuzungumza juu ya kazi ni bure.

"Shughulikia Maisha ya Umma na Angalia Namna za Kufanya Kazi" (Januari 27, 1934), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Katika kazi yo yote, kama haujatolewa mwito wa jumla na kutapakazwa, umma mkubwa hauwezi kukusanywa pamoja ili kuchukua hatua. Lakini ikiwa watu waongozao wanajifunga katika kutoa mwito wa

jumla tu — kama wao wenyewe hawajiingizi ndani na vilivyo katika kazi inayotakiwa katika baadhi ya idara, kufungua njia pahala pamoja, kupata maarifa na kuyatumia maarifa hayo katika kuongoza idara nyingine — basi hawatakuwa na njia ya kujaribu usahihi wa mwito wao wa jumla au kuongeza maana ya mwito huo, na kuna hatari ya kwamba hakitopatikana kitu cho chote.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Hapana kiongozi ye yote mwenye uwezo wa kutoa uongozi wa jumla kwa shirika zote isipokuwa akipata maarifa hasa ya watu na matukio maalum ya shirika maalum za chini. Njia hii iendelezwe kila pahala ili makada wanaoongoza wa daraja zote wajifunze kuitumia.

Kama juu.

Katika mahala fulani po pote, hapawezi kuwa na kazi kuu kadha kwa wakati mmoja. Katika wakati maalum kunaweza kuwa

na kazi kuu moja tu ikijalizwa na kazi nyenginezo za daraja ya pili au ya tatu kwa umuhimu. Kwa hivyo, mtu mwenye dhamana ya jumla ya pahala afikirie historia na hali ya mapigano katika pahala hapo na aziweke kazi mbali mbali katika mwahala mwao mnamotakiwa; asiitekeleze kila amri kama vile inavyokuja kutoka juu bila ya kufanya mipango yake mwenyewe, na kwa namna hiyo kuleta mkururo wa "kazi kuu" na kusababisha hali ya mbabaiko na mchafuko. Na shirika yo yote ya juu isitoe kwa wakati mmoja kazi nyingi kuzipa shirika za chini bila ya kuonyesha umuhimu na haraka ya kila moja au bila ya kusema wazi ipi ni ya mwanzo, kwani hiyo italeta mbabaiko katika hatua zinazotaka kuchukuliwa na shirika za chini katika kazi zao na kwa hivyo hapana matokeo mahsusi yatakayopatikana. Ni sehemu ya ustadi wa uongozi kuifikiria hali yote kwa jumla na kufanya mipango kwa mujibu wa hali ya mambo ya kihistoria na hali iliyopo katika kila mahala, kufanya uamuzi barabara juu ya kiini cha kazi na utaratibu wa kazi katika

kila kipindi, kutekeleza uamuzi kwa uthabiti, na kuhakikisha kuwa matokeo mahsusi yatapatikana.

Kama juu.

Ni lazima kuelewa kwa wakati wote maendeleo ya kazi, kubadilishana maarifa na kusahihisha makosa; isingoje mpaka miezi kadha, nusu mwaka au hata mwaka kupita kabla ya kuitisha mikutano ya kukusanya maarifa, kukagua na kusahihisha makosa kwa jumla. Kungojea huleta hasara kubwa, lakini kusahihisha makosa yanapotokea tu kunapunguza hasara.

"Juu ya Siasa ya Makarahana na Biashara" (Februari 27, 1948), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Usingoje mpaka matatizo yamejirundika na kusababisha matata chungu nzima kabla ya kujaribu kuyatanzua. Viongozi lazima waende mbele ya vugu vugu, wasibaki nyuma yake.

Maelezo ya utangulizi katika "Masikilizano ya Kazi kwa Majira" (1955).

Tunachohitaji ni akili ya jitihada lakini iliyotulia na kazi ya bidii lakini yenye mpango.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

23. UCHUNGUZI NA MASOMO

Kila mtu anayeshughulika na kazi hasa lazima achungue hali ya mambo katika daraja za chini. Uchunguzi kama huo unahitajika kufanywa hasa na wale ambao wanajua nadharia tu lakini hawajui hali ya mambo hasa, kwani kama si hivyo hawatoweza kuunganisha nadharia na vitendo. Ingawa msemo wangu, "Bila ya uchunguzi, huna haki ya kusema", umekejeliwa kama ni "fikra ndogo za kufuata maarifa tu", lakini mpaka hii leo sijuti kuwa nimesema hivyo; mbali na kujuta, bado ninasisitiza kwamba bila ya uchunguzi ni muhali kuwepo haki yo yote ya kusema. Kuna watu wengi ambao "mara tu baada ya kuteremka katika gari lao rasmi" wanafanya kelele, wanarusha maoni yao, wanatoa makosa hili na kuponda

lile; lakini, kwa hakika, kumi katika kumi ya wao watafeli. Kwani maoni kama hayo au utoaji makosa kama huo, ambao hauna msingi wa uchunguzi kamili, si lo lote isipokuwa porojo la kijinga. Kwa mara zisizo na hesabu Chama chetu kimepata taabu katika mikono ya "wajumbe wa mfalme" kama hao, ambao huzunguka huku, kule na kila pahala. Stalin alisema barabara kwamba "nadharia huwa haina madhumuni ikiwa haikuunganishwa na vitendo vya kimapinduzi". Na aliongeza barabara kwamba "vitendo hupapasa papasa katika giza kama njia yake haikumurikwa kwa nadharia ya kimapinduzi". Mtu ye yote asipewe jina la "mwenye fikra ndogo za kutegemea maarifa tu" isipokuwa yule "mtu wa vitendo" anayepapasa papasa katika giza na hana mustakbala wala haoni mbali.

"Dibaji na Maelezo Zaidi Juu ya *Uchunguzi wa Mashambani*" (Machi na Aprili 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kuwa na tabia kama hiyo ni kuutafuta ukweli kutokana na mambo thabiti. "Mambo

thabiti" ni vitu vyote ambavyo viko hasa, "ukweli" maana yake ni uhusiano wao wa ndani, yaani, kanuni zinazoviongoza, na "kutafuta" maana yake kusoma. Inatupasa tuanzie kutoka hali hasa ya mambo ya ndani na nje ya nchi, jimbo, wilaya au mudiria, na kutokana nayo tupate kanuni za kuongoza vitendo vyetu, kanuni ambazo zimo ndani ya hali yenyewe wala sio za kuotea tu, yaani, lazima tugundue mahusiano ya ndani ya mambo yanayotokea tulipo. Na ili kufanya hivyo ni lazima tutegemee sio ndoto za mtu, hima ya muda tu, sio vitabu visivyo na uhai, bali mambo thabiti yaliopo hasa; lazima tuyaangalie mambo kwa urefu na, tukiongozwa na kanuni za msingi za Umarx-lenin, tutoe uamuzi sahihi kutokana nayo.

"Geuza Masomo Yetu" (Mei 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kujifanya kama "mtu anayekamata zuwarde huku amefungwa macho", au "kipofu anayepapasia samaki", kufanya mambo ovyo ovyo, kujishughulisha na kusema tu,

kutoshelezeka na ujuzi wa kuokotea okotea — huo ndio mtindo mbaya sana wa kufanya kazi ambao bado ungalipo miongoni mwa makomredi wengi katika Chama chetu, mtindo ambao ni kinyume kabisa na moyo wa msingi wa Umarx-lenin. Marx, Engels, Lenin na Stalin wametusomesha kwamba ni lazima kusoma hali ya mambo kwa makini na kuanzia kutoka ukweli halisi wa mambo na sio kutoka matamanio ya mtu; lakini makomredi wetu wengi wanakwenda kinyume kabisa na ukweli huo.

Kama juu.

Huwezi kutanzua tatizo? Basi, nenda ukafanye uchunguzi wa mambo yake ya hivi sasa na historia yake! Utakapokwisha kufanya uchunguzi kamili wa hilo tatizo, utajua namna ya kulitanzua. Uamuzi siku zote unakuja baada ya uchunguzi na sio kabla. Ni mpumbavu tu ambaye husumbua akili yake peke yake au pamoja na kikundi cha watu, "kutafuta tanzuo" au "kuvumbua fikra" bila ya kufanya uchunguzi wo wote. Lazima kutiliwa mkazo kwamba jambo

kama hili haliwezi asilani kuleta tanzuo lo lote linalofaa au fikra yo yote nzuri.

Pinga Kuabudu Vitabu (Mei 1930).

Uchunguzi unaweza kufananishwa na miezi mingi ya uja uzito, na kutanzua tatizo huwa kama siku ya uzazi. Kulichungua tatizo, hakika, ni kulitanzua.

Kama juu.

Inafaa tutumie nadharia na njia ya Umarx-lenin katika kufanya uchunguzi na masomo kwa mpango na ukamilifu kuhusu hali ya pahala tulipo. Tusifanye kazi kwa hamu tu peke yake, bali kama Stalin alivyosema, kwa kuchanganya hamasa ya kimapinduzi na moyo wa utendaji mambo hasa.

"Geuza Masomo Yetu" (Mei 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Njia pekee ya kujua hali ya mambo ni kufanya uchunguzi wa jamii, kufanya

uchunguzi wa hali ya kila tabaka la jamii katika maisha hasa. Kwa wale waliopewa dhamana ya kuongoza kazi, njia ya msingi ya kujua hali ya mambo ni kushughulikia miji michache na vijiji vichache kwa mujibu wa mpango na, kwa kutumia mtizamo wa msingi wa Umarx, yaani, njia ya uchambuzi wa matabaka, kufanya uchunguzi uliokamilika kwa mara kadha.

"Dibaji na Maelezo Zaidi Juu ya *Uchunguzi wa Mashambani*" (Machi na Aprili 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mkutano wa kutafuta ukweli si lazima uwe mkubwa; kutoka watu watatu mpaka watano au saba au wanane wanatosha. Uwepo wakati wa kutosha na mpango wa uchunguzi utayarishwe; zaidi ya hayo, mtu afanyaye uchunguzi yeye mwenyewe aulize masuala, aandike yanayozungumzwa na afanye majadiliano na waliohudhuria mkutano. Kwa hivyo, bila ya shaka, mtu hawezi kufanya uchunguzi, au kuufanya vyema, bila ya kuwa na juhudi, azma ya kuinamisha

macho yake na kiu ya kutaka ujuzi, na bila ya kuvua vazi baya la kujiona na kuwa mwanafunzi msikivu.

Kama juu.

Mipango sahihi ya kamanda inatokana na maazimio yake sahihi na maazimio yake sahihi yanatokana na uamuzi wake sahihi, na uamuzi wake sahihi unatokana na upelelezi kamili na ulio wa lazima na kwa kuzipima na kuziweka pamoja habari za aina mbali mbali zilizokusanywa kwa kufanya upelelezi. Anatumia kila njia inayowezekana na ya lazima kwa kufanyia upelelezi, na anapima habari zilizokusanywa kuhusu hali ya adui, kuzitupa zile zisizo na maana na kuchagua zilizo muhimu, kuziwacha zile za uwongo na kuziweka za kweli, akianzia la kwanza na kwendea la pili na kutoka nje kwendea ndani; tena, hufikiria hali ya mambo ya upande wake mwenyewe, na kuzisoma kwa makini pande zote mbili na mahusiano kati yao, kwa namna hiyo anafanya uamuzi wake, anakata shauri na

kupanga mipango yake. Huo ndio mwenendo kamili wa kuijua hali ya mambo ambao bingwa wa kijeshi anaupitia kabla hajaunda mpango wa hila ya jumla ya vita, mpango wa kampeni au mpango wa mapigano.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

24. KUSAHIHISHA MAWAZO YA MAKOSA

Hata kama tunapata mafanikio makubwa kabisa katika kazi yetu, hapana sababu yo yote ya kujiona na kuwa na kiburi. Unyenyekevu unamsaidia mtu kusonga mbele, na majivuno yanamfanya mtu abakie nyuma. Huu ni ukweli ambao siku zote lazima tuutie akilini.

"Hotuba ya Ufunguzi Katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kitaifa wa Chama cha Kikomunisti cha China" (Septemba 15, 1956).

Kwa sababu ya ushindi, tabia fulani huenda zikakua ndani ya Chama — kiburi, mtu kujipa mwenyewe sifa ya ushujaa, uzito na kutopendelea kusonga mbele, kupenda anasa na kuchukia kuendelea na

maisha magumu. Kwa sababu ya ushindi, umma utatushukuru na mabepari watajitokeza kutuvisha vilemba vya ukoka. Imethibitishwa kwamba adui hawezi kututeka kwa nguvu za silaha. Juu ya hivyo, sifa za uhange zitolewazo na mabepari huenda zikawateka wale wenye nyoyo dhaifu miongoni mwetu. Huenda wakawepo baadhi ya Wakoministi ambao hawakutekwa na maadui wenye bunduki na kwa hivyo wastahili sifa ya mashujaa kwa kupambana na maadui hawa, lakini ambao hawawezi kuzizuia risasi zilizopakwa sukari; watashindwa kwa risasi zilizopakwa sukari. Lazima tujihadhari na hali ya mambo kama hiyo.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Vitu vingi vinaweza vikawa mizigo, vinaweza vikaleta dhiki kama tutaving'ang'ania kwa upofu bila ya kuvipima.

Natuchukue baadhi ya mifano. Baada ya kufanya makosa, unaweza ukahisi kwamba, lije litakalokuja, mambo yameshakuzonga na kwa hivyo ukavunjika moyo; kama hukufanya makosa, unaweza ukajihisi kwamba huna makosa na kwa hivyo ukajiona. Ukosefu wa mafanikio katika kazi unaweza ukazaa fikra za kuvunjika moyo na kuwa na huzuni, na ilhali mafanikio yanaweza kuzaa majivuno na kiburi. Komredi ambaye hajakuwemo katika mapigano kwa muda mrefu anaweza kukataa kuchukua dhamana kwa sababu hii, na kwa wakati huo huo mtu aliyebobea katika mapigano anaweza akajiona kwa sababu ya sifa yake ya mapigano marefu. Makomredi walio wafanya kazi na wakulima, kwa sababu ya kujivunia asili yao ya kitabaka, huenda wakawadharau wataalamu, na huku wataalamu, kwa sababu wanacho kiwango fulani cha ujuzi, huenda wakawadharau makomredi walio wafanya kazi na wakulima. Ustadi wo wote maalum unaweza kufanywa kuwa kama rasilmali na kwa hivyo huenda ukaleta kiburi na kuwadharau wengine. Hata umri wa mtu huenda ukawa

sababu ya majivuno. Vijana kwa sababu ya uhodari na uwezo wao, huenda wakawadharau vizee; na vizee kwa sababu wana maarifa mengi huenda wakawadharau vijana. Vitu vyote kama hivyo vinaleta dhiki au mizigo kama hapana ufahamu wa kuvipima.

"Masomo Yetu na Hali ya Mambo" (Aprili 12, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Baadhi ya makomredi katika jeshi wamekuwa na majivuno na ujeuri katika tabia yao mbele ya askari, umma, serikali na Chama, na siku zote huwalaumu makomredi wanaofanya kazi za kienyeji na milele hawajilaumu wenyewe; wao siku zote wanaona mafanikio yao tu lakini maisha hawaoni upungufu wao, na siku zote wanakaribisha kuvishwa vilemba vya ukoka lakini hawakaribishi kutolewa makosa. . . . jeshi lazima lijitahidi kuondosha upungufu huu.

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kazi ngumu ni kama mzigo uliowekwa mbele yetu, tukitizamwa kama tunathubutu kuubeba. Mizigo mingine ni mepesi, mingine mizito. Baadhi ya watu wanaipendelea mizigo mepesi na huikimbia mizito; wao huichukua mizigo mepesi na kuisukuma ile mizito kwa wengineo. Hii si tabia njema. Baadhi ya makomredi ni tofauti: wao huwaachia wengine raha na wao wenyewe kuichukua mizigo ilio mizito; wao ndio wa mwanzo wa kuvumilia shida, na wa mwisho wa kula raha. Watu hao ni makomredi wazuri, na ni lazima tusome kutokana na moyo huo wa mkoministi.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Wako watu kadha wasio na tabia ya madaraka katika kazi yao, wapendeleao kazi nyepesi na kuikimbia kazi nzito, wanaowapa wenzao kazi ngumu na wao wenyewe kujichagulia kazi nyepesi. Katika kila kitu, wao wanajifikiria binafsi kabla ya kuwafikiria watu wengine. Wanapoifanya kazi

ndogo ya manufaa, wao mara hujaa majivuno na hulisema jambo hilo kila waendapo kwa kuogopea wengine hawatolijua. Hawana ukunjufu, huruma, hawawajali, na ni watepetevu kwa makomredi wenzao na umma. Kusema kweli, watu kama hao si Wakoministi au kwa uchache hawawezi kuhesabiwa kama ni Wakoministi wa kikweli kweli.

"Kwa Ajili ya Ukumbusho wa Norman Bethune" (Desemba 21, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Wale wanaong'ang'ania kijeuri aina hii ya "uhuru" kwa kawaida wanakuwa wameyakumbatia mawazo ya "mimi kwanza" na mara nyingi wanakosea katika suala la mahusiano baina ya mtu binafsi na Chama. Ijapokuwa kwa maneno wao wanajidai kuheshimu Chama, lakini katika vitendo wao wenyewe wanajiweka kwanza na Chama mwahala pa pili. Watu hawa wanataka nini? Wanataka fahari na hadhi na wanataka kujipatia jina. Wakati wanapopewa dhamana

ya sehemu fulani ya kazi, wao hung'ang'ania kijeuri "uhuru" wao. Kwa madhumuni haya, wao huwaingiza ndani baadhi ya watu na kuwatoa nje wengineo na wanafanya mambo ya kujisifu sifu, kuvalishana vilemba vya ukoka na urafiki wa kujipatia faida za kibinafsi miongoni mwa makomredi, na kwa hivyo kuleta mtindo muovu wa vyama vya kisiasa vya kibepari katika Chama cha Kikoministi. Ni ukosefu wao wa uaminifu ambao unawaletea majonzi. Naamini kwamba inatupasa kufanya mambo kwa uaminifu, kwani bila ya tabia ya uaminifu ni muhali kabisa kutimiza jambo lo lote katika ulimwengu huu.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

-

Wakoministi lazima waielewe kanuni ya kuziweka haja za sehemu chini ya haja za jumla. Ikiwa shauri linaonyesha linafaa kwa sehemu ya hali ya mambo lakini halifai kwa hali nzima, basi sehemu lazima iipishe hali

nzima. Kinyume cha hivyo, ikiwa shauri si muwafaka kwa sehemu fulani lakini ni muwafaka kwa hali nzima kwa jumla, kwa mara nyengine sehemu lazima iipishe hali nzima. Huu ndio mtizamo wa kuzingatia hali yote kwa jumla.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kusaka taanasa. Katika Jeshi Jekundu vile vile wako kiasi cha watu ambao ubinafsi wao unajitokeza katika kusaka taanasa. Siku zote wanatumaini kwamba kikosi chao kitakwenda kwenye miji mikubwa. Wanataka kwenda huko sio kwa ajili ya kufanya kazi bali kujistarehesha. Kitu wasichokipendelea kabisa ni kufanya kazi katika Maeneo Mekundu ambako maisha ni magumu.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Lazima tuupinge muelekeo wa uchoyo wa kiidara [*departmentalism*], ambao unamfanya mtu kuangalia maslaha ya idara yake tu na kutoyajali maidara mengineo. Ye yote asiyejali shida za wengine, anayekataa kuwapeleka makada walioko chini ya uongozi wake katika idara nyengine wakati anapoombwa kufanya hivyo, au kuwachilia makada wabaya tu, "kutumia konde la jirani kama ni tundu la kutolea mfuriko wa kondeni mwake" na kutozingatia hata chembe maidara mengine, mwahala mwengine na watu wengine — mtu kama huyo ni mchoyo wa kiidara ambaye ameutupa kabisa moyo wa kikoministi. Kutofikiria hali ya mambo kwa jumla na kutojali kabisa idara nyenginezo, mwahala mwengineko au watu wengineo ni tabia maalum ya mchoyo wa kiidara. Lazima tuengeze juhudi zetu kuwaelimisha watu kama hao na kuwafanya waelewe kwamba uchoyo wa kiidara ni muelekeo wa fikra za kufuata madhehebu

ambao utakuwa wa hatari sana pindi ukiachiliwa kukua.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mawazo ya kiliberali yajitokeza kwa namna nyingi.

Kuyawacha mambo yaende ovyo ovyo kwa ajili ya amani na urafiki katika wakati ambapo mtu kafanya makosa ya dhahiri na kutofanya mabishano ya msingi kwa sababu mtu aliyefanya makosa ni mtu unayejuana naye tokea zamani, mtu wa mji mmoja naye, mmesoma shule pamoja au ni rafiki yako mkubwa, mpenzi wako, mwenzako wa kazini wa zamani au mfuasi wako wa zamani. Au kulitoa makosa jambo fulani kwa kijuu juu tu badala ya kulisahihisha kikweli, ili kuendeleza masikilizano naye. Matokeo ni kwamba chama pamoja na mtu anayehusika wote watadhurika. Hii ni aina ya kwanza ya mawazo ya kiliberali.

Kulitoa makosa jambo kwa njia isiyo ya madaraka katika mwahala pa faragha badala ya kuyapeleka mashauri yako kwa chama kwa juhudi. Kutowaambia watu cho chote mbele ya uso wao na badala yake kunong'ona nong'ona nyuma ya mgongo wao, au kutosema cho chote katika wakati wa mkutano na badala yake kunong'ona nong'ona baadaye. Kuonyesha kutoheshimu msingi wa maisha ya pamoja na badala yake kufanya mambo kama unavyojitakia mwenyewe. Hii ni aina ya pili.

Kuyawacha mambo yajiendee ovyo ovyo maadam hayakuathiri wewe binafsi; kusema kidogo kama iwezekanavyo na ilhali unajua wazi makosa gani yaliyofanywa. Kuwa mwerevu na kutojitia "matatani" ili kujitafutia kuepuka lawama. Hii ni aina ya tatu.

Kutotii amri na badala yake kuwa na majivuno juu ya maoni yako. Kudai fursa maalum katika chama lakini kupuuza nidhamu zake. Hii ni aina ya nne.

Kumshambulia mtu binafsi, kufanya ugomvi usio na maana, kuzimwaga chuki zako za kibinafsi au kulipiza kisasi badala

ya kufanya jihadi na mabishano dhidi ya mawazo yasio barabara kwa ajili ya umoja, maendeleo au kazi kufanywa vizuri. Hii ni aina ya tano.

Kuyasikia maoni yasiyo barabara bila ya kuyapinga na hata kuyasikia maneno ya wapinga mapinduzi bila ya kuyaripoti, na badala yake kunyamaa kimya kama vile hapana lo lote lililotokea. Hii ni aina ya sita.

Kuwa miongoni mwa umma bila ya kueneza siasa ya chama, kutowashajiisha, kutosema cho chote, kutofanya uchunguzi miongoni mwao au kutowauliza hali zao na kutowajali na kutofanya jambo lo lote katika kutengeza maisha yao na kujisahau kama ni Mkoministi — yaani Mkoministi kujiweka kama vile ni mtu wa kidesturi asiye Mkoministi. Hii ni aina ya saba.

Kumwona mtu akiyadhuru maslaha ya umma na bila ya kuhamaki, kumnasihi asitishe vitendo vyake au kumzuia na kumfahamisha na badala yake kumwachia aendelee na vitendo vyake viovu. Hii ni aina ya nane.

Kufanya kazi kwa shingo upande bila ya mpango au muelekeo maalum; kufanya kazi

kwa uzembe na kujipurukusha purukusha — "Maadam mtu ni *monk* basi ataendelea kupiga kengele ya hekalu". Hii ni aina ya tisa.

Kujifikiria kama umefanya kazi kubwa katika mapinduzi, kujivunia kama ni mtu mkubwa, kupuuza kazi ndogo ndogo na ilhali kazi kubwa huwezi kuzifanya, kufanya kazi ovyo ovyo na kutojitahidi katika kujifunza. Hii ni aina ya kumi.

Kufahamu makosa yako na ilhali hufanyi jambo lo lote katika kuyasahihisha makosa yako — yaani kujitendea kwa tabia ya kiliberali. Hii ni aina ya kumi na moja.

"Yapinge Mawazo ya Kiliberali" (Septemba 7, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mawazo ya kiliberali yana madhara makubwa kwa mkusanyiko wa kimapinduzi. Mawazo haya ni kama kutu inayodhoofisha umoja na kuharibu mafungamano, inayosababisha utepetevu na kuleta mafarikiano. Mawazo haya yanawafanya wana-mapinduzi kutoungana imara katika chama chao, yaharibu nidhamu kamili, yanazuia siasa

kutekelezwa kwa ukamilifu na yanaleta mtengano baina ya Chama na umma unaoongozwa na Chama. Ni mwendo mbaya kabisa.

Kama juu.

Watu wenye mawazo ya kiliberali wanaifikiria misingi ya Umarx kama ni maneno ya vitabuni ya kubuni vichwani tu. Wao wanaukubali Umarx lakini hawako tayari kuutekeleza au kuutekeleza kwa ukamilifu; wao hawako tayari kuyatupa mawazo yao ya kiliberali na kuufuata kikweli Umarx. Watu hawa wanao Umarx na vile vile wanayo mawazo ya kiliberali. Wao hubobozokwa juu ya Umarx lakini vitendo vyao ni vya mawazo ya kiliberali. Wao wanautekeleza Umarx juu ya watu wengine lakini, kuhusu wao wenyewe, wanayatekeleza mawazo ya kiliberali. Wanazo bidhaa za aina mbili ghalani kwa matumizi mbali mbali. Hivyo ndivyo zinavyofanya kazi akili za baadhi ya watu.

Kama juu.

Dola ya watu inawahami watu. Ni watu wanapokuwa na dola kama hiyo tu ndio wanaweza kujisomesha na kujigeuza kuwa bora kwa njia za kidemokrasi nchini kote, kila mmoja akishiriki, na kujiepusha na athari za wapinga maendeleo wa nchini na wa nje (ambazo bado ni kubwa sana, zitadumu kwa muda mrefu na haziwezi kuondoshwa kwa upesi), kujiondoshea desturi na fikra mbaya zinazotokana na jamii kongwe, kujizuia kupotezwa njia na wapinga maendeleo na kuendelea kusonga mbele — kusonga mbele kuelekea jamii ya kisoshalisti na kikoministi.

> "Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Si vigumu kwa mtu kutenda wema kidogo. Vigumu ni mtu kutenda wema maisha yake yote na maisha asifanye jambo baya, daima kufanya mambo yanayoambatana na maslaha ya umma mkubwa, vijana na mapinduzi, na kufanya jitihada kwa ushupavu kwa makumi

ya miaka. Hicho ndicho kitu kigumu kuliko vyote.

"Salamu za Pongezi kwa Kutimia Miaka 60 Tangu Kuzaliwa Komredi Wu Yu-chang" (Januari 15, 1940).

25. UMOJA

Muunganisho wa nchi yetu, umoja wa watu wetu na umoja wa mataifa mbali mbali ya nchi yetu — hizi ndizo dhamana za msingi za kuhakikisha ushindi wa jihadi yetu.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Ni kwa umoja wa Chama cha Kikomunisti tu ndio umoja wa tabaka lote na taifa lote unaweza kupatikana, na kwa umoja wa tabaka lote na taifa lote ndio adui anaweza kushindwa na kazi za mapinduzi ya kitaifa na ya kidemokrasi zinaweza kutimizwa.

"Uvute Umma kwa Mamilioni kwa Ajili ya Muungano wa Pamoja wa Taifa Dhidi ya Japani" (Mei 7, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Tutaziunganisha imara nguvu zote za Chama chetu kwa kanuni za ujumuia na nidhamu za mpango wa demokrasi-uongozi. Tutaungana na kila komredi ikiwa anakubali kufuata Mpango, Katiba na maazimio ya Chama.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Njia hii ya kidemokrasi ya kutanzua hitilafu miongoni mwa umma ilifupishwa katika mwaka 1942 kwa kifungu cha maneno "umoja, utoaji makosa, umoja". Kwa urefu, ina maana ya kuanza kutokana na hamu ya kuwa na umoja, kutanzua hitilafu kwa kutoa makosa au kwa mapigano na kufikia umoja mpya juu ya msingi mpya. Kwa maarifa yetu, hii ndio njia sahihi ya kutanzua hitilafu miongoni mwa umma.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Jeshi [letu] hili limepata umoja unaostahili sifa kati ya safu zake na pia na wale

wasiokuwa katika safu zake. Ndani ya jeshi, kuna umoja baina ya maofisa na maaskari, baina ya wenye vyeo vya juu na wenye vyeo vya chini, na baina ya kazi ya kijeshi, kazi ya kisiasa na kazi ya kutoa mahitajio ya kijeshi. Nje ya jeshi, kuna umoja baina ya jeshi na umma, baina ya jeshi na serikali, na baina ya jeshi letu na majeshi ya kirafiki. Ni jambo la lazima kukishinda kitu cho chote kinachoharibu umoja huu.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

26. NIDHAMU

Miongoni mwa umma, demokrasi inafuatana na uongozi, na uhuru unafuatana na nidhamu. Hizi ni pande mbili zinazopingana katika kitu chenyewe hasa, pande ambazo zinahitilafiana na kuungana kwa wakati huo huo, na kwa hivyo tusitilie mkazo upande mmoja tu kwa kukanusha upande mwengineo. Miongoni mwa umma, hauwezi kukosekana uhuru, kama vile haiwezi kukosekana nidhamu; na haiwezi kukosekana demokrasi, kama vile hauwezi kukosekana uongozi. Umoja huu wa demokrasi na uongozi, wa uhuru na nidhamu, ndio unaofanya mpango wetu wa demokrasi-uongozi. Chini ya mpango huu, umma unapata demokrasi na uhuru wa

kutosha, na kwa wakati huo huo inawabidi wasiikiuke nidhamu ya kisoshalisti.

Juu ya Kutanzua kwa Usahibi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Lazima tuzitilie nguvu upya nidhamu za Chama, nazo ni:

(1) kila mtu binafsi yuko chini ya Chama;

(2) wachache wako chini ya wengi;

(3) daraja ya chini iko chini ya daraja ya juu; na

(4) wanachama wote wako chini ya Kamiti Kuu.

Ye yote anayevivunja vifungu hivi vya nidhamu anaharibu umoja wa Chama.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mojawapo ya nidhamu za Chama ni kwamba wachache wawe wanawasikiliza walio wengi. Kama maoni ya wachache yamekataliwa, basi ni lazima waunge mkono azimio lililopasishwa na wengi. Ikiwa inahitajika, wao wachache wanaweza kulileta jambo hilo kuzingatiwa tena kwenye mkutano unaofuata lakini mbali ya kitendo hichi, wao ni lazima kwa namna yo yote wasitende cho chote kinyume na azimio lililopasishwa.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Kanuni Tatu Kuu za Nidhamu ni kama zifuatazo:

(1) Fuata amri katika vitendo vyako vyote.
(2) Usichukue hata sindano moja au kipande cha uzi cha umma.
(3) Kilete kila kitu ulichokiteka.

Mambo Manane ya Kuangaliwa ni kama yafuatayo:

(1) Sema kwa upole.
(2) Toa malipo ya haki kwa kila kitu unachokinunua.
(3) Rejesha kila kitu unachokiazima.
(4) Toa malipo kwa cho chote unachokiharibu.
(5) Usiwapige watu wala usiwatukane.
(6) Usiharibu mimea.
(7) Usijichukulie uhuru kwa wanawake.
(8) Usiwatendee vibaya mateka.

"Juu ya Kutolewa Tena Kanuni Tatu Kuu za Nidhamu na Mambo Manane ya Kuangaliwa — Amri ya Makao Makuu ya Jeshi la Ukombozi la Umma la China" (Oktoba 10, 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Wao [maofisa na maaskari wote wa jeshi letu] lazima waongeze ufahamu wao wa nidhamu na kwa uthabiti watekeleze amri, watekeleze siasa yetu, watekeleze Kanuni Tatu Kuu za Nidhamu na Mambo Manane ya Kuangaliwa, lazima jeshi na umma kuungana, jeshi na serikali kuungana, maofisa na maaskari kuungana na jeshi letu

zima kuungana, na wasiruhusu uvunjaji wo wote wa nidhamu.

"Tangazo Kuu la Jeshi la Ukombozi la Umma la China" (Oktoba 1947), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

27. KUTOA MAKOSA NA KUJITOA MAKOSA

Chama cha Kikoministi hakiogopi kutolewa makosa kwa sababu sisi ni wafuasi wa Umarx, ukweli uko upande wetu, na umma wa msingi — wafanya kazi na wakulima — wako upande wetu.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Watu wanaoamini kikweli elimu ya uyakinifu ni mashujaa wasio na hofu yo yote; tunatumainia kwamba wapiganaji wenzetu wote, kwa ushujaa, watabeba majukumu yao na watazishinda shida zote, hawatoogopa vipingamizi, minong'ono au

kejeli wala hawatochelea kututoa makosa sisi Wakoministi na kutuambia mashauri yao. "Yule asiyeogopa kifo cha kukatwa vipande vipande anathubutu kumwangusha mfalme kutoka kwenye farasi" — wakati tunapopigania usoshalisti na ukoministi lazima tuwe na moyo huu mkubwa usioshindika.

Kama juu.

Tunayo silaha ya Kimarx-lenin ya kutoa makosa na kujitoa makosa. Tunaweza kuuondosha mtindo mbaya na kuudumisha ule mzuri.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kufuata au kutofuata njia ya kujitoa makosa kwa udhati ni alama nyengineyo iliyo dhahiri ya mpambanuo baina ya Chama chetu na vyama vyenginevyo vyote

vya siasa. Kama tulivyosema, vumbi litakusanyika ikiwa chumba hakifagiliwi mara kwa mara, nyuso zetu zitakuwa chafu kama hazioshwi mara kwa mara. Akili za makomredi wetu na kazi za Chama chetu vile vile huenda zikaingiwa na vumbi, na vile vile zinahitaji kufagiliwa na kuoshwa. Ule mfano usemao "Maji yanayokwenda daima hayanuki na bawaba ya mlango hailiwi na mchwa" unakusudia kwamba mwendo wa daima unaepusha vijia vya vidudu vibaya na wadudu wengineo. Kuikagua kazi yetu kila baada ya muda na katika mwenendo huu kuikuza mitindo ya kidemokrasi ya kufanya kazi, kutoogopa kutolewa makosa na wala kujitoa makosa, na kuzitumia zile methali mashuhuri zenye faida za watu wa China kama "Sema kila unalolijua na bila ya kubania", "Usimlaumu msemaji bali chukulia maneno yake kama ni onyo" na "Yasahihishe makosa kama umeyafanya na jihadharishe nayo kama hukuyafanya" — hii ndio njia ya pekee inayofaa katika kuzuia aina zote za mavumbi ya siasa na vidudu vibaya vya siasa kuzitia

ugonjwa akili za makomredi wetu na mwili wa Chama chetu.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Upinzani na mapigano baina ya fikra za aina mbali mbali daima yanatokea ndani ya Chama; huu ni mmathilisho ndani ya Chama wa hitilafu baina ya matabaka na baina ya mambo mepya na makongwe katika jamii. Ndani ya Chama ingelikuwa hapana hitilafu na hapana mapigano ya kifikra kwa ajili ya kuzitanzua, basi maisha ya Chama yangesita.

"Juu ya Hitilafu" (Agosti 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Sisi tunatetea kufanya mapigano ya kifikra yenye msingi, kwa sababu hiyo ni silaha ya kuhakikisha umoja katika Chama cha Kikoministi na vyama vyenginevyo vya kimapinduzi kwa ajili ya maslaha ya mapigano yetu. Kila Mkoministi na kila

mwana-mapinduzi lazima aichukue silaha hii.

Lakini mawazo ya kiliberali yanakataa mapigano ya kifikra na yanataka amani isio na msingi, na kwa hivyo huleta kuchomoza tabia mbovu na mwendo mbaya wa kushughulikia mambo ya upuuzi na kuleta uharibikaji wa kisiasa miongoni mwa baadhi ya maidara na watu waliomo katika Chama chetu na vyama vyengine vya kimapinduzi.

"Yapinge Mawazo ya Kiliberali" (Septemba 7, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika kupinga tabia ya kuweka mbele fikra za mtu mwenyewe, fikra za kufuata madhehebu na maandishi ya Chama ya namna hiyo kwa hiyo tu kila siku, lazima akilini mwetu tuwe na madhumuni mawili: kwanza, "soma kutokana na makosa ya zamani ili kuepukana na yajayo", na pili "yatibu maradhi ili kumuokoa mgonjwa". Makosa ya zamani lazima yafichuliwe bila

ya kuchelea kwamba mtu fulani atachukizwa; ni lazima kuchambua na kutoa makosa kwa tabia ya kisayansi ubaya wa zamani ili kazi katika siku za mbele zifanywe kwa hadhari zaidi na vyema zaidi. Hii ndio inaokusudiwa kwa "soma kutokana na makosa ya zamani ili kuepukana na yajayo". Lakini madhumuni yetu katika kufichua makosa na kutoa makosa upungufu, kama yale ya daktari anavyoyatibu maradhi, ni kwa ajili ya kumuokoa mgonjwa tu na sio kumfanyia uganga wa kumuua. Mtu mwenye kuumwa *appendix* anaokolewa wakati daktari anapoikata *appendix* yake. Madhali mtu ye yote aliyefanya makosa hafichi maradhi yake kwa hofu ya kutibiwa au haendelei na makosa kwa ukaidi mpaka akawa hawezi kutibiwa, madhali kwa kweli na kwa dhati anataka kutibiwa na kujisahihisha, basi inatupasa tumkaribishe na tumtibu maradhi yake ili aweze kuwa komredi mzuri. Daima hatuwezi kufaulu kama tunasikiza hamaki zetu tu na kumshambulia ovyo. Katika kuutibu ugonjwa wa kifikra au wa kisiasa, mtu lazima asijitie nguvu na papara bali lazima

achukue msimamo wa "yatibu maradhi ili kumuokoa mgonjwa" ambayo ndio njia pekee sahihi na inayofaa.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Jambo jengine ambalo linahitaji kutajwa kuhusu utoaji makosa wa ndani ya Chama ni kwamba baadhi ya makomredi wanapuuza matatizo muhimu na wanashughulikia mambo madogo madogo wakati wanapotoa makosa. Hawafahamu kwamba kazi kubwa katika kutoa makosa ni kuonyesha makosa ya kisiasa na ya matengenezo. Kuhusu upungufu wa mtu binafsi, madhali haujahusika na makosa ya kisiasa na ya matengenezo, basi hapana haja ya kutoa makosa kupita kiasi au makomredi waliohusika watakuwa hawajui nini la kufanya. Zaidi ya hayo, mara tu utoaji makosa kama huo unapoendelea, kuna hatari kubwa kwamba ndani ya Chama hadhari yote itakuwa kwenye makosa madogo madogo tu,

na kila mmoja atakuwa mwoga na mwenye wasi wasi kupita kiasi na kusahau kazi za siasa za Chama.

"Juu ya Kusahihisha Mawazo ya Makosa Katika Chama" (Desemba 1929), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Katika utoaji makosa wa ndani ya Chama, jihadhari na mambo ya kuweka mbele fikra za mtu mwenyewe, kukata shauri peke yako na kujishughulisha na mambo ya upuuzi; sema maneno yenye ushahidi thabiti na utoaji makosa utilie mkazo upande wa siasa.

Kama juu.

Utoaji makosa wa ndani ya Chama ni silaha ya kukazanisha matengenezo ya Chama na kuengeza nguvu zake za mapigano. Lakini utoaji makosa ndani ya Chama katika Jeshi Jekundu baadhi ya wakati sio wa namna hii, na wakati mwengine unageuka kuwa mashambulizi juu ya mtu binafsi. Matokeo yake ni kuyadhuru

matengenezo ya Chama na vile vile watu binafsi. Haya ni madhihirisho ya ubinafsi wa mabepari wadogo. Njia ya kusahihisha ni kuwasaidia wanachama kufahamu kwamba madhumuni ya utoaji makosa ni kuongeza nguvu za mapigano za Chama ili kupata ushindi katika mapigano ya kitabaka na kwamba usitumiwe kama ni fursa ya kumshambulia mtu binafsi.

Kama juu.

Ikiwa tunao upungufu, hatuogopi kuonyeshwa na kutolewa makosa, kwa sababu sisi tunatumikia umma. Mtu ye yote, haidhuru ni nani, anaweza kutuonyesha makosa yetu, na ikiwa jambo analolisema ni barabara basi tutayasahihisha makosa hayo. Kama shauri lake litanufaisha umma, basi tutalitekeleza.

"Tumikia Umma" (Septemba 8, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ilivyokuwa sisi Wakoministi wa China tunafanya kila jambo kwa kufikiria maslaha ya juu kabisa ya umma mkubwa

kabisa wa watu wa China na tunaamini kamili haki ya jihadi yetu, daima hatuogopi kupoteza cho chote chetu binafsi na tuko tayari wakati wo wote kujitolea mhanga maisha yetu kwa ajili ya jihadi yetu, jee tunaweza kuona taabu kuwacha fikra, mtizamo, maoni au njia yo yote ambayo haiambatani na mahitajio ya umma? Tunaweza kuwa radhi kuachilia mavumbi na vidudu vya siasa kuzitia uchafu nyuso zetu safi au kuingia katika miili yetu yenye siha? Mashujaa wasio na hesabu wa kimapinduzi wamejitolea maisha yao kwa ajili ya maslaha ya umma, na nyoyo zetu zinaungulika tunapowakumbuka, basi panaweza kuwepo maslaha ya mtu binafsi ambayo hatuwezi kuyatupa au makosa yo yote ambayo hatuwezi kuyaacha?

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Tusiridhike na mafanikio yo yote yanayopatikana. Ni juu yetu kujihadhari na maridhiko na mara kwa mara tutoe makosa upungufu wetu, kama vile inavyotubidi

kuosha nyuso zetu au kufagia sakafu kila siku ili kuondosha uchafu na kuziweka safi.

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Ama kuhusu utoaji makosa, inahitaji ufanywe kwa wakati; usiwe na tabia ya kutoa makosa baada ya jambo kupita.

Juu ya Suala la Ushirika wa Kilimo (Julai 31, 1955).

Kwa kufunzwa na makosa na vipingamizi, tumepata busara zaidi na tunayaendesha mambo yetu vyema zaidi. Ni vigumu kwa chama cho chote cha kisiasa au mtu ye yote kuepuka makosa, lakini tufanye makosa machache kama inavyoyumkinika. Mara tu baada ya makosa kufanywa, tuyasahihishe, na kila yakisahihishwa kwa upesi na kwa ukamilifu zaidi ndio bora zaidi.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

28. WAKOMINISTI

Mkoministi lazima awe kapanuka akili yake, mtiifu na mtu imara mwenye juhudi, lazima ayafikirie maslaha ya mapinduzi kama ni maisha yake hasa, na maslaha yake mwenyewe yawe chini ya maslaha ya mapinduzi; siku zote na kila mwahala, ashikilie kufuata msingi sahihi pamoja na kufanya mapigano bila ya kuchoka dhidi ya mawazo yasio sahihi na vitendo visivyo sahihi, ili kuimarisha maisha ya pamoja ya Chama na kutilia nguvu maingiliano ya Chama na umma; lazima ajishughulishe zaidi na Chama na umma kuliko mtu binafsi, na awafikirie watu wengine zaidi kuliko anavyojifikiria yeye mwenyewe. Ni

kwa namna hiyo tu ndiyo ataweza kufikiriwa kuwa ni Mkoministi.

"Yapinge Mawazo ya Kiliberali" (Septemba 7, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kila komredi lazima afahamishwe kwamba kipimo cha juu kabisa cha maneno na vitendo vyote vya Mkoministi ni kama maneno na vitendo vyake vinakubaliana na maslaha ya juu kabisa ya umma mkubwa kabisa wa watu na vinaungwa mkono nao.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Mkoministi inampasa, katika wakati wo wote na mahali po pote, asiyaweke mbele maslaha yake, bali ayaweke chini ya maslaha ya taifa na ya umma wa watu. Kwa hivyo, uchoyo, ulegevu, upotofu, kupigania

umaarufu, na kadhalika, ni mambo yanayodharauliwa kabisa, lakini kutojifikiria binafsi, kufanya kazi kwa juhudi, kujisabilia katika kazi za umma kwa moyo wote, na kufanya kazi kimya kwa bidii huleta heshima.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Wakoministi lazima wawe tayari wakati wote kuushikilia ukweli, kwa sababu ukweli wo wote unaambatana na maslaha ya umma; Wakoministi lazima wawe tayari wakati wote kusahihisha makosa yao, kwa sababu makosa yo yote hayaambatani na maslaha ya umma.

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Wakoministi lazima siku zote wajiulize kwa nini jambo lo lote kutokea, watumie vichwa vyao na kwa makini wapime kama

kitu hicho kinakubaliana na ukweli wa mambo au la na kama kweli kina msingi imara; kwa hali yo yote wasifuate kama vipofu na kushajiisha tabia ya utumwa.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Inatubidi tuwahimize makomredi kufikiria maslaha ya kitu kizima. Kila mwanachama wa Chama, kila tawi la kazi, kila taarifa na kila kitendo ni lazima kuanzia kutoka maslaha ya Chama kizima; hairuhusiki kabisa kuivunja kanuni hii.

Kama juu.

Wakoministi lazima waweke mfano katika kufanya vitendo vinavyoambatana na ukweli wa mambo na kuwa na busara ya

kuona mbali. Kwani ni kwa kufanya vitendo vinavyoambatana na ukweli wa mambo tu ndio huweza kutimiza kazi walizopewa, na kwa kuwa na busara ya kuona mbali tu ndio huweza kujizuia kupoteza njia ya kusongea mbele.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Wakoministi inawabidi wawe wanaoona mbali kabisa, wanaojitolea mhanga kuliko wote, imara kuliko wote, na walio wanyenyekevu kuliko wote katika kupima hali ya mambo, na ni lazima wautegemee wingi wa umma na wapate kuungwa mkono nao.

"Kazi za Chama cha Kikoministi cha China Katika Wakati wa Kupinga Ushambulizi wa Japani" (Mei 3, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Wakoministi tena lazima waweke mfano katika kusoma; siku zote wawe walimu na vile vile wanafunzi wa umma.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Kila Mkoministi anayeshughulika katika mavugu vugu ya umma inambidi awe rafiki wa umma na sio bwana wao, awe mwalimu asiyechoka na sio mwana-siasa wa kibwanyenye.

Kama juu.

Wakoministi wasijitenge abadan na wingi wa umma au kuwapuuza kwa kuongoza vikundi vichache vilivyoendelea katika kusonga mbele kwa njia ya upweke na ya papara, bali lazima wachukue hadhari kufanya maingiliano imara baina ya wale walioendelea mbele na umma mkubwa. Hii ndio maana ya kufikiri kwa mujibu wa walio wengi.

Kama juu.

Sisi Wakoministi ni kama mbegu na umma ni kama ardhi. Po pote twendapo lazima tuungane na umma, tuoteshe mizizi na tuchanue kati yao.

"Juu ya Mazungumzo ya Chungking" (Oktoba 17, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Sisi Wakoministi lazima tuweze kujiunga na umma katika mambo yote. Ikiwa wanachama wetu wa Chama wanapitisha maisha yao yote kukaa ndani na hawaendi nje kupambana na dharuba na kuikabili dunia, watakuwa na maana gani kwa watu wa China? Hawatakuwa na maana yo yote, na hatuna haja ya watu kama hao kuwa wanachama wa Chama. Sisi Wakoministi inatubidi kupambana na dharuba na kuikabili dunia, dharuba kali ya mapigano ya umma na dunia kubwa ya mapigano ya umma.

"Jikusanyeni!" (Novemba 29, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kuwa mbele na kuweka mfano ni jambo muhimu sana kwa Wakoministi. Wakoministi katika Jeshi la Njia ya Nane na Jeshi Jipya la Nne lazima waweke mfano katika kupigana kwa ushujaa, kutekeleza amri, kufuata nidhamu, kufanya kazi za kisiasa na kukuza muungano na umoja wa ndani.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mkoministi abadan asijifikirie kuwa kila jambo lake ni barabara, kuwakalia watu juu, kujifikiria kwamba yeye ni hodari katika kila kitu na kwamba wengine si hodari katika cho chote; abadan asijifungie ndani ya chumba chake kidogo, au kujigamba na kujisifu na kuwatawala wengine.

"Hotuba Katika Baraza la Wajumbe la Eneo la Mpakani mwa Shensi-Kansu-Ningsia" (Novemba 21, 1941), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Wakoministi lazima wasikilize kwa makini maoni ya watu wa nje ya Chama na wawaachilie waseme. Kama wanayosema ni barabara, inatubidi tuyakaribishe, na tujifunze kutokana na mambo yao yalio bora; ikiwa wasemayo si barabara, tuwaachilie wamalize wanayoyasema na halafu tuwafahamishe mambo yenyewe kwa upole.

Kama juu.

Msimamo wa Wakoministi kwa mtu ye yote aliyefanya makosa katika kazi yake uwe ule wa kumshawishi ili kumsaidia abadilike upesi na kuanza upya na sio ule wa kumtenga, isipokuwa kama hageuziki.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi chà China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Ama kuhusu watu ambao wako nyuma katika siasa, Wakoministi wasiwapuuze au

kuwadharau, bali wafanye urafiki nao, waungane nao, wawatie imani na wawahimize kusonga mbele.

Kama juu.

29. MAKADA

Ili kuhakikisha kwamba Chama chetu na nchi yetu haitobadilika rangi, si kama lazima tuwe na msimamo sahihi na siasa sahihi tu bali lazima tuwafundishe na kuwatayarisha mamilioni ya warithi watakaoendeleza jihadi ya mapinduzi ya kifanya kazi.

Katika uchambuzi wa mwisho, suala la kuwafundisha warithi wa jihadi ya mapinduzi ya kifanya kazi ni suala la kama watakuwapo au hawatakuwapo watu wa kuendeleza jihadi ya mapinduzi ya Umarx-lenin iliyoanzishwa na kizazi cha mababa cha wana-mapinduzi wa kifanya kazi, kama uongozi wa Chama chetu na dola yetu utabaki katika mikono ya wana-mapinduzi wa kifanya kazi au la, kama watoto wetu wataendelea kufuata njia sahihi iliyowekwa na Umarx-lenin au la, kwa maneno mengine,

kama tutaweza au hatutaweza kufaulu katika kuzuia uchomozaji wa ubadilishaji fikra wa Khrushchov katika China. Kwa ufupi, hili ni suala muhimu kabisa, la kufa kupona kwa Chama chetu na nchi yetu. Hili ni suala la umuhimu wa msingi kwa jihadi ya mapinduzi ya kifanya kazi kwa miaka mia, elfu, hata elfu kumi. Kwa kuyachukulia mabadiliko yaliotokea katika Umoja wa Soviet, wabashiri wa kibeberu wanayaweka matumainio yao ya "mabadiliko ya amani" juu ya kizazi cha tatu au cha nne cha Chama cha China. Lazima tuuvunje kabisa ubashiri huu wa kibeberu. Kutoka idara zetu za juu kabisa mpaka chini kabisa, lazima kila mahali tuangalie kwa wakati wote ufundishaji na utayarishaji wa warithi wa jihadi ya mapinduzi.

Warithi wanaostahiki wa jihadi ya mapinduzi ya kifanya kazi lazima wawe na mambo gani?

Lazima wawe wafuasi wa kweli wa Umarx-lenin na sio wabadilishaji fikra kama Khrushchov akivaa joho la Umarx-lenin.

Lazima wawe wana-mapinduzi wanaotumikia kwa moyo wote sehemu kubwa kabisa ya watu wa China na dunia nzima, na wasiwe kama Khrushchov anayetumikia maslaha ya watu wachache wa daraja ya kibepari yenye fursa mahsusi katika nchi yake mwenyewe na maslaha ya ubeberu na wapinga maendeleo katika ulimwengu.

Lazima wawe wana-siasa wa kifanya kazi wenye uwezo wa kuunga na kufanya kazi pamoja na sehemu kubwa kabisa ya watu. Sio kama waungane na wale wanaokubaliana nao tu, bali lazima vile vile wawe mahodari katika kuungana na wale wasiokubaliana nao na hata na wale ambao zamani waliwapinga na baadaye kuthibitishwa kwa vitendo kuwa walikuwa na makosa. Lakini lazima wawe na hadhari zaidi kwa wale wanaojijenga na wapikao majungu kama Khrushchov na kuzuia watu wabaya kama hao wasije wakanyakua uongozi wa Chama na dola katika daraja yo yote.

Lazima wawe mifano ya kutekeleza mpango wa demokrasi-uongozi wa Chama, lazima waishike vyema njia ya uongozi kwa mujibu wa msingi wa "kutoka kwa umma, kurejea kwa umma", na lazima wajizoeze mtindo wa kidemokrasi wa kuweza kuyasikiliza vyema maoni ya umma. Wasiuvunje mpango wa demokrasi-uongozi wa Chama kama afanyavyo Khrushchov, na kuwakalia watu juu, kuwafanyia makomredi ushambulizi wa ghafla au kufanya mambo ya kijeuri na udikteta.

Lazima wawe wanyenyekevu na wenye hadhari na kujiepusha na majivuno na papara; lazima wajae na moyo wa kujitoa makosa na kuwa na ushujaa wa kusahihisha upungufu na makosa katika kazi zao. Daima wasiyafunike makosa yao na kujipa sifa zote na kuwasukumia lawama zote watu wengine kama afanyavyo Khrushchov.

Warithi wa jihadi ya mapinduzi ya kifanya kazi wanatokeza katika mapigano ya umma na wanaimarishwa katika dharuba kubwa za mapinduzi. Ni jambo la lazima kuwajaribu na kuwapambanua makada na

kuwachagua na kuwafundisha warithi katika mwenendo mrefu wa mapigano ya umma.

Maneno yaliyonukuliwa katika *Juu ya Ukoministi wa Uwongo wa Kikhrushchov na Funzo Lake la Kihistoria kwa Ulimwengu* (Julai 14, 1964).

Matawi ya Chama chetu lazima yaenezwe nchini kote na lazima kwa makusudio kuwatayarisha makada kwa makumi ya maelfu na mamia ya viongozi wa umma walio bora kabisa. Wao lazima wawe makada na viongozi wanaojua kikweli Umarx-lenin, wanaoweza kuona mbali kwa kisiasa, wenye uwezo wa kazi, waliojaa moyo wa kujitolea mhanga, wanaoweza kupambana na matatizo wao peke yao, wanaotulia imara katika wakati wa shida na waaminifu na waliojisabilia katika kutumikia taifa, tabaka na Chama. Ni watu hao ambao Chama kinawategemea kujiunganisha na wanachama na umma, na kwa kuutegemea uongozi wao imara juu ya umma ndio Chama kinaweza kufaulu

kumshinda adui. Makada na viongozi kama hao inawapasa wasiwe wachoyo, wasiwe na ushujaa wa kibinafsi, kujionea fahari, uvivu, uzembe, na fikra za kufuata madhehebu kwa kujivuna, na lazima wawe mashujaa wa kitaifa na kitabaka wasiojifikiria binafsi; hizo ndizo sifa na mtindo wa kufanya kazi wanaotakiwa wawe nao wanachama, makada na viongozi wa Chama chetu.

"Uvute Umma kwa Mamilioni kwa Ajili ya Muungano wa Pamoja wa Kitaifa Dhidi ya Japani" (Mei 7, 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Makada ni kitu cha uamuzi baada ya kwisha katwa shauri juu ya msimamo wa kisiasa. Kwa hivyo, ni kazi yetu ya kimapigano kuifundisha idadi kubwa ya makada wepya kwa njia ya mpango.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Katika siasa yake kuhusu makada, Chama cha Kikoministi kimechukua mipambanuo ifuatayo: kama kada anatekeleza kwa uthabiti msimamo wa Chama, kuzifuata nidhamu za Chama, kuingiliana sana na umma, kuwa na uwezo wa kujiongoza mwenyewe, kuwa na harakati, kufanya kazi kwa bidii na kutotafuta maslaha ya binafsi. Hii ndio maana ya "kuwachagua watu kwa mujibu wa sifa zao".

Kama juu.

Ni jambo la lazima kuendeleza mpango wa makada kushiriki katika kazi za pamoja za uchumi. Makada wa Chama chetu na dola yetu ni wafanya kazi wa kawaida na sio mabwana wanaowakalia watu juu ya vichwa. Kwa kushiriki katika kazi za pamoja za uchumi, makada wanaendeleza maingiliano makubwa kabisa, ya daima na imara pamoja na watu wanaoishi kwa jasho lao. Hili ni jambo kubwa lenye umuhimu wa msingi kwa mpango wa kisoshalisti; linasaidia kuondosha mambo ya ubwana-serikali na kuepusha ubadilishaji fikra na

mambo ya kufuata kikasuku maneno ya vitabuni.

Maneno yaliyonukuliwa katika *Juu ya Ukoministi wa Uwongo wa Kikhrushchov na Funzo Lake la Kihistoria kwa Ulimwengu* (Julai 14, 1964).

Lazima tujue vyema namna ya kuwapambanua makada. Tusifanye uamuzi wetu juu ya wakati mfupi au tukio moja tu katika maisha ya kada, lakini lazima tuzingatie maisha yake yote na kazi yake kwa jumla. Hii ndio njia muhimu ya kupambanua makada.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Lazima tujue namna ya kuwatumia makada vizuri. Katika uchambuzi wa mwisho, viongozi wana dhamana mbili: kutoa mashauri, na kuwatumia makada. Mambo kama vile kuweka mipango, kukata maazi-

mio, na kutoa amri na maongozi n.k., yote yamo katika sehemu ya "kutoa mashauri". Ili kuyatekeleza mashauri hayo kwa vitendo, ni lazima kuwaunganisha makada na kuwahimiza wayatekeleze; haya yanakuja chini ya sehemu ya "kuwatumia makada".

Kama juu.

Lazima tuwe hodari katika kuwaangalia vizuri makada. Kuna njia kadha za kufanya hivyo:

Kwanza, wape uongozi. Hii ina maana ya kuwapa uwanja wa kuendesha kazi zao ili wawe na moyo wa kuchukua dhamana na, kwa wakati huo huo, kuwapa maongozi kwa wakati unaofaa ili, wakiongozwa na msimamo wa kisiasa wa Chama, waweze kutumilia vilivyo juhudi yao ya kuanza mambo.

Pili, inua daraja yao. Hii ina maana ya kuwaelimisha kwa kuwapa fursa ya kusoma ili waweze kuzidisha fahamu yao ya nadharia na uwezo wao wa kazi.

Tatu, kagua kazi yao, na wasaidie kukusanya maarifa yao, kupeleka mbele mafanikio yao na kusahihisha makosa yao. Kutoa kazi bila ya kufanya ukaguzi na kutanabahi wakati makosa makubwa yameshafanywa — hiyo sio njia ya kuwaangalia vyema makada.

Nne, kwa jumla, tumia njia ya kuwashawishi makada waliofanya makosa, na wasaidie kusahihisha makosa yao. Njia ya mapigano itumiwe kwa wale tu waliofanya makosa makubwa na juu ya hivyo wanakataa kuongozwa. Hapa subira ni kitu cha lazima. Ni makosa kuwapiga watu chapa ya "upotovu" kwa wepesi au "kufanya mapigano" dhidi yao ovyo.

Tano, wasaidie katika shida zao. Makada wanapokuwa katika shida kwa sababu ya maradhi, dhiki, au matatizo ya nyumbani au mengineo, ni lazima tuhakikishe kwamba tunawaangalia kama inavyoyumkinika.

[illegible]dio namna ya kuwaangalia vyema

Kama juu.

Kundi la uongozi ambalo limeungana kikweli na limeingiliana na umma linaweza kuundwa taratibu katika mwenendo wa mapigano ya umma tu, wala sio katika hali nyingine. Katika mwenendo wa mapigano makubwa, watu waliomo katika kundi la uongozi mara nyingi haifai na wala haiwezekani kubakia katika hali moja bila ya kubadilika hata kidogo katika wakati wote wa daraja ya mwanzo, ya kati na ya mwisho; wale watu wenye harakati wanaojitokeza katika wakati wa mapigano lazima kwa wakati wote wapelekwe mbele kuchukua mahala pa wale wa mwanzo wa kundi la uongozi ambao kwa kulinganishwa wamekuwa dhaifu au wameharibika.

"Baadhi ya Masuala Kuhusu Njia za Uongozi" (Juni 1, 1943), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Kama Chama chetu hakina makada wengi wapya wanaofanya kazi kwa pamoja na kushirikiana na makada wa zamani, jihadi

yetu itasita. Kwa hivyo, makada wote wa zamani lazima wawakaribishe wale wapya kwa hamu kubwa kabisa na kuwahangaikia kwa dhati. Kweli, makada wapya wana upungufu wao. Hawajakuwamo katika mapinduzi kwa muda mrefu na hawana maarifa, na ni jambo lisiloweza kuepukika kwa baadhi yao kuja na masalio ya fikra mbovu za jamii kongwe, masalio ya fikra za ubinafsi wa mabepari wadogo. Lakini upungufu kama huo unaweza kuondoshwa kwa taratibu baada ya kuelimishwa na kuimarishwa katika mapinduzi. Ubora wa makada wapya, kama alivyosema Stalin, ni kwamba wao huwa wepesi wa kuhisi mambo mepya na kwa hivyo huwa na hamu na harakati kubwa sana — sifa ambazo baadhi ya makada wa zamani wanapungukiwa nazo. Makada wapya na wa zamani lazima waheshimiane, kila mmoja asome kutoka kwa mwenziwe na waushinde upungufu wao kwa kujifunza kutokana na yale yalio mazuri ya mwengine, ili waungane kama kitu

kimoja katika jihadi ya pamoja na kujihadhari na mwelekeo wa fikra za kufuata madhehebu.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Tuwashughulikie makada wasiokuwemo katika Chama kama tunavyowashughulikia makada waliomo katika Chama. Wapo watu wengi nje ya Chama wenye uwezo ambao lazima tusiwapuuze. Wajibu wa kila Mkoministi ni kujiondoshea tabia ya kujiweka mbali na wengine na majivuno na kufanya kazi vyema pamoja na makada wasiokuwa wanachama, wawasaidie kwa dhati, wawe na moyo mkunjufu wa kikomredi kwa makada hao na wavute juhudi zao katika jihadi kubwa ya kuzuia ushambulizi wa Japani na kulijenga taifa upya.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

30. VIJANA

Dunia ni yenu, pia ni yetu, lakini katika uchambuzi wa mwisho, ni yenu. Nyinyi vijana, mkiwa mmejaa hamasa na nguvu, maisha yenu ndio kwanza yanachanua, ni kama jua la saa mbili au tatu ya asubuhi. Matumaini yetu yapo juu yenu.

. . . .

Dunia ni yenu. Mustakbala wa China ni wenu.

Mazungumzo katika mkutano na wanafunzi na wafanya kazi wa Kichina wanaoongeza maarifa katika Moscow (Novemba 17, 1957).

Lazima tuwasaidie vijana wetu wafahamu kwamba nchi yetu bado ni masikini sana kwamba hatuwezi kuigeuza hali hii kwa

msingi katika muda mfupi, na kwamba kwa bidii za pamoja za vijana wetu na watu wetu wote, wakifanya kazi kwa mikono yao wenyewe, ndio China itaweza kuwa nchi yenye nguvu na iliyostawi katika muda wa makumi kadha ya miaka. Kuasisiwa kwa mpango wetu wa kisoshalisti kumefungua njia inayoongozea kwenye jamii inayotarajiwa ya siku za mbele, lakini kuileta jamii hiyo inahitaji kazi ngumu.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Kwa sababu ya upungufu wao wa maarifa ya kisiasa na ya kijamii, vijana wengi hawawezi kuona vyema tofauti baina ya China kongwe na mpya, na si rahisi kwao kuelewa barabara shida nyingi zilizowapata watu wetu katika mapigano ya kujikomboa kutokana na ukandamizi wa mabeberu na wapinga maendeleo wa Kikuomintang, au muda mrefu wa kazi kubwa unaohitajika kabla ya kuweza kuasisiwa jamii ya kisoshalisti yenye furaha. Ndiyo maana lazima

siku zote tuendeleze elimu ya kisiasa ya hamasa na ifaayo miongoni mwa umma na siku zote lazima tuwaambie ukweli juu ya shida zinazotokea na tujadiliane nao juu ya namna ya kuzishinda shida hizo.

Kama juu.

Vijana ndio nguvu ya harakati yenye uhai kabisa katika jamii yote. Wao ndio wenye hamu kubwa ya kusoma na wasio na fikra nyingi za kung'ang'ania mambo yalio ya zamani. Jambo hilo ni kweli hasa katika zama za usoshalisti. Tunatumai kwamba matawi ya kienyeji ya Chama katika mahala mbali mbali yatayasaidia na kufanya kazi pamoja na matawi ya Umoja wa Vijana na kuzingatia suala la kufanya nguvu, hususan za vijana, kutumika kwa kikomo chake. Matawi ya Chama yasiwaangalie vijana kama yanavyowaangalia wengine na kuzipuuza tabia zao maalum. Bila ya shaka, vijana lazima wasome kutoka kwa wazee na watu wazima, na wapiganie kama inavyoyumkinika

kukubaliwa nao kujishughulisha na mambo yote yenye faida.

Maelezo ya utangulizi katika "Kikosi cha Kazi za Ghafla cha Vijana wa Chama cha Ushirika cha Watoaji Kilimo No. 9 Katika Mji Mdogo wa Hsinping, Mudiria ya Chungshan" (1955).

Vipi tuamue kama kijana ni mwana-mapinduzi au la? Vipi tunaweza kuwa-pambanua? Uko mpambanuo mmoja tu, nao ni, kama yuko tayari au la kujichanga-nyisha na umma mkubwa wa wafanya kazi na wakulima na anafanya hivyo kwa vitendo. Ikiwa yuko tayari kufanya hivyo na anafanya hivyo kwa vitendo, yeye ni mwana-mapinduzi; kama si hivyo basi si mwana-mapinduzi au mpinga mapinduzi. Ikiwa leo anajichanganyisha na umma wa wafanya kazi na wakulima, basi leo yeye ni mwana-mapinduzi; ikiwa kesho atasita kufanya hivyo au kugeukia kuwakandamiza

watu wa kawaida, basi atakuwa si mwana-mapinduzi au mpinga mapinduzi.

"Muelekeo wa Vugu Vugu la Vijana" (Mei 4, 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Wataalamu mara nyingi huwa wanayaangalia mambo kwa jinsi wanavyoyafikiria wenyewe tu na huwa na ubinafsi, fikra zao huwa haziambatani na hali hasa ya mambo na si imara katika vitendo vyao mpaka wanapojiingiza kwa moyo wao wote katika mapigano ya kimapinduzi ya umma, au wamekata shauri kuyatumikia maslaha ya umma na kuwa kitu kimoja na umma. Kwa hivyo, ijapokuwa umma mkubwa wa wataalamu wa kimapinduzi katika China wanaweza kuchukua sehemu ya kuwa mbele na kuwa kama daraja, lakini si wote wataoweza kuwa wana-mapinduzi mpaka mwisho. Baadhi yao watatoka katika safu za wana-mapinduzi katika nyakati ngumu za kimapinduzi na kuwa watepetevu, ilhali wachache huenda hata wakawa maadui wa mapinduzi. Wataalamu wanaweza kuushinda upungufu

wao huu katika mapigano ya umma tu kwa muda mrefu.

"Mapinduzi ya China na Chama cha Kikoministi cha China" (Desemba 1939), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Mbali na kuendelea na kushirikiana na Chama katika kazi yake kuu, Umoja wa Vijana unataka ufanye kazi yake wenyewe inayofaa tabia maalum za vijana. China mpya lazima iwatunze vijana wake na kuushughulikia ukuaji wa kizazi cha vijana. Vijana inawapasa kusoma na kufanya kazi, lakini wamo katika umri wa ukuaji wa kiwiliwili. Kwa hivyo, kazi na masomo yao na pia starehe, michezo ya riadha na mapumziko yao, yote haya yaangaliwe kwa ukamilifu.

Maongozi katika upokeaji wa Kikundi cha Wenyekiti cha Mkutano wa Pili wa Taifa wa Umoja wa Vijana (Juni 30, 1953).

31. WANAWAKE

Katika China wanaume kwa kawaida huelemewa na taratibu tatu za utawala [utawala wa kisiasa, utawala wa koo za jadi moja na utawala wa kidini — mtengenezaji] . . . . Kuhusu wanawake, zaidi ya kutawaliwa na taratibu hizi tatu za utawala, wao vile vile wanatawaliwa na wanaume (utawala wa waume zao). Utawala wa aina nne hizi — utawala wa kisiasa, koo za jadi moja, kidini na wa waume — ni mambo yanayowakilisha fikra na mpango mzima wa kimwinyi wa kuumeni na mambo haya ni kamba nne nene zinazowafunga watu wa China, hususan wakulima. Imeshaelezwa hapo juu vipi wakulima waliupindua utawala wa mabwana-shamba. Utawala wa kisiasa wa mabwana-shamba ni uti wa mgongo wa taratibu zote nyenginezo za utawala. Kwa

kuangushwa chini utawala wa kisiasa wa mabwana-shamba, utawala wa koo za jadi moja, utawala wa kidini na wa waume, namna hizi zote za utawala zikaanza kutikisika. ... Kuhusu utawala wa waume, jambo hili siku zote lilikuwa dhaifu kidogo miongoni mwa wakulima masikini kwani kwa kutokana na mahitajio ya kiuchumi, akina mama wao iliwabidi wafanye kazi zaidi kuliko wanawake wa matabaka matajiri na kwa hivyo wana satwa zaidi katika kutoa maoni na kukata shauri mambo ya ukoo. Kuengezeka kufilisika uchumi wa mashambani katika miaka ya karibuni kumeleta kuvunjwa msingi wa utawala wa waume juu ya wake zao. Na hivi karibuni kwa kutokeza vugu vugu la wakulima, wanawake wa mwahala mwengi wameanza kuasisi jumuia za wanawake za mashambani; fursa ya kunyanyua juu vichwa vyao imekuja, na utawala wa waume umo kutikisika zaidi na zaidi kila kukicha. Kwa ufupi, fikra na mpango wote wa kimwinyi wa kuumeni

umo kutikisika kila nguvu za wakulima zinapoengezeka.

"Ripoti Juu ya Uchunguzi wa Vugu Vugu la Wakulima wa Hunan" (Machi 1927), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Unganeni na mshiriki katika kazi za uchumi na nyenendo za siasa ili mnyanyue juu daraja ya wanawake katika mambo ya uchumi na siasa.

Maneno ya pongezi kwa Gazeti la *Wanawake wa China Mpya* lililochapwa katika toleo la kwanza, Julai 20, 1949.

Yahifadhini maslaha ya vijana, wanawake na watoto — toeni msaada kwa vijana waliokosa masomo, wasaidie vijana na wanawake kujikusanya ili washiriki kwa hali moja na wengine katika kazi zote za manufaa kwa ajili ya juhudi za Vita vya Kupinga Ushambulizi wa Japani na kuleta maendeleo ya jamii, kuhakikisha uhuru wa kuoana na usawa baina ya wanawake na

wanaume, na kuwapa vijana na watoto elimu ya manufaa. . . .

"Juu ya Serikali ya Muungano" (Aprili 24, 1945), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Jukumu letu la msingi kabisa katika kazi zetu za kilimo ni kuyarekibisha matumizi ya nguvu za kazi kwa njia ya mpango na kuwahimiza wanawake washiriki kufanya kazi kondeni.

"Siasa Yetu ya Uchumi" (Januari 23, 1934), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Kwa ajili ya kujenga jamii kubwa ya kisoshalisti, ni muhimu sana kuuamsha umma mkubwa wa wanawake waingie katika kazi za uchumi. Wanaume na wanawake lazima wapate mshahara sawa kwa kazi sawa katika uchumi. Usawa wa kweli baina ya wanaume na wanawake hauwezi kupatikana isipokuwa katika mwenendo wa

mabadiliko ya kisoshalisti ya jamii yote kwa jumla.

Maelezo ya utangulizi katika "Wanawake Wamekwenda Kwenye Medani ya Kazi" (1955).

Baada ya kukamilishwa ushirika wa kilimo, vyama vyingi vya ushirika vinajiona vina upungufu wa nguvu za kufanya kazi. Imekuwa ni lazima kuamsha umma mkubwa wa wanawake ambao kabla hawakufanya kazi kondeni kuchukua mwahala pao katika medani ya kazi. . . . Wanawake wa China ni hazina kubwa ya nguvu za kazi. Hazina hii inataka itumike katika mapigano ya kujenga nchi kubwa ya kisoshalisti.

Maelezo ya utangulizi katika "Waamshe Wanawake Kushiriki Katika Kazi za Uchumi na Kutanzua Matatizo ya Upungufu wa Nguvu za Kazi" (1955).

Muwezeshe kila mwanamke anayeweza kufanya kazi kuchukua mwahala pake katika medani ya kazi, kwa kanuni ya mshahara

sawa kwa kazi sawa. Jambo hili linataka lifanywe kwa upesi kama inavyoyumkinika.

Maelezo ya utangulizi katika "Mpango wa Jumuia ya Wanawake ya Kidemokrasi ya Mudiria Hsin Tai Juu ya Kuengeza Kiwango cha Kazi za Wanawake Katika Vugu Vugu la Ushirika wa Kilimo" (1955).

32. UTAMADUNI NA SANAA

Katika dunia ya leo, utamaduni wo wote, uandishi wo wote na sanaa yo yote ni ya matabaka maalum na inaelekezwa kwenye msimamo maalum wa kisiasa. Kusema kweli, hapana kitu kiitwacho sanaa kwa ajili ya sanaa, sanaa isiohusika na matabaka au sanaa inayotengana au isiofungamana na siasa. Uandishi na sanaa za kifanya kazi ni sehemu ya jihadi yote ya kimapinduzi ya tabaka la kifanya kazi; vitu hivi, kama Lenin alivyosema, ni "meno ya gurudumu na skrubu" katika mashine yote ya kimapinduzi.

"Mazungumzo Katika Mkutano wa Yenan wa Mambo ya Uandishi na Sanaa" (Mei 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Utamaduni wa kimapinduzi ni silaha yenye nguvu ya kimapinduzi kwa ajili ya umma mkubwa wa watu. Utamaduni wa kimapinduzi unatayarisha mawazo ya kimapinduzi kabla ya kuja mapinduzi na ni medani muhimu na ya lazima katika medani ya jumla mnamo wakati wa mapinduzi.

"Juu ya Demokrasi Mpya" (Januari 1940), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Uandishi na sanaa zetu zote ni kwa ajili ya umma wa watu; kwanza kabisa ni kwa ajili ya wafanya kazi, wakulima na wanajeshi; zinatungwa kwa ajili ya wafanya kazi, wakulima na wanajeshi na kwa ajili ya matumizi yao.

"Mazungumzo Katika Mkutano wa Yenan wa Mambo ya Uandishi na Sanaa" (Mei 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Wafanya kazi wetu wa mambo ya uandishi na sanaa lazima waitimilize kazi hii na waubadilishe msimamo wao; lazima hatua baada ya hatua waiondoshe miguu yao na kuipeleka kwenye upande wa wafanya kazi, wakulima na wanajeshi, yaani kwenye upande wa tabaka la wafanya kazi, kwa kupitia mwenendo wa kuingiliana nao kikweli kweli na kuingia kwenye mapigano hasa na kuusoma Umarx na kuisoma jamii. Ni kwa njia hii tu ndio tunaweza kuwa na uandishi na sanaa zilizo kweli kwa ajili ya wafanya kazi, wakulima na wanajeshi, yaani uandishi na sanaa zilizo za kifanya kazi hasa.

Kama juu.

Inatubidi tuhakikishe kwamba kazi za uandishi na sanaa ziwe ni sehemu inayofaa vyema katika mashine yote ya kimapinduzi, kwamba vitu hivi viwili viwe ni silaha zenye nguvu katika kuunganisha na kuelimisha umma na katika kumshambulia na kumbomoa adui na viwe vinasaidia umma

katika kupigana na adui kwa moyo mmoja na akili moja.

Kama juu.

Utoaji makosa wa uandishi na sanaa una vipimo viwili: kipimo cha kisiasa na kipimo cha kisanaa. . . .

Ilivyokuwa kuna kipimo cha kisiasa na kipimo cha kisanaa, nini, basi, mahusiano baina ya vipimo hivi viwili? Siasa haiwezi kuwekwa sawa sawa na sanaa kama vile ilivyokuwa mtizamo wa jumla kuhusu ulimwengu hauwezi kufanywa kuwa sawa sawa na njia ya utungaji wa kisanaa na utoaji makosa wa kisanaa. Sisi si kama tunakataa tu kwamba kipo kipimo kisichoonekana na kisichoweza kubadilika kabisa cha kisiasa bali tunakataa vile vile kwamba kipo kipimo kisichoonekana na kisichoweza kubadilika kabisa cha kisanaa; kila tabaka, katika kila jamii ya matabaka, lina kipimo chake wenyewe cha kisiasa na kisanaa. Lakini tabaka lo lote, katika jamii yo yote yenye matabaka, linaweka mbele kipimo cha kisiasa na kuweka kipimo cha kisanaa

mwahala pa pili. . . . Jambo tunalolitaka sisi ni umoja wa siasa na sanaa, umoja wa maana na umbo, umoja wa maana ya kisiasa ya kimapinduzi na umbo la kisanaa linalokamilika kabisa kama inavyoyumkinika. Kazi za kisanaa zenye upungufu wa sifa za kisanaa hazina nguvu, hata zikiwa ni za kimaendeleo namna gani kwa kisiasa. Kwa hivyo, tunapinga kazi za sanaa zenye maoni ya makosa ya kisiasa kama vile tunavyopinga mwelekeo wa kuendea kwenye "mtindo wa mabango yenye maneno na kutoa miito" — mwelekeo ambao ni barabara kwa maoni ya kisiasa lakini una upungufu wa nguvu za kisanaa. Katika suala la uandishi na sanaa, lazima tufanye jihadi kwenye medani mbili.

Kama juu.

Kuyawachia maua mia yachanue na aina mia za mawazo yapambane ni siasa ya kupeleka mbele maendeleo ya sanaa na sayansi na kustawisha utamaduni wa kisoshalisti katika nchi yetu. Aina na mitindo mbali mbali ya sanaa inaweza kuendelea

kama itakavyo na fikra za aina mbali mbali katika sayansi kupambana bila ya vipingamizi. Tunafikiria ni jambo lenye madhara kwa ukuaji wa sanaa na sayansi ikiwa hatua za kiserikali zitachukuliwa kutilia nguvu mtindo fulani wa sanaa na aina fulani ya mawazo na kupiga marufuku nyengineo. Masuala ya usahihi au makosa katika mambo ya sanaa na sayansi yanataka yatanzuliwe kwa njia ya majadiliano huru miongoni mwa wana-sanaa na wana-sayansi kwa njia ya kufanya kazi hasa katika mambo haya. Yasitanzuliwe kwa njia ya kukata shauri kwa mkato tu.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Jeshi lisilokuwa na utamaduni ni jeshi la kijinga na jeshi la kijinga haliwezi kumshinda adui.

"Muungano wa Pamoja Katika Kazi ya Utamaduni" (Oktoba 30, 1944), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

33. MASOMO

Katika kuigeuza China iliyo nyuma inayotegemea kilimo kuwa nchi iliyoendelea mbele katika kazi za makarahana, tunakabiliwa na kazi ngumu sana na maarifa yetu yako mbali na kutosha. Kwa hivyo lazima tuwe mahodari katika kusoma.

"Hotuba ya Ufunguzi Katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Kitaifa wa Chama cha Kikoministi cha China" (Septemba 15, 1956).

Hali ya mambo inabadilika kila wakati, na ili kuzifanya fikra za mtu ziambatane na hali mpya ya mambo, lazima mtu asome. Hata wale wanaofahamu vizuri Umarx zaidi na kwa kulinganishwa ni imara katika msimamo wao wa kifanya kazi, vile vile inawabidi kuendelea kusoma, kuyatia

kichwani yalio mepya na kusoma kwa makini matatizo mepya.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Tunaweza kujifunza yale tusiyoyajua kabla. Sisi sio mahodari katika kuibomoa dunia kongwe tu, bali vile vile ni mahodari katika kuijenga dunia mpya.

"Ripoti Katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Kamiti Kuu ya Saba ya Chama cha Kikoministi cha China" (Machi 5, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Kuna tabia mbili tofauti za kusoma. Moja ni ile tabia ya kufuata mambo kikasuku ya kupandikiza kila kitu, ikiwa kinafaa kwa hali ya nchi yetu au hakifai. Tabia hii si nzuri. Tabia nyengine ni kutumia akili zetu na kusoma mambo ambayo yanawafikiana na hali zetu, yaani kuchukua maarifa yote

ambayo yana faida kwetu. Hiyo ndio tabia inayotaka tuichukue.

Juu ya Kutanzua kwa Usahihi Hitilafu Miongoni mwa Umma (Februari 27, 1957).

Nadharia ya Marx, Engels, Lenin na Stalin inafaa po pote pale katika dunia nzima. Tusiichukulie kuwa ni ya kufuatwa kikasuku, bali kama dira ya kuongoza vitendo vyetu. Kuusoma Umarx-lenin sio kusoma maneno na vipande vya maneno yake tu bali kuusoma kama ni sayansi ya mapinduzi. Si kama lazima kufahamu tu kanuni za kawaida zilizofikiliwa na Marx, Engels, Lenin na Stalin baada ya wao kuyasoma kwa makini maisha hasa na maarifa ya kimapinduzi kwa vilivyo, bali vile vile lazima kusoma msimamo wao na njia yao ya kuchungua na kutanzua matatizo.

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Ikiwa tunayo nadharia sahihi lakini tufanyalo ni kuizungumza tu, tunaifungia ndani na hatuitekelezi kwa vitendo, basi nadharia hiyo, hata ikiwa nzuri namna gani, haina maana yo yote.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Ni jambo la lazima kuielewa vyema nadharia ya Umarx na kuitumia, kuielewa vyema kwa madhumuni ya kuitumia tu. Ikiwa unaweza kutumia mtizamo wa Umarx-lenin katika kufafanua tatizo moja au mawili ya mambo hasa, inafaa usifiwe na kupewa heshima ya kupata mafanikio machache. Kila ukifafanua matatizo mengi zaidi kwa ukamilifu zaidi na kwa maana kubwa zaidi, mafanikio yako yatakuwa makubwa zaidi.

"Masahihisho ya Mtindo wa Kazi za Chama" (Februari 1, 1942), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu III.

Vipi kufungamanisha nadharia ya Umarx-lenin na vitendo vya mapinduzi ya China? Kutumia msemo wa kawaida, ni kwa "kupiga mshale kwenye shabaha". Kama mshale ulivyo kwa shabaha basi ndivyo Umarx-lenin ulivyo kwa mapinduzi ya China. Juu ya hivyo, baadhi ya makomredi "wanapiga mshale bila ya shabaha", wanapiga ovyo, na watu kama hao wanaweza kuyadhuru mapinduzi.

Kama juu.

Wale wenye maarifa ya kazi lazima wasome nadharia na wasome kwa bidii; ni hapo tu ndio wataweza kuyapanga uzuri na kuyaunganisha maarifa yao na kuyainua kufikia daraja ya nadharia, ni hapo tu ndio hawatofanya kosa la kufikiria maarifa yao yasiyokamilika kuwa ni ukweli unaofaa po pote na hawatofanya makosa ya kutegemea maarifa ya zamani tu.

Kama juu.

Kusoma ni kujifunza, lakini kutekeleza pia ni kujifunza na ndio aina muhimu zaidi ya kujifunza. Njia yetu kuu ni kujifunza mambo ya vita kwa kuwemo katika vita. Mtu ambaye hajapata fursa ya kwenda skuli naye pia anaweza kujifunza habari ya vita — anaweza kujifunza kwa kupigana katika vita. Vita vya kimapinduzi ni jambo la umma; aghlabu si jambo la kujifunza kwanza na halafu kutenda, bali la kutenda na halafu kujifunza, kwani kutenda peke yake ndio kujifunza.

"Matatizo ya Hila ya Jumla Katika Vita vya Kimapinduzi vya China" (Desemba 1936), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Kuna pengo baina ya raia wa kawaida na mwanajeshi, lakini pengo hili si Ukuta Mkuu, na linaweza kuzibwa kwa haraka, na njia ya kuliziba ni kushiriki katika mapinduzi, katika vita. Kwa kusema kwamba si rahisi kujifunza na kutekeleza, tunakusudia kwamba ni taabu kujifunza kwa ukamilifu na kutumia kwa ustadi. Kwa

kusema kwamba raia wanaweza kuwa wanajeshi kwa haraka, tunakusudia kwamba si taabu kukikiuka kizingiti. Ili kuyaunganisha maneno haya mawili, tunaweza kutumia ule msemo maarufu wa Kichina, "Hapana kitu kilichokuwa cha taabu duniani kwa yule mtu aliyekiazimia." Kukikiuka kizingiti si taabu, na ustadi pia, mtu anaweza kuwa nao kama ameazimia kuifanya kazi hiyo na ni hodari katika kusoma.

Kama juu.

Lazima tujifunze kazi ya uchumi kutokana na wote wenye ujuzi huo (bila ya kujali ni mtu gani). Lazima tuwaheshimu kama waalimu, tujifunze kutoka kwao kwa adabu na kwa bidii. Tusijidai kujua ikiwa hatujui.

"Juu ya Udikteta wa Kidemokrasi wa Umma" (Juni 30, 1949), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu IV.

Ujuzi ni jambo la sayansi, na udanganyifu na majivuno ya namna yo yote hayaruhusiki. Kinachotakiwa bila ya shaka ni kinyume cha hivyo — uaminifu na unyenyekevu.

"Juu ya Vitendo" (Julai 1937), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu I.

Fikra ya kutoshelezeka ni adui wa masomo. Hatuwezi kusoma kitu cho chote kwa ukweli mpaka tujiondoshee fikra ya kutoshelezeka. Tabia yetu juu yetu sisi wenyewe inataka iwe "kutokinai kujifunza" na kwa watu wengine "kutochoka kusomesha".

"Madaraka ya Chama cha Kikoministi cha China Katika Vita vya Kitaifa" (Oktoba 1938), *Maandishi Yaliyoteuliwa*, Juzuu II.

Baadhi ya watu wamesoma mabuku machache ya Umarx na wanajifikiria kwamba wamekuwa wajuzi, lakini waliyoyasoma hayajawaingia vichwani mwao, hayajaota mizizi katika ubongo wao, kwa hivyo

hawajui namna ya kuyatumia na hisia zao za tabaka zimebaki kuwa kama zamani. Wengine wanajivuna sana, na baada ya kujifunza vipande vichache vya maneno kutoka katika kitabu wanajifikiria hapana kama wao na wajuvi sana; lakini dharuba inapotokea, wanachukua msimamo tofauti kabisa na ule wa wafanya kazi na wingi wa wakulima. Wao huyumba yumba wakati wafanya kazi na wakulima husimama imara, na hubabaisha maneno wakati wafanya kazi na wakulima husema kinaga ubaga.

Hotuba Katika Mkutano wa Taifa Juu ya Kazi za Uenezi Siasa wa Chama cha Kikoministi cha China (Machi 12, 1957).

Ili kuelewa kikweli Umarx, mtu sio ajifunze kutoka katika vitabu tu, bali lazima ajifunze hasa kwa kupitia mapigano ya kitabaka, kupitia kazi hasa na maingiliano ya karibu na umma wa wafanya kazi na wakulima. Ikiwa wataalamu wetu, zaidi ya kusoma baadhi ya vitabu vya Umarx, wamepata ufahamu kidogo kwa kupitia

maingiliano ya karibu na umma wa wafanya kazi na wakulima na kwa kupitia kazi yao wenyewe hasa, basi sisi sote tutakuwa tunasema lugha moja, sio lugha moja ya kupenda nchi na lugha moja ya mpango wa kisoshalisti tu, lakini inawezekana hata kusema lugha moja ya mtizamo wa kilimwengu wa kikoministi. Ikiwa jambo hilo litatokea, basi ni hakika kwamba sisi sote tutafanya kazi vyema sana zaidi.

Kama juu.

毛 主 席 语 录

*

外文出版社出版（北京）
1972年版
编号：（斯）1050—570
00077
1—Sa—734Pc